ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini.
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni.
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais.
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu.
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais.
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.

12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais.
13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/\Jimbo la Jang'ombe.
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.

23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake.
32.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais

37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
58.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
65.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
66.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
70.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
71.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Tano – Tarehe 28 Januari, 2014

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani hotuba ya kuwasilisha ripoti ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya mwaka 2012/2013.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba na mimi kwa ruhusa yako kuwasilisha mezani hotuba ya kuwasilisha ripoti ya utekelezaji kwa maagizo ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya mwaka 2012/2013.

Naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto (Kny: Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali): Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani hotuba ya kuwasilisha ripoti ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya mwaka 2012/2013.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naweka hati mezani Muhtasari wa Hotuba ya Ripotiya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya mwaka 2013/2014.

Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 42

Operesheni ya Kuweka Mji Safi Kutozingatia Haki za Binaadamu kwa Mujibu wa Katiba

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Operesheni ya kuweka mji safi zinazofanywa na askari wa Vikosi vya SMZ na watendaji wa Baraza la Manispaa, zinaonekana kuwa na mapungufu kadhaa ya msingi; ikiwemo kutozingatiwa misingi ya kikatiba inayotaka wananchi kufanya kazi na kujipatia riziki na kipato halali.

Hali hii imewaathiri wafanyabiashara wadogo wadogo kadhaa wa maeneo mbali mbali hasa eneo la Darajani, Mjini Zanzibar, wakiwemo wauza mikate ambao kutokana na mapungufu ya operesheni hizo, wamekuwa wakifanya biashara zao hizo, zinazowasaidia kujipatia riziki halali wao na familia zao, kwa hofu na kujificha.

(a) Je, kwa nini operesheni hizo zinawadhibiti wauza mikate badala ya wauza madawa ya kulevya, na kupelekea wauza mikate hao wafanye biashara hiyo kwa wasiwasi na hofu jambo ambalo ni kinyume na Katiba.

(b) Kwa nini wauza mikate hawa wanyonge, masikini, huwa wananyang'anywa mikate yao na askari wa Manispaa, halafu hawarejeshewi. Je, mikate hiyo, wanaponyang'anywa huwa inapelekwa wapi. Huu si uvunjaji wa haki za binaadamu mtu kunyang'anywa mali yake na kupotea katika mazingira yasiyoeleweka.

(c) Kwa nini Baraza la Manispaa linawasumbuwa na kuwakamata wauza mikate wakati wanalipa ada mbali mbali za usafi na kadhalika. Kufanya hivyo si sawa na kuwapa haki ya kufanya biashara zao kwa mkono wa kulia na kuwapokonya haki hiyo kwa mkono wa kushoto.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako na kabla ya kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake namba 42 lenye kifungu a, b na c naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, sikubaliani na maelezo ya awali kuwa operesheni za kuweka Mji safi zinafanywa na Vikosi vya SMZ, shughuli za uwekaji Mji safi ni kazi za kawaida za Baraza la Manispaa pamoja na wakaazi waliopo katika eneo la Manispaa. Aidha, sikubaliani na maelezo yake kuwa askari wa Vikosi vya SMZ hawazingatii misingi ya Katiba wakati wa utekelezaji wa kazi zao.

Mhe. Spika, ufanyaji biashara na usafi wa Mji, unasimamiwa na Sheria na Kanuni za Manispaa, lakini kwa bahati mbaya baadhi ya wananchi huwa hawataki kuzifuata hata wanapoeleweshwa juu ya Sheria na Kanuni hizo. Naomba pia ieleweke kuwa Sheria na Kanuni hizo zinazingatia mahitaji ya matumizi ya Mji kwa makundi yote wakiwemo wao wafanyabiashara, wanafunzi, watalii na watu mbali mbali wanaofuata huduma mbali mbali katika Mji wa Zanzibar.

Hivyo, likitokea kundi moja kati ya hayo likafanya mambo kinyume na utaratibu linaathiri makundi mengine. Mfano mmoja wa kundi linaloathirika ni wanafunzi wanaosoma katika Skuli ya Darajani na Vikokotoni kunakosababishwa na ghasia, lugha za kihuni zinazotolewa na baadhi ya wafanyabiashara hao, makonda wa daladala pamoja na wapiga debe.

Mhe. Spika, hali ya kutotii Sheria, Kanuni na taratibu husababisha vurugu na kuondosha haiba nzuri ya mji wetu, na inapotokea hali hiyo ndio hulazimika vikosi vyetu kuwepo katika maeneo ya Darajani kwa ajili ya kuhakikisha kuwa Sheria, Kanuni na taratibu zinafuatwa.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 42 kama ifutavyo:-

a) Operesheni ya kuwakamata wafanyabiashara wadogo wadogo wakiwemo wauza mikate ilifanywa kwa mujibu wa Sheria ndogo ndogo za Manispaa ili kudhibiti ufanyaji wa biashara kinyume na maelekezo ya kufanya biashara ndani ya Mji kisheria. Kuhusu madawa ya kulevya, Baraza la Mji halitoi vibali kwa wauza madawa ya kulevya, pia kuuza dawa za kulevya ni kosa la jinai. Kwa hivyo, hatuwezi kuhusika katika kuhalalisha kufanyika kwa biashara hiyo. Aidha, namuomba Mhe. Mwakilishi kama anawaelewa

wafanyabiashara wa Madawa ya kulevya katika eneo la Darajani na sehemu nyengine atoe taarifa katika vyombo husika ili wachukuliwe hatua kisheria.

b) Bidhaa zote zinazokamatwa na Askari wa Manispaa katika Operesheni yoyote huwasilishwa Mahakama ya Mwanzo Malindi iliyopo ndani ya Jengo la Manispaa kwa hatua za kisheria. Iwapo muhusika hakujitokeza baada ya mali yake kukamatwa bidhaa hizo huhifadhiwa ghalani kwa muda wa siku 14, baada ya hapo mali hizo huuzwa kwa usimamizi wa Mahakama. Hadi sasa hatuna mtu aliyeripoti katika Baraza la Manispaa akidai kuchukuliwa kwa mikate yake, na kama Mhe. Mwakilishi anao watu waliomlalamikia naomba atuwasilishie orodha ya watu hao ili tuweze kulichunguza jambo hilo kwa kushirikiana na wahusika wengine.

c) Baraza la Manispaa haliwasumbui na kuwakamata ovyo wafanyabiashara wadogo wadogo wakiwemo wauza mikate, bali inasimamia taratibu, kanuni za Sheria ndogo ndogo za Manispaa zilizoundwa chini ya Sheria ambayo Baraza lako tukufu imeipitisha na kuipa baraka zote. Mfanyabiashara anatakiwa afanye biashara kwa mujibu wa masharti ya leseni yake na leseni wanazokata wauza mikate ni za kutembeza mikate na sio kuwa duka la mikate katika eneo ambalo halikuruhusiwa kisheria.

Hivyo, hakuna mfanyabiashara anayetembeza mikate katika Mji wa Zanzibar akiwa na leseni akakamatwa. Isipokuwa kama wakijichanganya na wafanyabiashara wanaofanya biashara katika eneo la Darajani kinyume na utaratibu uliowekwa wataondolewa kama wafanyabiashara wengine wasiofuata utaratibu wanavyoondolewa. Sote tunakubaliana kuwa wafanyabiashara wote walioko Darajani wanatafuta rizki halali, katika kutafuta rizki halali wanapaswa kufanya hivyo kwa kufuata taratibu katika maeneo yaliyopangwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri ya kusikitisha naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(a) Wafanyabiashara kuondolewa katika eneo la Darajani na kubaki kuzagaa katika eneo la Kisiwandui na Jamhuri Garden ni kuhifadhi mji au kuendeleza mji.

(b) Wafanyabiashara wa mikate tokea asili huko tunakotoka walikuwa wakiuza mikate, na kwa kweli wale hawahusiki na Skuli ya

Vikokotoni wala Darajani wala hawana bughudha kimazingira wala uchafuzi, unatoa kauli gani kuhusu suala hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, swali lake la (a) naomba alirejee, lakini naomba kumjibu swali la (b).

(b) Kama nilivyosema kwenye jibu langu mama naomba kumjibu Mheshimiwa kwamba, wafanyabiashara wa mikate ni wafanyabiashara wanaopewa leseni za kutembeza biashara sio biashara za kuweka kituo cha kuweka mikate. Kama wafanyakazi wa Manispaa walikuwa wanawavumilia ni kuwavumilia tu, lakini ni kinyume na utaratibu, kama mfanyabiashara yoyote hasa hawa wenzetu ambao wanafanya biashara ya mikate kutumia baskeli zao ni lazima wafuate utaratibu.

Biashara za mikate ni za kutembeza vyenginevyo kama unataka uwe na kituo basi uwe na duka la kuuzia mikate na yapo maduka ya kuuzia mikate. Lakini kama unachukua mikate kwenye susu na baskeli leseni yako inakuwa ni ya kutembeza, biashara hiyo sawa sawa na wauza dagaa, samaki na wauza embe na madafu, hawatakiwi wasimame kwenye kituo kimoja.

Kwa hiyo, kufanya hivyo sio kuwaonea wala kuvunja haki za binadamu wala katiba, utaratibu ni kufuata sheria. Hivyo, nakuomba sana Mhe. Mwakilishi kwamba utetezi wako wa kutaka wafanyabiashara wavunje sheria hautakubalika na haukubaliki. Wafanyabiashara wauza mikate nawasihi sana wafuate utaratibu kisheria, wanapewa leseni au vibali vya kutembeza mikate watembeze mikate, kama Mhe. Jaku Hashim unakaa pale nyumbani kwako na kama una mteja wako maalum akupitishie nyumbani kwako kukuuzia mikate, lakini sio aweke katika kituo ambacho hakijaruhusiwa. Naomba rejea swali la (a).

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: (a) Mhe. Waziri anaposema mtu akate leseni ya duka mlango wa duka gharama zake ni kubwa kuendesha na mkate faida yake ni sentí 20 au 50. Haoni anawanyima haki wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika: Hilo sio swali lako la kwanza, tunaendelea tuliache hili sio swali lake la kwanza, kabadilisha na hakuna utaratibu wa kuuliza mara mbili. *(Kicheko)*

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi asubuhi hii kuweza kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Waziri. Mhe. Waziri ametueleza sheria jinsi gani vibali vinavyotoka kwa wauza mikate. Je, ikiwa kama mimi ni muuzaji nikawa ninakwenda hivi nikirudi hivi, sheria hiyo inanikubali.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwenda na kurudi katika eneo lisilozidi mita 50 itakuwa ni kufanya ujanja, kinachotakiwa wewe utembeze usikae katika eneo moja. Kwa hivyo, kwenda na kurudi kwa mfano unatoka mwanzo wa soko mpaka mwisho wa soko unafanya ujanja tu ili uonekane unatembea. Ruhusa uliyopewa urande katika eneo kubwa zaidi linalovuka zaidi ya mita 10 na kuendelea.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kunipa fursa na mimi nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza. Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri lakini wafanyabiashara wa mikate kwanza hawako kule kwenye skuli wako upande wa pili, na tangu zamani tunawaona kama wauza mikate Darajani wapo, na kwa kuwa wauza mikate si wachafuzi wa biashara na mtu akiwa anatembeza anatakiwa atembeze lakini apate kituo ili wafanyabiashara wajue kwamba kituo fulani tukifika mikate tutaipata na hao ndivyo wanavyofanya, wanatembeza baadae wanakuja Darajani wanakaa kwa sababu wanajua hapa tushazoeleka upande wa pili wanauza mikate yao.

Je, kuwafukuza si kuwanyima haki na wakati serikali inahimiza kupunguza umasikini na watu kujiajiri wenyewe. Hilo moja.

La pili, Mhe. Waziri amesema kwamba wanapokamatwa mikate yao ikichukuliwa au kitu chochote kikichukuliwa kinakaa kwa muda wa siku sita baadae vinapigwa mnada wa serikali. Ni kiasi gani cha fedha kimekusanywa kutokana na mauzo hayo ya vitu vinavyochukuliwa kwa wafanyabiashara hao.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, katika mji wa Zanzibar, Manispaa yote inaruhusiwa kufanywa biashara kwa kufuata taratibu na sheria zilizowekwa, hakuna upande wa pili wala wa kwanza, ukifanya biashara kinyume na utaratibu unastahiki kuchukuliwa hatua. Kwa hiyo eneo la upande wa pili wanakokaa wafanyabiashara wa mikate nalo linatakiwa lifuate utaratibu ule ule na sheria za mji.

Mhe. Spika, alisema pia kuhusu kuwaondosha wafanyabiashara. Nakubali kwamba wao wanaweza wasiwe sehemu ya kuwakera wanafunzi, lakini nao

kwa upande mmoja wanavunja sheria ya kufanya biashara pahala ambapo hapastahiki kufanya biashara. Hiki ndicho kilichowaondosha wao, hakikuwaondosha kile tu peke yake, lile jibu lilikuwa ni jibu la jumla kuhusu operesheni ya Darajani. Lakini serikali, sisi na ilani yetu imesema wazi kwamba, tutahakikisha tunatafuta namna ya kuweza kuwapunguzia umasikini wananchi wetu.

Mhe. Spika, kufanya biashara ya mikate na biashara nyenginezo ni moja kati ya fursa ambazo zinatolewa na serikali ili ziweze kuwasaidia wananchi kukuza kipato na kupunguza umasikini. Lakini bado hiyo haisababishi kupunguza umasikini kwa mfanyabiashara yoyote yule na kujiongezea kipato avunje sheria. Bado huyo anayepunguza umasikini na kuongeza kipato anatakiwa afuate utaratibu. Hapa tatizo letu ni kufuata utaratibu tu, wawe wauza mikate 1,000 au 100,000 kama watafuata utaratibu sisi hatuna tatizo nao.

Jengine ni kuwa kiasi gani kilichokusanywa katika kupiga mnada bidhaa hizi. Nataka niseme kwanza nilisema kuwa biashara ili ipigwe mnada inatakiwa ikae kwa muda wa siku 14 na sio siku sita. Hizi tarakimu za kiasi gani kimekusanywa kama kipo maana sisi hatuna kumbukumbu hizo kama kuna wafanyabiashara wengi ambao wamekamatwa na bidhaa zao hawajaja kuchukua, lakini kama kipo napenda nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba hesabu hiyo tutamletea kwa maandishi.

Nam. 43

Uchakavu wa Soko la Kuku na Matunda Darajani

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Soko la kuku na matunda hapo Darajani limekuwa ni kivutio kikubwa kwa wageni wanaotembelea hifadhi ya Mji Mkongwe, lakini wafanyabiashara wamekuwa wakifanya kazi zao katika mazingira magumu kutokana na kukithiri kwa uchafu, kuvuja na kuleta sura mbaya kwa nchi.

(a) Serikali ina mpango gani wa kulifanyia matengenezo makubwa soko hilo hasa kwa kuzingatia wafanyabiashara wamekuwa wakilipa kodi.

(b) Sehemu ya ndani kuna majengo yametengenezwa, wafanyabiashara wangapi wamenufaika na milango hiyo na wafanya biashara wangapi wapya waliopewa milango lakini hawakuwepo kabla ya kufanyika matengenezo hayo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ – Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 43 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Serikali kupitia Baraza la Manispaa imeshajipanga katika kulijenga upya soko hilo na tayari imeshatayarishwa michoro na pia imeshawasiliana na Mamlaka ya Mji Mkongwe kwa dhamira ya kupata kibali cha ujenzi, kwa kuzingatia kwamba soko hilo lipo katika eneo la Mji Mkongwe ambao una taratibu zake katika kulinda Historia iliyopo.

b) Ni kweli sehemu ya ndani lililokuwa soko la matunda kuna majengo mapya yamejengwa kwa mpango wa *Build operate Transfer (BOT)*, ambapo ujenzi huo umeweza kutengeneza jumla ya milango 16 na jumla ya wafanyabiashara 16 wamepatiwa milango ambao takriban wote ni wapya. Hali hiyo ya upya imetokana na wale wa awali waliokuwepo pahala hapo walikuwa ni wafanyabiashara ndogo ndogo wa mboga mboga, ambao wengi wao walipatiwa nafasi katika soko la mboga mboga la Mombasa na wengine katika soko la mboga mboga Darajani.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri. Nilichokuwa nikizungumza mimi ni kujua kwamba je, alikuwa anataka kulivunja soko lote zima. Kwa sababu kilichokuwepo pale kipenu kutoka mwanzo mpaka mwisho na wanalipa shilingi 1,000 kwa siku na hivi sasa nafikiri wameshazidishiwa ni shilingi 2,000 wala hawana faida. Hivi sasa lile banda vipenu vyote viko chini, mbao zishaoza linavuja, nafikiri ni kazi ya siku tatu tu ya ujenzi ule. Anatoa kauli gani Mhe. Waziri wakati wananchi wanachangia na mvua zinakaribia kufika.

La pili, kwa nini walijenga mabanda ya maduka hawakuona kuwa wamebadilisha ramani ya Mji Mkongwe, na wakati maduka yale yamejengwa kwa idhini ya Mji Mkongwe haikutoa ruhusa na baadae ndio wakenda Mji Mkongwe.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kuwepo kipenu na ubovu wa kuvujiwa wafanyabiashara ndio uliotusababisha sisi tuanze kulijenga upya soko la mboga mboga la Darajani. Tunaelewa kwamba kuna vipenu na kuna ubovu unaowafanya wafanyabiashara wasikae kwa vizuri ndio unaotusababisha sisi tuweze kulijenga upya soko la Darajani.

Fedha shilingi 2,000 zinazotolewa na wananchi hawaioni faida. Wananchi kwa ujumla hawawezi kuiona faida, lakini wafanyabiashara wanaofanya biashara wanaolipa shilingi 2,000 lazima watakuwa wanaiona faida. Kwa sababu, biashara yoyote inapotozwa ada au leseni inafanyiwa tathmini mtaji wake ni kiasi gani na yeye Mhe. Jaku Hashim ni mfanyabiashara, faida ni kiasi gani ndipo taasisi inayohusika na kutoza leseni inatoza kwa mujibu wa tathmini ambayo itakuwa imefanywa. Sasa mimi sioni kama wafanyabiashara hawaioni faida, lakini kwa hali iliyopo sasa na bei inayotozwa sasa inalingana na hiyo hali halisi ya soko lenyewe lilivyo na wakati soko litabadilika pia bei za kodi ya *slubs* zile itabadilika kulingana na mahitaji ya wakati huo.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, kunipa ruhusa kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Katika majibu yake mama alisema kuwa tayari soko hilo limeshawekwa michoro. Je, Mhe. Waziri soko hilo litagharimu kiasi gani cha fedha za Tanzania.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kama nilivyosema mwanzo kuwa suala la soko la Darajani tunataka kulijenga upya na tayari tumeshatengeneza michoro. Gharama halisi ya ujenzi wa soko hilo tutazipata baada ya mainjinia kusema kama watu wa Mji Mkongwe wanakubaliana na hiyo michoro tuliyoipeleka, tutazijua gharama za michoro iliopo sasa. Kama watu wa Mji Mkongwe wakisema hawakubaliani na michoro tuliyoipeleka, maana yake itabidi tufanye upywa michoro kufuatana na wataalamu wa Mji Mkongwe watakavyotuelekeza.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Spika, mawaziri wengi huwa wanasema kuwa tutafanya, tutafanya. Je, Mhe. Waziri haoni iko haja ya kusema kuwa bajeti hii ndio tutaweza kulijenga soko hilo jipya ambalo tunatarajia michoro yote itakuwa imekamilika.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwanza nataka nimhakikishie, sisi hapa hatutoi ahadi hewa, tukisema tutafanya maana yake tutafanya. Suala lake anasema niseme kwamba ndani ya bajeti hii tutalitekeleza hilo. Bahati nzuri utaratibu tunaokuja nao si wa kutumia pesa za Baraza la Manispaa wala za serikali katika kulijenga soko hili, utaratibu tutakaoutumia ni kuitisha *tender* kwa wawekezaji watakaokubaliana na mawazo yetu ndio tutakaowapa ruhusa ya kuweza kujenga soko hilo. Kwa hivyo, siwezi kusema kwamba ndani ya bajeti ya mwaka 2013/14 tutaweka bajeti kwa ajili ya kazi hii kwa sababu fedha hizi hazitokani na bajeti ya serikali.

Nam. 34

Gharama za Uwekaji Nyasi Bandia Uwanja wa Amani

Mhe. Nassor Salim Ali - Aliuliza:-

Mhe. Spika, kabla ya majibu naomba kufanya masahihisho kidogo. Swali la (b) nafanya masahihisho kwamba, 'fedha hizo zimetoka wapi' isomeke kwamba 'fedha hizo zimetolewa na serikali pekee au na wahisani'. Baada ya hayo naomba kujibiwa swali langu Nam. 34.

Naipongeza Serikali kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa kuufanyia utengenezaji wa kuweka nyasi bandia Uwanja wa Amani katika kipindi hiki cha Sherehe za miaka 50 ya Mapinduzi matukufu ya mwaka 1964.

(a) Je, ni gharama za kiasi gani zilizotumika kuweka nyasi bandia Uwanja wa Amani.

(b) Fedha hizo zimetoka wapi.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kuna masahihisho hayo mafupi kama hayatoingiliana na na majibu yalivyotayarishwa. Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Alijibu**:-**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake namba 34 lenye vifungu a na b kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, lakini kabla ya kujibu naomba niseme kwamba pongezi kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa hatua ya kuufanyia matengenezo uwanja wa Amani, kwa kuweka nyasi bandia katika kipindi cha Sherehe za miaka 50 ya Mapinduzi Matukufu tumezipokea.

Hata hivyo, kwa niaba ya Wizara ya Habari, Utamaduni Utalii na Michezo ningelipenda pongezi hizo za Mwakilishi nizilete kwako Mhe. Spika, na Wajumbe wa Baraza lako tukufu na hasa Mwenyekiti na Kamati ya Mifugo, Utalii na Habari. Kwa usimamizi wao na maelezo yao hadi hatua ya matengenezo yalipokamilika.

Baada ya maelezo hayo sasa jibu (a).

a) Mhe. Spika**,** fedha zilizotumika kwa kazi ya uwekaji wa nyasi hizo bandia ni shillingi 526, 315,938/=.

b) Mhe. Spika**,** fedha hizo zote zilitoka serikalini kupitia Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo iliyopitishwa na Baraza lako tukufu yaani Bajeti ya mwaka 2013/14.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, mbali na majibu mazuri ya Mhe. Waziri katika swali lake mama alijibu kwamba fedha hizi zimetoka serikalini ambazo ni fedha za walipa kodi.

Je. Wizara ina mpango gani kuhakikisha kwamba fedha hizi ambazo ni za walipa kodi wa nchi hii ambazo zimetengeneza uwanja ule kwa sherehe hizi za miaka 50.

Je, kuna mipango gani na mikakati gani kuweza kuchezwa mechi mbali mbali za kimataifa ili kuweza kupata fedha, kuzirejesha fedha hizo?

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, serikali ilipofanya matengenezo ya Uwanja wa Amani na dhamira nyengine za kufanyia matengenezo viwanja mbali mbali, hatufanyi kama ni kitega uchimi, lengo letu ni kufanya miundo mbinu ambayo itasababisha kukuza michezo mbali mbali nchini.

Kwa hivyo, lengo si kwamba fedha iliyotumika baade irudi. Fedha itarudi pale ambapo viwango vya wanamichezo wa Zanzibar vitakapokuwa juu ndio ilivyokusudia serikali. Kwa hivyo, jitihada itafanywa kwa kushirikiana na vyama mbali mbali ambavyo vitatumia viwanja vile ili waweze kutumia zaidi kwa lengo la kuongeza viwango vya wanamichezo wetu. Sio kwamba fedha milioni mia tano iliyotumika baada ya muda irudi, sio lengo la serikali. Lengo ni kuongeza viwango vya michezo mbali mbali katika nchi yetu.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, kwa kuwa shilingi milioni mia tano ni fedha nyingi za walipa kodi ambazo zimetoka kwa ajili ya kufanikisha sherehe zetu hizi za Mapinduzi Matukufu ya mwaka 64. Kwa kuwa nyasi bandia hazihimili vishindo vya sarakasi na gwaride, na Umahiri wa juu wa Jeshi la Wananchi ambalo huwa wanalicheza gwaride pale. Jambo ambalo

linaweza kuathiri zile nyasi bandia na kupelekea kuweka tena shilingi milioni mia tano kwa ajili ya kuweka tena nyasi bandia, kwa sababu sherhe hizi zinafanyika mwaka hadi mwaka.

Je, Mhe. Spika, kuendelea kuweka nyasi bandia kila tutakapofanikisha sherehe za aina yake na kujenga uwanja ambao utakuwa makini na kustahamili katika gwaride. Je, isingekuwa vyema kufanya hivyo kuliko kutumia shilingi milioni mia tano kila mwaka kwa kuweka nyasi bandia kwa ajili ya kufanikisha sherehe hizi.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, nakushukuru na kwa idhini yako naomba nimjibu Mhe. Saleh Nassor Juma Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Wawi.

Kwanza Mhe. Spika, naomba niweke sahihi kwamba nyasi zile bandia hazikuwekwa kwa sababu ya sherehe za miaka 50. Ni kwamba dhamira ya wizara na malengo yake ni kuona kwamba viwanja vyote vya michezo vimewekwa miundombinu ya kileo, ambayo vijana wetu wanataka tujenge. Na ndio maana hata uwanja wa Gombani hatukuweka kwa ajili ya sherehe, ile ni kwa sababu tu ndio mikakati ya wizara yetu kufanya hivyo.

Kwa hivyo, hiyo ni muhimu kujua wananchi waelewe hivyo. Hata kama tuna sherehe za miaka 50 mikakati ya wizara kwa mujibu uliojipangia ni kwamba viwanja vya michezo viwekwe katika hali hiyo.

Tuko katika mashauriano na Serikali ya China pia kwa kutengeneza kiwanja cha Mao tse tung hata kama hatuna sherehe za miaka 50. Ninachosema ni kwamba kwa utaratibu wa kileo na kwa miundo mbinu ya michezo, masuala ya uwekaji wa nyasi bandia katika viwanja vya michezo ni jambo muhimu. Na vinahimili shughuli mbali mbali za michezo kama ambavyo tumeona Jeshi wamecheza gwaride pale bila ya matatizo. Kwa hiyo, hilo si jambo ambalo tumelifanya kwa sababu ya sherehe tu kwa sababu nyengine.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, katika kipindi hiki ambacho kulikuwa kuna sherehe za Mapinduzi pale kiwanja cha Amani. Kwa kivutio kiwanja chetu kuwa kizuri, kulikuwa na michezo ya Kombe la Mapinduzi na

wananchi wa Zanzibar walikuwa wameitikia wito na walikuwa wamevutiwa sana na michezo ile iliyokuwepo katika kiwanja chetu.

Ni kiasi gani cha fedha kimekusanywa kwa ajili ya Michezo ile ya Mapinduzi Cup?

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, suala linalohusiana na viingilio, makusanyo linahitaji muda kidogo. Kwa hivyo, naomba nimtafutie jibu sahihi halafu nitamletea kwa jibu la maandishi.

Nam. 18

Sababu za Zanzibar Kutokuwa na Shirika la Ndege

Mhe. Saleh Nassor Juma– Aliuliza**:-**

Kwa kuwa Zanzibar ni nchi, kama zilivyo nchi nyengine zenye jiografia ya kisiwa kama vile Mauritius, Comoro, Madagascar nk, aidha, kama vilivyo visiwa vyengine Zanzibar ina milango mikuu miwili ya kuingilia kwa maana ya Bandari na Airport ikiwemo Karume Interational Airport, lakusikitisha Zanzibar imekosa Shirika la Ndege kama zilivyo nchi nyengine.

Je, ni sababu gani za msingi zilizopelekea Zanzibar kukosa Shirika lake la Ndege.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa ruhusa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 18 kama ifuatavyo:-

Aidha kabla ya kumjibu napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kumponya salama. Maana jana tulipata taarifa hali yake haikuwa nzuri.

Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa ni kweli kwamba Zanzibar ni kisiwa na njia pekee za usafiri ni njia ya bahari au kupitia uwanja wa ndege ili kuweza kuunganisha na mataifa mengine.

Aidha, nchi yetu imepita katika mikondo mingi hadi kufikia hatua hii iliyopo hivi sasa ambazo serikali kwa mtazamo mzuri iliamua kuja na sera huria ili kutoa nafasi kwa wananchi wake na watu wengine, wenye uwezo kuweza kutumia fursa kwa ajili ya kuekeza na kulitumia soko la ndani.

Ni jambo la faraja na la tija sana pale ambapo kama nchi kuweza kuwa na shirika lake wenyewe la ndege, kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi wake. Aidha, naomba tukubaliane kwamba biashara ya ndege inahitaji wawekezaji na umahiri mkubwa sana ili kuwa na muendelezo wake unakuwa endelevu. Bado kama serikali tunapaswa kuliangalia jambo hilo kwa kina na baadae tuweze kufikia maamuzi.

Mhe. Spika, kutokana usafiri wa anga kuimarika hapa Zanzibar, Serikali inafikiria kuanzisha Shirika lake la Ndege. Kwa sasa lengo kubwa ni kutoa kipaumbele kwa sekta binafsi, ili kuweza kumudu kutoa huduma za usafiri wa anga ulio bora na wenye ushindani na Serikali ibakie kuwa ni Msimamizi Mkuu tu wa sekta. Pale ambapo itaonekana kuna haja ya serikali kuwa na Shirika lake la Ndege basi wizara itachukua hatua ya kuishauri serikali ili kufanya maamuzi hayo.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri katika majibu yake amesema suala la kuekeza katika sekta ya anga ni suala ambalo linahitaji pesa nyingi. Kwa kuwa tuna uzoefu kwamba hapa Zanzibar kuna hata vijikampuni vidogo vidogo kama vile *Coastal Air, Zan Air* hata na hizi *Tropical Air* wanazo ndenge nyingi kidogo navyo ni vikampuni vidogo vidogo.

(a) Mhe. Spika, anaweza kunambia kwamba serikali ni masikini zaidi kuliko haya mashirika madogo madogo ya ndege, na hivyo tumeshindwa kuekeza katika sekta hiyo?

(b) Kwa kuwa, sisi tulikuwa nayo *Jet* hapa ambayo ilikuwa ikitumika kwa ajili ya kumsafirisha Mhe. Rais wetu. Pamoja na kwamba katika mazingira yasiyoeleweka hatujui ilipo kwa sasa. Je, umasikini huu huu ndio ulioshindwa kui- *handle* na ikapotea hivi hivi pesa za walipa kodi zikateketea?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:

(a) Mhe. Spika, la kwanza katika majibu yangu ya msingi sikuwahi kutamka kwamba uwekezaji katika biashara hii ya huduma za Anga kwamba inahitaji mtaji mkubwa kiasi ya kwamba serikali imeshindwa.

Nilichokisema inahitaji uwekezaji na umahiri; umahiri haumaanishi kwamba uwepo mtaji mkubwa, lakini jambo la msingi kwamba serikali kipaumbele chake ni kuunganisha sekta hii kama ni msimamizi wa kuweka mazingira mazuri. Kila mwenye uwezo wa kuhitaji kufanya biashara hii aweze kupata fursa kama zilivyo sekta nyengine.

Hatuoni haja kama serikali kujiingiza moja kwa moja, ulazima wa kufanya biashara hii na tumesema kwamba tukiona kuna ulazima huo, sisi kama wizara tutaishauri serikali kwa sababu msingi mkubwa ni kuona huduma za usafiri wa anga zinaimarika. Hivi sasa hakuna tatizo katika nchi yetu. Kila mwenye kuhitaji kusafiri anapata kusafiri kwa wakati anaoutaka.

(b) Mhe. Spika, siamini kwamba umasikini ndio uliopelekea ndege hii kupotea. Na mimi taarifa niliokuwa nazo kwamba ndege hii ilikuwa kwa mfumo wa kuwa imenunuliwa na malipo yalikuwa yanaendelea. Serikali pamoja na muuzaji katika makubaliano yao ndio ilikopelekea ndege hii kuwachwa huko ilikonunuliwa.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, jibu langu la (b) sikulisikia huko mwisho.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri hebu rudia majibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, nimesema mimi siamini kwamba kwa sababu ya umasikini ndio uliwopelekea ndege hii ipotee. Ndege hii ilinunuliwa na malipo yakawa yanaendelea.

Lakini katika msingi wa makubaliano hayo hayo ya manunuzi ndio iliyopelekea ndege hii ibakie huko ilikonunuliwa.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Mhe. Spika, kwanza nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini kwa masikitiko makubwa ya wananchi wetu na wageni wetu wanapofika Zanzibar hasa bandarini na *Airport*. Kama unavyojua sasa mashine yetu ya *X-ray* ya *Airport* imeharibika.

Ule upekuzi unaofanywa na wafanyakazi wetu wa *Airport* utakuta mzigo wa mwanamme, lakini anaufungua mwanamke anauangalia ndani. Kwa kweli, hatua hii mimi mwenyewe imenikuta Pemba nilipofika mzigo wangu kaufungua mwanamke kauangalia. Hata bandarini Unguja mambo haya nimeshayaona kwa wananchi wetu kwamba wanakaguliwa mizigo yao na wanaume na mwanamke anafungua mzigo wa mwanamme.

Kwa hivyo, naomba Mhe. Naibu Waziri anipe sababu zipi za msingi hata inakuwa upekuzi huu unakuwa hivi. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Kwanza naomba Mhe. Spika, nimpe pole kama kadhia hiyo imemkuta. Lakini

matarajio na utaratibu wa ukaguzi ni kwamba ukaguzi unazingatia jinsi, mwanamme akaguliwe na mwanamme mwenzake na mwanamke akaguliwe na mwanamke mwenzake.

Kwa hivyo, kama kuna tatizo limetokezea pengine inawezekana wakati huo ilikuwa labda wafanyakazi wetu walikuwa wachache abiria wako wengi na wanaharaka ikapeleka hivyo. Lakini sisi kama wizara tutaendelea kuwasihi na kuwakumbusha wenzetu hawa kuona kwamba utaratibu uliopo wa kuendesha utaratibu wa upekuzi kwa kuzingatia jinsi unapewa kipaumbele na itakuwa ndio utaratibu wa kudumu.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Spika, naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri ni taasisi ipi katika wizara yake inayo uwezo wa kutoa ruhusa au kibali cha kuanzisha Shirika la Ndege hapa Zanzibar. Je, taasisi hiyo imewahi kupokea maombi hayo na kama imewahi yamefikia wapi?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, utaratibu wa kuanzisha *Airline Zanzibar* hatutoi kibali, kibali hiki kinatolewa na *TCAA*. Kama sote tunavyokumbuka kwamba tulipitisha sheria hapa mbili mwaka 2011 ya Zanzibar *Airport Authority* na *Zanzibar Aerodrome Act*. Sheria hizo zote mbili hazitoi fursa ya sisi kuweza kuanzisha Mashirika ya ndege.

Kwa msingi huo hadi muda huo hakuna maombi yoyote au hatuna ruhusa yoyote iliyotolewa ya kuanzisha Mashirika haya ya ndege.

Nam 41

Ongezeko la bei ya Umeme

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza**:-**

Kwa kuwa hali ya maisha na ya kipato cha wananchi ni ya chini, na bado Serikali inahangaika kuinuwa hali za maisha ya wananchi kutoka chini ya dola moja kwa siku.

Na kwa kuwa sehemu kubwa ya kipato cha wananchi wetu inatokana na kilimo, biashara, uvuvi na sehemu ndogo tu ya kipato cha mwananchi inatokana na ajira katika sekta ya umma na kwa uchache sana inatokana na sekta binafsi.

Na kwa kuwa hivi karibuni wananchi hao katika hali hiyo ngumu ya maisha na kipato, wameongezewa mzigo wa bei ya umeme kwa kupandishwa ghafla.

(a) Je, katika hali kama hiyo ya ugumu wa maisha na kipato kwa wananchi, serikali haioni kuwa inawasababishia wananchi kushindwa kumudu kulipia huduma ya umeme ambayo kwa maisha ya sasa imekuwa siyo ya anasa bali ya lazima.

(b) Je, kwanini serikali isitafute mpango mwengine utakaowezesha Shirika la Umeme Zanzibar kumudu gharama za ununuzi wa nishati ya umeme na uendeshaji wa shirika.

(c) Serikali ina mpango gani wa kuwaondoshea makali ya ongezeko la bei ya umeme wananchi wa kipato cha chini ambao ndiyo wengi nchini kwetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swala lake namba 41 lenye vifungu a na b kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, ni kweli kuwa kupanda kwa bei ya umeme inasababisha kupanda kwa hali ya maisha, hata hivyo nia ya serikali sio kuwabebesha mzigo wananchi bali inatokanana kupanda kwa bei ya kununulia umeme kutoka TANESCO.

b) Ili Shirika liweze kumudu gharama za ununuzi wa umeme na uendeshaji, juhudi kubwa zinachukuliwa za kuhakikisha kuwa mita zote zinabadilishwa na kuwekwa za TUKUZA na pia kuhakikisha kuwa Taasisi zote zinalipa bili zake kwa wakati.

c) Katika kupanga bei za umeme serikali huwa inawaangalia kwa karibu sana wananchi wa kipato cha chini ambao hata katika bei iliyopo sasa wananchi hao wanalipa T.Sh. 66 tu kwa *unit* moja badala ya T.Shs 222 kwa *unit* moja zinazolipwa na wananchi wa kawaida.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub:

(a) Ahsante sana Mhe. Spika, kwa mujibu wa maelezo yake kwa kuwa bei zimekuwa zikipangwa kwa kuangalia wananchi wa kipato cha chini na wananchi wa kawaida. Je, fomula gani inayotumika kuangalia wananchi wa chini na wananchi wa juu.

(b) Unatoa kauli gani kwa wananchi kwa hivi sasa kwa hii bei itapanda tena au ndio imefika hapa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati : Mhe. Spika, siku zote shirika linaangalia katika upandishaji wa bei na kuangalia wananchi. Aidha, wenye kipato cha chini na wale watumiaji wa kawaida wenye *size* ya kati. Hili halikuanza sasa hivi, limeanza toka linaanza Shirika la Umeme hapa Zanzibar, hiyo hali tunaendelea nayo.

Suala la pili naomba kidogo Mhe. Mwakilishi alirejee.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, mimi nafikiri nianze mwanzo kwa sababu hata mwanzo naona hakulisikia inavyoonesha Mhe. Naibu Waziri.

Kwa mujibu wa maelezo ya Mhe. Waziri kwa kuwa bei zimekuwa zikipanda kwa kuangalia wananchi wa kipato cha chini na wananchi wa kawaida.

(a) Je, ni *formula* gani imekuwa ikitumika kujua wananchi wa kipato cha chini na wa kipato cha juu.

(b) Unatoa kauli gani kwa wananchi hivi juzi tu umeme huo umepanda, kweli wizara unayoiongoza wewe ina muda mfupi unataka kuongeza tena bei ya umeme ni kweli suala hili?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati : Mhe. Spika, naomba nimrejeshee tena Mhe. Mwakilishi kama hivi ifuatavyo:-

Kama nilivyoeleza hapo awali kuhusu kupanda kwa bei ya umeme inaangalia wananchi toka lilipoanzishwa shirika.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, nimemuuliza katumia kigezo gani au fomula gani yakujua kipato cha chini kwa mwananchi na kipato cha juu atueleze hivi.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati : Mhe. Spika, kuna wananchi hapa Zanzibar matumizi yao hayazidi *unit 50*. Kwa hivyo, hao ni wa kipato cha chini. Na wanaozidi hapa ni wananchi wa kawaida.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, katika waya wetu huu mpya ambao umetandikwa hivi karibuni nimeambiwa kuwa una *Megawatt* 100.

Je, shirika linalazimika kulipa kiwango kikubwa chote hicho kwa TANESCO au linalipa kutokana na matumizi na mahitaji yetu tuliokuwa nayo. Lakini pia kama tunalipa kiwango chote hatuoani kwamba kulipa kiwango chote ambacho hatukitumii kinasababisha gharama za umeme kuwa kubwa. Kama ni mkataba ambao unazungumzia hivyo haioni kwamba kuna haja ya serikali sasa kuangalia upya mkataba huo na shirika la TANESCO.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati : Mhe. Spika, uwezo wa waya ni *Megawatt* 100. Lakini tunachokilipa ni kile tunachokitumia. Sasa nikilijibu suala hili kwa hivyo suala la pili litakuwa limeshatoa jibu hivyo hivyo.

Kwa sababu uwezo wa waya ni *Megawatt* 100. Lakini tuna mita zetu kule tunazotumia huku ambazo zinarikodi, kwa hivyo kile unachotumia ndicho unacholetewa bili.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Spika, kwa kuwa mwananchi anaetaka kuungiwa umeme anaomba kwa ridhaa yake kwa Shirika la Umeme na gharama zote analipia mwananchi mpaka kufika umeme nyumbani kwake. Ni sababu gani inayochangia kupanda mara kwa mara umeme huu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati : Mhe. Spika, kinachosababisha kupanda gharama za umeme ni kutokana na manunuzi tunayonunua umeme kutoka Tanesco.

Nam. 31

Mpango wa Kuwasaidia Wavuvi wadogo wadogo Kupambana na Ukimwi

Mhe. Saleh Nassor Juma– Aliuliza**:-**

Tafiti nyingi zilizofanywa na wataalmu wa sekta ya afya zinaonyeshwa kuwa, sekta ya uvuvi ni moja kati ya harakati zinazopelekea ongezeko la Virusi vya ukimwi hususan katika maeneo ya Mwanzoni mwa Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika ambamo wavuvi hupiga kambi (dago kwa ajili ya uvuvi). Kwa kuwa Tanzania Bara wamo mbioni kuanzisha mfuko wa afya ili kupambana na gonjwa hilo. Na kwa kuwa Zanzibar wavuvi hupiga kambi zao kwenye mwambao wa Bahari ya Hindi kwa kipindi kirefu jambo linaloweza kupelekea maingiliano ya kijinsia baina ya wavuvi na wakaazi wa maeneo hayo.

Ni hatua gani zilizochukuliwa na zile zitakazochukuliwa na serikali katika kuwasaidia wavuvi wa nchi hii katika suala zima la mapambano ya Ukimwi na Virusi vya Ukimwi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swala lake Nam. 31 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza naomba unipe nafasi nimpe pole Mhe. Saleh Nassor Juma maana jana alikuwa mgonjwa na nimem-*miss*!

Lakini napenda kumpa pole na napenda pia nimpe mawaidha kwamba jana tulijibu suala la afya na nafikiri kutokana na matatizo yake yasioambukiza anahitaji mazoezi.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Wawi swali lake namba 31 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, hatua zimechukuliwa na serikali baada ya tafiti kufanyika na kutambua kwamba wavuvi wa dago ni kundi lililo katika hatari ya kuambukizwa Ukimwi na kuambukiza wengine, wanaporudi majumbani kutokana na mazingira ya kazi yao.

Katika kuwasaidia wavuvi hao, wizara kupitia Kitengo chake shirikishi cha Ukimwi, Kifua Kikuu na Ukoma, hutoa huduma za mkoba za kupima maambukizi ya VVU kwa watu makundi mbali mbali wakiwemo wavuvi. Wale ambao kwa bahati mbaya hugundulika na maambukizo ya VVU hupewa rufaa ya kwenda kwenye vituo vyetu vya afya vinavyotoa huduma kwa watu wanaoishi na VVU.

Vile vile, Wizara kupitia kitengo chake imo katika matayarisho ya kufanya utafiti mwengine baada ya ule uliofanyika miaka ya nyuma utakaotusaidia kujua kiwango cha maambukizi ya *VVU* miongoni mwa wavuvi kwa sasa. Utafiti huo unategemea kufanyika mwaka huu.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante Mhe. Spika, napenda nimhakikishie Mhe. Naibu Waziri, kwamba jana niliumwa, lakini leo nipo *fit.* Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba niulize swali dogo la nyongeza.

Kwanza, kwa kuwa lengo na madhumuni ya SMZ katika masuala ya ukimwi na virusi vya ukimwi, ni kufikia zero tatu. Na kwa kuwa wenzetu wa

Tanzania Bara tayari wameanzisha mfuko ambao utasaidia katika suala zima la kuweza kupambana na ukimwi na hatimaye kufikia zero. Je, ni lini hapa Zanzibar itafikiria kuanzisha mfuko huu ambao unaweza ukatusaidia sana katika suala zima la kuweza kupambana na ukimwi.

Pili, kwa kuwa ndoa nyingi Mhe. Spika, zimeshaanza kuvunjika hapa Zanzibar pale wavuvi wanapotoka dago na kutaka kuanza kufanya tendo la ndoa na ahali zao. Je, ni lini Serikali yetu ya SMZ itaanzisha utaratibu wa kuwapa taaluma wavuvi kusudi wanaporudi dago waweze kwenda kufanya mambo ya vipimo, ndio wafanye tendo la ndoa na ahali zao, ili kuzinusuru hizi ndoa zisivunjike, sambamba na kuweza kujikinga na virusi vya ukimwi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ni katika wale walioridhia zero tatu ili kusiwe na maambukizi mapya, ili kusiwe na vifo, ili wote wanaoambukizwa wapate dawa. Sasa ili kuweza kuyafanya hayo, wenzetu wa Bara wametayarisha mfuko, lakini mfuko hautayarishwi na Wizara ya Afya, sisi kazi yetu ni kukinga na kutibu, *ZAC* ambayo ipo chini ya Makamu wa Kwanza wa Rais hao ndio wanaohusika na suala hili. Kwa hiyo, ningependa aelekeze suala hilo kwa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ili aweze kupata jawabu sahihi.

Pili, kuhusu taaluma ya wavuvi tumesema kwamba wavuvi wa dago wanafikiwa na huduma za mkoba na wanapewa taaluma. Na kwa kuthibitisha hilo utafiti uliofanyika katika mwaka 1998 ambao ndio nilikuwa naunukuu katika jibu langu la msingi. Ulipofanywa utafiti asilimia 97.7 ya wavuvi hao walikuwa na ufahamu mzuri kuhusu maradhi ya ukimwi, kaswende na *gonorrhoea.* Ina maana yanayopitia ngono.

Lakini pia, wavuvi hawa asilimia 16 walikuwa na uhusiano wa kimapenzi nje ya ndoa. Na kati ya hao asilimia 4.3 tu ndio waliosema wanatumia *condom* kwenye mahusiano yao ya kimapenzi. Na sababu iliyotolewa kwa nini hawatumii *condom?* Wanasema hivi kwamba wao kwanza wanawaamini wale wanaotembea nao.Kwa hiyo, wanafanya bila ya kutumia *condom.* Lakini pia, cha kushangaza wanasema kwamba kutumia *condom* ni kinyume cha maelekezo ya dini, lakini kuzini inakubalika. Lakini la tatu, kukosa raha ya ngono wanapotumia *condom.* Kwa hiyo, hayo ndio wavuvi waliyoyasema.

Lakini pia, baada ya hapo wengi wao pia walikuwa wakiendelea na tabia hatarishi zinazochangia kupata maambukizi ya *VVU*. Sasa Wizara katika kuendelea kufuatilia tabia hiyo na viwango vya maambukizi inatoa elimu kwa wavuvi walioko kwenye madago. Na kwa sababu imeona kwamba tatizo linaendelea ndio maana tukatayarishwa sasa tuangalie mwaka 1998 tulipofanya na leo hii hali ikoje.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na naomba niongeze juu ya majibu mazuri ambayo yametolewa na Mhe. Naibu Waziri wa Afya, kuhusiana na suala zima la uanzishwaji wa mfuko unaoshughulikia masuala ya maradhi ya ukimwi.

Ni kweli kwa hakika ni matakwa ya nchi zote ambazo ni wanajumuiya ya *SADC,* kuweza kuanzisha mfuko maalum ambao kwa lugha ya kigeni wanaita *HIV Aids Fund*. Kwa sababu kunaonekana kuwa washirika wa maendeleo kwa kiasi kikubwa wameanza kupunguza ufadhili wao katika kushughulikia masuala ya ukimwi. Na dunia hivi sasa inataka nchi zenyewe zichukue na kubeba dhima hiyo kwa kiasi kikubwa katika kushughulikia suala la vita dhidi ya ukimwi na kufikia zero tatu.

Ni kweli wenzetu Tanzania Bara tayari wapo katika hatua ya mwisho ya mfuko huo, na sisi hivi sasa tupo katika mchakato wa kuanzisha mfuko huo. Utakapokuwa tayari Mhe. Spika, tutaleta sheria hiyo ya kuanzishwa mfuko huo hapa katika Baraza lako tukufu ili iweze kuridhiwa na uwepo mfuko huo.

TAARIFA ZA SERIKALI

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya mwaka 2012/13 - Wizara ya Katiba na Sheria

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima na kufika hapa katika uendelezaji wa shughuli zetu muhimu. Lakini pili, napenda pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunirejesha salama Pemba.

Mhe. Spika, Wizara ya Katiba na Sheria ilianzishwa baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2010 chini ya kifungu cha 42 (1) cha Katiba kinachompa mamlaka Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na taasisi mbali mbali za serikali. Kwa ujumla Wizara ya Katiba na Sheria iliundwa kuratibu shughuli za sekta ya sheria na kusimamia utoaji haki, kutoa huduma za usajili wa biashara na mali, matukio ya kijamii na hatimiliki, kusimamia shughuli za kiislam zikiwemo mali za wakfu na amana na shughuli za Afisi ya Mufti. Majukumu haya yanatekelezwa na taasisi 12 za Wizara hii kama ifuatavyo:

1. Mahakama.
2. Afisi ya Mwanasheria Mkuu.
3. Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka.
4. Tume ya Kurekebisha Sheria.
5. Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali.

6. Afisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo.
7. Afisi ya Msajili wa Hakimiliki.
8. Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana.
9. Afisi ya Mufti.
10. Idara ya Utumishi na Uendeshaji.
11. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.
12. Afisi Kuu Pemba.

Mhe. Spika, tulizounda hapa Zanzibar kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar, zinatekelezwa na kufuata mgawanyo wa madaraka wa mamlaka tatu za dola ambazo ni mamlaka ya uendeshaji Serikali, mamlaka ya kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma, na mamlaka ya utoaji haki. Kila mamlaka kati ya hizo inatakiwa kutekeleza shughuli zake kwa kuzingatia mipaka yake.

Mhe. Spika, katika kutekeleza kazi za usimamizi wa shughuli za umma Baraza la Wawakilishi limeunda Kamati za Kudumu kwa mamlaka iliyopewa na Katiba ya Zanzibar chini ya kifungu 85. Kamati hizo zinafanya kazi za ufuatiliaji wa shughuli za serikali na kutoa taarifa mbele ya Baraza. Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ni miongoni mwa Kamati hizo. Katika taarifa yake ya ufuatiliaji wa shughuli za serikali ya mwaka 2012/13 iliyowasilishwa kwenye Baraza, Kamati hiyo ilipewa maagizo sita kwa Wizara ya Katiba na Sheria ili yafanyiwe kazi.

Mhe. Spika, maagizo hayo na hatua iliyofikiwa katika kuyafanyia kazi ni kama ifuatavyo:

Agizo la mwanzo Mahakama ya Makunduchi ifanyiwe matengenezo ya haraka.

Mhe. Spika, naomba kulijulisha Baraza lako tukufu kwamba agizo hilo limeshafanyiwa kazi. Katika mwaka huu wa fedha 2013/14. Mahakama ilitenga fedha kwa ajili ya matengenezo ya jengo hilo, utaratibu wa kumpata mjenzi umefanyika na kazi za ujenzi zimeanza. Kazi zinazofanyika ni kuezua paa na kuezeka upya, kuongeza vyumba ili kuongeza nafasi ya jengo, kupigwa plasta na kutiwa rangi. Kuwekwa dari pamoja na kuunganishwa umeme. Hadi sasa jumla ya shilingi milioni 72,642,629/= zimelipwa kwa ajili ya kazi hizo.

Kumalizika kwa kazi hizo kutasaidia kuliweka jengo hilo katika hali nzuri na kuziwezesha shughuli za Mahakama kufanyika kwa ufanisi zaidi. Tunatarajia kuwa kazi hiyo itamalizika katika kipindi hichi cha mwaka 2014/15.

Agizo la pili, Kamati ilishauri ni vyema Wizara ikalihamisha suala la kesi za ubakaji katika Mahakama ya Watoto ili haki iweze kupatikana kwa urahisi zaidi. Na hali hiyo itazidisha uhuru wa mtoto katika kesi hasa ukizingatia kwamba mazingira ya Mahakama hiyo yameandaliwa kuwavutia watoto na kuwatoa hofu.

Mhe. Spika, ili tutekeleze ipasavyo agizo hili, inabidi kwanza yafanyiwe marekebisho ya sheria ili kumruhusu mtoto anayebaka apelekwe Mahakama ya Watoto. Kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto Nam. 4 ya 2011, mtoto ni binadamu yeyote ambaye umri wake si zaidi ya miaka 18. Sheria hii inaeleza kuwa pindi mtoto anapotumiwa kufanya kosa lolote la jinai anastahiki kufikishwa mbele ya Mahakama ya Watoto kwa lengo la kuhukumiwa, na inazuia kwa mtoto aliyetuhumiwa kufanya kosa la mauaji kwa makusudi, uhaini na ubakaji. Hivyo, mtoto anayebakwa hawezi kupelekwa Mahakama ya Watoto kwa sababu sheria inakataza.

Kwa upande mwengine Wizara imepokea pongezi zilizotokana na uamuzi uliochukuliwa na Mahakama kwa kuanzisha Mahakama ya Watoto kwa Unguja. Hatua ya kuanzishwa kwa Mahakama kama hiyo Pemba hivi sasa zinaendelea.

Agizo la tatu, ni kwamba Kamati imeagiza Wizara kulifuatilia kwa haraka suala la uajiri wa Afisi ya Msajili wa Hakimiliki ili kuwezesha taasisi kuwa na watendaji wa kutosha.

Mhe. Spika, hatua za utekelezaji zimechukuliwa kwa Wizara kwa watendaji watatu kwa ajili ya Afisi ya Msajili wa Hakimiliki Unguja na Pemba. Watendaji hao tayari wameshaanza kazi katika mwaka huu wa fedha 2013/14. Walioajiriwa ni Afisa Leseni mmoja, Afisa Usajili Kumbukumbu mmoja ambao wanafanya kazi zao Afisi za Unguja. Na Afisa Usajili Kumbukumbu mmoja ambaye anafanya kazi Pemba.

Hata hivyo, Wizara inakiri kwamba bado afisi hii haijakuwa na watendaji wanaotosha kumudu kazi zake kikamilifu. Hivyo, itaendelea na juhudi zake kwa ajili ya watendaji wa kutosha na wenye uwezo wa kufanya kazi hiyo ipasavyo.

Agizo la nne, suala la ucheleweshaji kupatikana magamba kutoka *Zanzibar Press* afisi ijipange ili kuhakikisha wanatafuta njia mbadala ya kuchapisha magamba hayo kwa haraka zaidi.

Mhe. Spika, hatua za utekelezaji zimechukuliwa kwa kuiwezesha Afisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo kupunguza tatizo hilo kwa kiasi kikubwa. Afisi hii

imeweza kuagiza idadi kubwa ya magamba kwa ajili ya shughuli za usajili wa vizazi na vifo. Hali hii imepelekea kuondoka kwa tatizo la magamba ya usajili na huduma ya usajili inaendelea bila ya matatizo yoyote hivi sasa.

Kamati ilipendekeza kwamba waraka wa kupendekeza punguzo la bei ya malipo ya vyeti vilivyopita muda yaani *late registration* ambao kwa sasa upo kwa Makatibu Wakuu, bei isiyo zaidi ya shilingi 10,000/= kutokana na hali za maisha ya wananchi wa Zanzibar. Kwa sasa ambapo bado waraka huo haujathibitishwa na serikali, Afisi ingekuwa na utaratibu wa kuwapunguzia gharama wananchi wenye hali ngumu ya kimaisha.

Mhe. Spika, naomba kulijulisha Baraza lako tukufu kwamba waraka wa mapendekezo ya kupunguza bei ya vyeti imewasilishwa Baraza la Mapinduzi, nalo limetoa maagizo ya kufanya marekebisho kadhaa kwenye mapendekezo hayo kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Tume ya Mipango. Kwa sababu hiyo viwango vya malipo vinavyolipwa vitaendelea kutumika hadi hapo kazi hiyo itakapokamilika na kupata baraka za Baraza la Mapinduzi. Kwa sababu hiyo tunajitahidi ili katika bajeti ya mwaka ujao wa fedha 2014/15 suala hili liwe limeshakamilika.

Agizo la tano, inaonekana kwamba migogoro mingi ya misikiti inatokana na maslahi yanayoingia msikitini kutoka katika vyanzo mbali mbali vikiwemo maduka ya misikiti. Hivyo, Afisi ya Mufti isimamie suala hilo ili kupunguza migogoro hiyo.

Mhe. Spika, migogoro misikitini si sababu ya kuwepo kwa maduka tu, bali zipo sababu tofauti zinazochangia migogoro hiyo zikiwemo tofauti za fikra, elimu na mitizamo. Afisi ya Mufti inachukua hatua mbali mbali katika jitihada za kusuluhisha migogoro hiyo zikiwemo kuonana na kuzungumza na viongozi wa misikiti hiyo kwa mfano Msikiti wa Biziredi, Masjid Tutani Bububu Kijichi, Msikiti wa Mshelishelini, Masjid Taqwa Mkoani na Masjid Nuur Chwale Madenjani Pemba. Ili kufanya mikutano na taaluma kwa ajili ya kuwaelimisha masheikh na wasomi wa kiislam jinsi ya kuepuka migogoro katika misikiti.

Hivi karibuni Afisi ya Mufti kwa kushirikiana na *World Plan Co-Society* kutoka Libya ilifanya mkutano uliojumuisha maimamu 150 kutoka Wilaya zote za Unguja. Miongoni mwa agenda zilizozungumzwa ni njia ya kuepuka na kukabiliana na migogoro ya misikitini. Mipango inatarajiwa ya kufanya mkutano kama huu Kisiwani Pemba hapo baadae.

Vile vile, wiki inayokuja tukijaaliwa Baraza la Ulamaa litakutana kujadili mambo mengi yakiwemo matatizo kama haya.

Agizo la sita na la mwisho, Mhe. Spika, ni kwamba Wizara isimamie kwa ukaribu zaidi taratibu za kupata hatimiliki ya jengo la afisi Pemba ili kuepusha usumbufu unaoweza kujitokeza siku zijazo. Mhe. Spika, hatua za utekelezaji zimechukuliwa kwa Wizara kuwasiliana na Wizara inayohusika kwa ajili ya kupata hatimiliki ya jengo hilo na mawasiliano yanaendelea vizuri huku kukiwa na matarajio makubwa ya kupatikana haki hiyo siku za karibuni.

Mwisho, Mhe. Spika, kwa heshima kabisa naomba niwashukuru sana Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ambayo wakati wote tunashirikiana kwa pamoja na maelekezo ambayo wanatoa tunajitahidi kuyafanyia kazi ili kuweza kupeleka mbele Wizara yetu.

Mhe. Spika, kwa heshima baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha ripoti hii ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ambayo tunaitoa kwa mwaka fedha 2012/13 kama nilivyoelezea hapo awali. Na naomba Waheshimiwa Wajumbe waijadili na hatimae waweze kuikubali au kutupa maagizo mengine. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Ussi Jecha Simai (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Muhtasari wa Ripoti ya Kamati ya Kudumu ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka wa fedha 2013/14.

Mhe. Spika, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa hidaya kubwa aliyotupa ya uhai na uzima hata tukaweza kuja hapa kuendelea na shughuli zetu za kuwatumikia wananchi wa nchi yetu.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Kamati nachukua nafasi hii kumuombea shufaa kwa *Allah Subhana Wataala,* Waziri wa Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma, Mhe. Haroun Ali Suleiman, kwa mtihani wa maradhi alioupata. *Inshaallah* utukufu wake *Allah Subhana Wataala* amjaalie uzima na afya njema ili arudi kuungana nasi katika harakati za kuiletea maendeleo nchi na wananchi wetu. *Amin.*

Mhe. Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi pamoja na Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kuipa Kamati yetu ushirikiano mkubwa uliotuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi mkubwa. Lakini pia, tunashukuru kwa kutupatia nafasi ya kueleza japo kwa muhtasari Ripoti ya Kamati inayotokana na kazi ambazo zimekuwa zikitekelezwa na Kamati kwa takriban mwaka mzima.

Mhe. Spika, napenda kuchukua nafasi hii adhimu kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa mashirikiano yao makubwa ambayo yametuwezesha kufanya kazi zetu kwa ufanisi wa hali ya juu. Kwa heshima kubwa naomba niwatambue Wajumbe hao kwa kuwataja kwa majina kama ifuatavyo:

1.	Mhe. Ussi Jecha Simai	-	Mwenyekiti
2.	Mhe. Abdulla Juma Abdulla	-	Makamu Mwenyekiti
3.	Mhe. Bikame Yussuf Hamad	-	Mjumbe
4.	Mhe. Nassor Salim Ali	-	Mjumbe
5.	Mhe. Suleiman Hemed Khamis	-	Mjumbe
6.	Mhe.Wanu Hafidh Ameir	-	Mjumbe
7.	Ndugu Aziza Wazir Kheir	-	Katibu
8.	Ndugu Khamis Hamad Haji	-	Katibu

Mhe. Spika, baada ya utambuzi huo naomba pia nitumie fursa hii kwa niaba ya Kamati kuzipongeza Wizara tunazozisimamia nchini chini ya Mawaziri mahiri wa Wizara hizo. Kwanza, Mhe. Haji Omar Kheir - Waziri wa Nchi (AR) na Idara Maalum za SMZ. Mhe. Abubakar Khamis Bakary - Waziri wa Katiba na Sheria. Na Mhe. Haroun Ali Suleiman - Waziri wa Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma. Kwa kutekeleza maagizo ya Kamati na ushirikiano wanaoipa Kamati wakati wote inapofanya shughuli zake.

Mhe. Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi imeundwa kwa mujibu wa kifungu cha kanuni ya 106 (f) ya Baraza la Wawakilishi toleo la mwaka 2012 na majukumu yake yametajwa katika kifungu cha 113.

Mhe. Spika, Kamati ilifanya kazi zake kwa utaratibu wa kupokea taarifa za utekelezaji wa malengo ya Wizara pamoja na taasisi zake na baadae kutembelea, kukagua utekelezaji wa shughuli zinazofanywa na taasisi hizo.

Wizara ya Katiba na Sheria. Mhe. Spika, Kamati yetu ilitembelea taasisi mbali mbali za Wizara hii na kukagua miradi kadhaa inayotekelezwa na taasisi hizo. Baada ya kutembelea na kuona utekelezaji wa shughuli hizo Kamati ilitoa maoni, maagizo na ushauri kwa Wizara na taasisi zake kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utekelezaji.

Mhe. Spika, muhtasari huu unabainisha baadhi ya mambo ambayo Kamati iliona kuwa ni muhimu sana kwa ajili ya kuisaidia serikali katika utekelezaji wake na wananchi kwa ujumla. Mambo yenyewe ni kama yalivyofafanuliwa hapa chini.

Mhe. Spika, Mahakama ni miongoni mwa mihimili muhimu ya dola yenye nguvu kikatiba. Miongoni mwa majukumu ya Mahakama ni pamoja na kuweka kumbukumbu na kuwa na mamlaka yote ya kesi za jinai na madai na nguvu nyengine kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na sheria nyengine.

Mhe. Spika, katika ziara ilizofanya Kamati ilipokuwa ikikagua na kutembelea Mahakama nyingi imegundua kuwa Mahakama hizo zinakumbwa na changamoto ya uchakavu wa majengo yake na kukosa nafasi kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake kama inavyotakiwa. Kutokana na hali hiyo, Kamati inaishauri serikali kujipanga na kufanya utaratibu wa kuyakarabati majengo ya Mahakama na wakati huo huo ikijipanga kujenga majengo mapya hasa kwa upande wa Mahakama Kuu.

Mhe. Spika, changamoto iliyopo hivi sasa ya ufinyu wa ofisi kulingana na mahitaji yaliyopo kuwa mengi hupelekea watendaji wa Mahakama hiyo kuwapisha Majaji wa Mahakama ya Rufaa pindi wanapokuja kwa ajili ya kusikiliza kesi za rufaa.

Mhe. Spika, Kamati ilipofanya ziara ya kutembelea jengo la Mahakama Kuu Chake Chake ilisikitishwa na hali ya ubovu wa jingo, lakini zaidi sehemu wanayowekwa mahabusu. Sehemu hiyo ni gofu lililochakaa na halina hata paa la kustiri jua wala mvua. Hata choo kinachotumiwa na mahabusu hao hakipo katika hali nzuri ya binadamu yoyote anayehitaji utu wake kukitumia. Hali hii inakwenda kinyume na msingi wa haki za binadamu iliyowekwa na Katiba yetu ambayo utu wa mtu na heshima yake vinalindwa akiwa huru au ameshikiliwa kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Spika, wakati serikali inashughulikia kujenga majengo mengine ya kumbukumbu na vivutio kwa gharama kubwa, isisahau pia kuwa kuna majengo mengine muhimu kama haya ya utoaji wa haki yanahitaji kufanyiwa ukarabati tu. Kamati imeshasema sana kuhusu ufinyu wa Kitengo cha Waendesha Mashtaka katika Mahakama ya Mwanakwerekwe ambacho kinahatarisha afya za watendaji waliopo pale.Ubovu wa jengo la Mahakama ya Makunduchi na Chake Chake na bado hatua muafaka hazijachukuliwa.

Mhe. Spika, Kamati hairidhishwi na baadhi ya dosari za kiutawala ambazo haziwezi kuhalalishwa kwa kisingizio cha ukosefu wa fedha. Kamati imepata taarifa ya ukosefu wa vitendea kazi muhimu vya Mahakama kama vile karatasi za kuchapisha hati za wito *(summons).*

Mhe. Spika, katika udadisi wake Kamati imepata taarifa kuwa mnamo tarehe 24 Disemba, 2013 na tarehe 31 Disemba, 2013 Mahakama ya Mwera

haikuweza kufanya kazi kwa sababu ya ukosefu wa karatasi za kuchapisha hati za wito tu. Hali hii inatia aibu kwa chombo kikubwa kama Mahakama kushindwa kufanya kazi zake kwa sababu ya ukosefu wa karatasi tu, ikizingatiwa kwamba bajeti ya vifaa *(stationary)* imepitishwa na Baraza hili.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo Kamati imeona iliseme kwa hadhari kubwa na bila ya kukiuka mpaka wa kikatiba kwa vyombo hivi viwili kuingiliana, ni malalamiko na kilio cha wananchi kuhusu uendeshaji wa Mahakama zetu. Kamati imepata malalamiko mengi kutoka kwa wahusika mbali mbali wa Mahakama na ambayo ni ya msingi.

Mhe. Spika, baadhi ya malalamiko hayo ni kutokufuatwa kwa taratibu za sheria katika kuendesha mashauri. Hapa naomba nitoe mifano michache kama ifuatavyo:

Kutolewa hukumu kwa mashauri bila ya kuzingatia taratibu za kisheria ya mwenendo wa makosa ya jinai. Yapo mashauri ambayo yalikatiwa rufaani Mahakama ya Rufaa na kuamuliwa yaanze upya kwa sababu tu ya Majaji wa Mahakama Kuu wameshindwa kwa kutokujua au kwa makusudi kufanya muhtasari wa kesi kwa Wazee wa Mahakama kabla ya kutoa hukumu.

Mhe. Spika, Majaji ambao walilalamikiwa kupuuza taratibu hizi ambazo zipo wazi kwenye Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai baadhi yao ni wale ambao mwaka 2010 Jumuiya ya Wanasheria wa Zanzibar ililalamika sana kuhusu uteuzi wao kwa Mhe. Rais. Hoja kubwa ikiwa ni uwezo mdogo wa Majaji hao na wengine uadilifu wao katika kuendesha mashauri ni wa mashaka.

Mhe. Spika, yapo mashauri katika Mahakama za Watoto ambayo yamekaa muda mrefu hayajasikilizwa na mengine yamefutwa kutokana na wazee kuchoka kusubiri. Lipo shauri limefutwa kwa sababu tu mtoto aliyefanyiwa udhalilishaji ameshafika umri ambao ni zaidi ya umri aliokuwa nao wakati akifanyiwa udhalilishaji huo. Na mzee wake kuamua kutokuendelea na kesi hiyo kwa hofu ya kutonesha hisia za mtoto wake ambaye wakati akifanyiwa vitendo hivyo hakuwa akifahamu kitu. Na mzee huyo akiwa ameshatumia gharama kubwa za matibabu ya kisaikolojia kwa mtoto huyo.

Mhe. Spika, yapo pia baadhi ya makosa ya ubakaji na udhalilishaji wa kijinsia ambayo yamepewa hukumu ambazo wamepewa hukumu ambazo zipo kinyume na sheria. Ipo kesi ambayo imeshatolewa hukumu, mtuhumiwa wa kesi ya udhalilishaji wa kijinsia amepatikana na hatia na kutakiwa kulipa faini ya shilingi laki nne tu, ambazo shilingi laki tatu zimekwenda serikalini na shilingi laki moja alipewa mtoto aliyeathiriwa na kitendo hicho.

Mhe. Spika, baadhi ya wahusika wengine wa Mahakama wamelalamika sana kuhusu utaratibu wa Mahakama kutoa dhamana bila ya kuzingatia sheria na kupelekea baadhi ya watuhumiwa wanaopewa dhamana kutopatikana tena wanapoachiwa kwa dhamana au kutokufahamika taarifa zao vizuri pamoja na wadhamini wao.

Mhe. Spika, kamati imepata taarifa kutoka kwa baadhi ya wahusika wengine wa Mahakama kuwa utoaji wa dhamana katika Mahakama zetu umekuwa ni kama biashara ya duka inayoingia kipato baadhi ya Mahakimu na Makarani wa Mahakama. Mhe. Spika, kinachosikitisha kamati ni kuona kuwa malalamiko yote haya dhidi ya watendaji wa Mahakama licha ya baadhi yao kufahamika, hakuna hatua zozote zinazochukuliwa na mamlaka za kinidhamu kama vile Tume ya Utumishi ya Mahakama ambayo kwa mujibu wa vifungu vya 36 (4) na kifungu cha 81 vya sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011 ndio yenye mamlaka ya kutilia nguvu, kufuatwa kwa maadili ya utumishi wa umma na hatua za kinidhamu kama maadili hayo hayafuatwi.

Mhe. Spika, kamati imepata malalamiko mengi kwenye eneo hili la Mahakama ambayo mengine kutokana na mipaka ya Kikatiba tutaweza kuyaeleza mbele ya chombo hichi, hivyo kamati inamtaka Mhe. Waziri, kukaa na watendaji wa Mahakama na Tume ya Utumishi wa Mahakama kuyashughulikia malalamiko haya dhidi ya watendaji wa Mahakama ili kurudisha imani za wananchi wetu kwa Mahakama zetu na mwakani atakapokuja na ripoti ya utekelezaji aeleze hatua zilizochukuliwa.

Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (*DPP*)

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo kamati imeona ni vizuri kuliainisha hapa ni suala zima la ufinyu wa bajeti katika taasisi nyingi ambazo kamati imetembelea ikiwemo Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Kamati ilipofanya ziara katika ofisi hii ilipewa taarifa kuwa ofisi inakabiliwa na ufinyu wa bajeti, jambo ambalo husababisha mambo mengi ya ofisi kutotekelezeka.

Mhe. Spika, sambamba na changamoto hiyo, kamati inasisitiza serikali kuweka sera maalum ya malipo ya mishahara ya watumishi wake serikalini kutokana na ukweli kwamba watumishi wengi wa serikali wamekuwa wakizikimbia idara ambazo malipo yake hayafanani na baadhi ya idara nyengine. Idara hizo nyengine kama vile mamlaka na taasisi zinazojitegemea zimekuwa zikichukua watumishi wa fani sawa na idara nyengine wanazotofautiana nazo kimishahara.

Mhe. Spika, kutokana na changamoto hiyo, kamati inaiagiza wizara kushirikiana na Wizara ya Kazi na Utumishi wa Umma kwa lengo la kujadili

tena suala la malipo ya Mawakili wa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kutokana na mazingira magumu na hatarishi wanayofanyia kazi na maslahi madogo wanayolipwa.

Mhe. Spika, wakati kamati inawasilisha taarifa hii tayari Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imeshakimbiwa na waendesha mashtaka waandamizi wapatao wanne ambao wamekwenda kwenye taasisi nyengine kufuata maslahi zaidi. Mhe. Spika, tusisahau kuwa sheria Nam. 2 ya 2011 tuliyoipitisha hapa Barazani, imeibebesha Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka jukumu la kusimamia udhibiti wa matendo ya jinai kwa kuhakikisha kuwa washtakiwa wote wa makosa ya jinai wanafunguliwa mashtaka Mahakamani. Hii inamaanisha kuwa usalama wa jamii yetu unategemea kutokuwepo wahalifu mitaani ambao ndio wanaotuibia na wanaobaka watoto wetu na wanaofanya mauaji.

Mhe. Spika, wakati Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka inafanya jukumu hili kwa ufanisi licha ya hali na mazingira kuwa magumu ni vyema basi maslahi yao yakaimarishwa ili utendaji wao wa kazi uwe wa ufanisi zaidi. Kamati inasisitiza kuwa haitosita kuchukua hatua zilizo kwenye uwezo wake kwa mujibu wa sheria na Kanuni wakati wa bajeti kuhakikisha kuwa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka inapata kasma kwa ajili ya kutekeleza kazi zake.

Tume ya Kurekebisha Sheria

Mhe. Spika, kamati yetu inasisitiza serikali kutilia mkazo suala la upatikanaji wa jengo la ofisi kwa ajili ya Tume ya Kurekebisha Sheria ya Zanzibar ambapo kwa sasa hawana jengo la ofisi kutokana na matatizo yaliyojitokeza katika jengo walilokuwa wakilitumia hapo awali.

Aidha, kamati ilielezwa kuwa huenda jengo la Ofisi Mwanasheria Mkuu wakapatiwa baada ya ofisi hiyo kuhamia katika jengo jipya. Kamati inaliunga mkono wazo hilo na imeiagiza serikali kuharakisha kuwapatia jengo hilo mara tu litakaporudishwa serikalini na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Spika, changamoto kubwa inayokabili taasisi hii ni ukosefu ofisi za kudumu kwa tume hii umeleta athari kubwa ya utendaji kwa ufanisi. Kamati inashauri serikali kuipatia Tume ya Kurekebisha Sheria jengo la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu watakapohamia kwenye ofisi yao.

Mhe. Spika, katika jukumu lake la kufanya mapitio ya sheria, kamati iliiagiza Tume ya Kurekebisha Sheria kufanya mapitio ya sheria ya ushahidi sura ya 5 kwa umakini mkubwa, kwani imeonekana kuwa kuna changamoto nyingi za kitekolojia ambazo zinakwaza ushahidi. Kwa mfano hivi karibuni kumezuka

vitendo vichafu kwa baadhi ya vijana kuwarekodi wasichana picha chafu kwa kutumia vifaa vya *digital* kama vile simu na kuzisambaza katika mitandao. Ni vyema sheria hii ya ushahidi ikaweka vizuri masharti ya kutambua ushahidi utakapopatikana katika vyombo hivyo utumike ili kuwatia hatiani watuhumiwa.

Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali

Mhe.Spika, changamoto za ofisi hii ni nyingi sana ambazo nyengine zinaweza kuepukika endapo serikali ikiamua kuzitekeleza sheria ziliopo kwa lengo la kuweka utaratibu mzuri hasa katika suala la ukusanyaji wa mapato. Mhe. Spika, kamati inapendekeza serikali kuanza haraka mpango wa kuifanya ofisi hii kuwa sehemu pekee ya kupata taarifa ya mwenendo wa ulipaji kodi wa kampuni kwa kuipa uwezo, kusajili taarifa za ukaguzi wa mahesabu ya kampuni zinazowasilishwa ambao utaondoa kabisa ujanja wa baadhi ya makampuni kukwepa kodi.

Mhe. Spika, utaratibu wa sasa wa kampuni kusajili taarifa za ukaguzi wa hesabu za kampuni moja kwa moja kwenye taasisi za kulipa kodi, unarahisisha ukwepaji wa kodi kwa kuwasilishwa taarifa zisizo sahihi. Iwapo Ofisi ya Wakala ya Biashara na Mali itafanya kazi ya usajili ya taarifa za ukaguzi wa hesabu za kampuni na taasisi na mamlaka nyengine za ukusanyaji kodi zitaweza kupata taarifa sahihi kuhusu kampuni hizo.

Mhe. Spika, kamati ilipokuwa ikipokea taarifa katika Ofisi ya Wakala ya Usajili na Biashara, iliarifiwa kuwa huduma ya mtandao (*internet*) imekosekana kwa zaidi ya miezi mitatu. Kamati inasikitishwa sana na taarifa hiyo na inaiagiza wizara na serikali kuchukua juhudi za makusudi kurudisha huduma hiyo ili watendaji wa ofisi hiyo waweze kutekeleza majukumu yao ambayo yanahitaji sana kuwepo huduma hiyo.

Mhe. Spika, ofisi hii pia inakabiliwa na changamoto kubwa ya kukimbiwa na wataalamu adimu wa fani ya teknolojia ya habari (*IT*) ambao wanahitajika sana katika taasisi hiyo. Sababu kubwa ni maslahi duni wanayolipwa. Kinachosikitisha ni kuona kuwa wataalamu hao wanahamia kwenye taasisi nyengine za serikali hii hii, kamati inastaajabu ni kwa vipi wataalamu hao walipwe mishahara mikubwa kwenye taasisi nyengine za serikali hii hii wanazokimbilia na ishindikane kulipa mishahara hiyo kwenye taasisi wanazotoka.

Kamati inaendelea kusisitiza kuwa hili lipo kwenye uwezo wa serikali na hatua zichukuliwe ili wataalamu hawa waweze kutulia sehemu moja ya kazi.

Ofisi ya Vizazi na Vifo:

Mhe. Spika, inapongeza taasisi ya vizazi na vifo kwa kufanya ukarabati wa Ofisi ya Vizazi na Vifo Wilaya ya Kaskazini A, Kusini na Kati. Kamati inaiomba wizara kuongezea bajeti ofisi hii ili iweze kuendelea na ukarabati katika wilaya zilizobakia.

Afisi Kuu Pemba:

Mhe. Spika, kamati yetu ilifanya kazi zake Kisiwani Pemba ambapo katika Wizara ya Katiba na Sheria, kamati ilielezwa kuwa Ofisi Kuu Pemba inakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti, jambo ambalo hupelekea shughuli nyingi zilizopangwa na serikali kutofanyika. Kwa mfano mwezi wa Agosti, 2013 ofisi ilipatiwa shilingi milioni mbili kwa matumizi ya kazi za kawaida (*OC*) kwa ajili ya kuendesha vitengo vinne vya wizara ambapo zikigaiwa kila kitengo kitapata shilingi laki tano.

Mhe. Spika, fedha hizo ni kidogo sana kwa ajili ya kuendesha ofisi na matokeo yake ni kuzifanya shughuli zilizopangwa zisifanyike. Kutokana na hali hiyo, kamati inaagiza wizara kufuatilia suala hilo aidha kwa kuwaingizia fedha kwa wakati kama zinavyopatikana kutoka Wizara ya Fedha na endapo fedha hizo hazipatikani, wizara ichukue jukumu la kufuatilia fedha hizo zipatikane kwa wakati na hatimaye malengo yaliyopangwa kufanyika katika ofisi hii yatekelezwe kama yalivyopangwa.

WIZARA YA NCHI (OR) TAWALA ZA MIKOA NA IDARA MAALUM ZA SMZ

Mhe. Spika, katika wizara hii kamati iliendelea na utaratibu wake wa kujua miradi na kupokea taarifa za utekelezaji wa bajeti na kuona jinsi inavyotekelezwa na taasisi hizo. Baada ya kutembelea na kuona utekelezaji wa shughuli hizo, kamati ilitoa maoni, maagizo na ushauri kwa wizara kwa taasisi zake kama ifuatazo:-

a) Baraza la Manispaa:

Mhe. Spika, inaipongeza Baraza la Manispaa kwa kutekeleza vyema maagizo ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa mwaka uliopita. Aidha kwa hatua yake ya ununuzi wa gari nyengine za kufanyia usafi. Kamati inaiomba serikali kuongeza ruzuku kwa Baraza la Manispaa liweze kumudu kazi zake vyema na kuweka vizuri mji wetu. Utaratibu huo wa kuzipa Manispaa ruzuku ndio unaotumika kwa Manispaa nyingi duniani.

Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi:

Mhe. Spika, kamati yetu ilifanya ziara katika Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi na kupokea taarifa ya utekelezaji pamoja na kupewa baadhi ya changamoto ambazo baadhi yake zimekuwa zikikwamisha juhudi za Halmashauri hiyo katika utekelezaji wa majukumu yake.

Kamati ilielezwa kuwa Halmashauri inakabiliwa na changamoto ya kutokujitosheleza kwa sheria ziliopo ambazo zimepitwa na wakati, baadhi yake husababisha mambo mengi yanapangwa kutotekelezeka.

Mhe. Spika, imepatiwa maelezo na wizara kuwa tayari taratibu zinakamilika za sera na sheria za Serikali za Mitaa, kupewa kwa wadau na hatimaye kuletwa Barazani kujadili na kupitishwa. Kamati inaiomba wizara kuharakisha taratibu hizo ili sheria hiyo iletwe Barazani haraka kwani muda mrefu umepita tokea taratibu hizo za kutengeneza hiyo zianze.

Aidha, marekebisho ya sheria ya Halmashauri yatasaidia kuondosha kilio cha muda mrefu kilichopo cha Madiwani kuangalia maslahi yao kama ilivyo kwa Wawakilishi wengine wa nafasi za kisiasa. Mhe. Spika, pia inaishauri serikali kufanya juhudi za makusudi kuzipatia Halmashauri usafiri ambao utatumika katika shughuli zake za kila siku. Kamati imesikitishwa sana wakati ikitembelea katika Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi na kusikia kuwa Halmashauri haina hata usafiri wa kufanyia shughuli zake. Hivyo, kamati inashauri waombewe japo msaada wa magari ambayo yatasaidia kuondoa baadhi ya changamoto ziliopo hivi sasa kama vile za kusafisha.

Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini A:

Mhe. Spika, haijaridhishwa na taarifa za utekelezaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini A ambayo ni asilimia 25 tu ya utekelezaji wa bajeti uliofanyika. Kiwango hiki cha utekelezaji ni kidogo kwa vile Halmashauri hii ndio pekee iliopo katika eneo ambalo lina vyanzo vingi vya makusanyo kuliko Halmashauri nyengine. Kamati inataka maelezo kwa nini utekelezaji umekuwa hafifu kiasi hicho.

Chuo cha Mafunzo:

Mhe. Spika, kamati ilifanya ziara katika baadhi ya Vyuo vya Mafunzo vya hapa nchini na kuelezwa changamoto mbali mbali ikiwemo ya mrundikano wa mahabusu wengi katika vyuo hivyo. Kamati ilifanya ziara siku ya tarehe 25 Novemba, 2013 katika Chuo cha Mafunzo Kilimani ambapo idadi ya

rumande ilikuwa ni 187. Wanafunzi waliokuwa ndani siku hiyo walikuwa ni 73 ambapo idadi hii kubwa ilikuwa ni ya rumande.

Mhe. Spika, kutokana na ufinyu wa bajeti uliopo katika Chuo cha Mafunzo, hivi sasa mrundikano huo wa rumande ni mzigo mkubwa sana kwa idara hiyo ambapo kwa mujibu wa sheria, idara ina wajibu wa kuwalisha rumande hao hadi hapo watakapopatiwa hukumu zao. Kutokana na umuhimu wa jambo hili kamati inashauri suala hilo lipewe uzito kwa kuweka bajeti ya ziada kwa vile idadi ya mahabusu inaongezeka kwa wakati bajeti inabakia vile vile.

Mhe. Spika, aidha katika Idara ya Chuo cha Mafunzo, kamati ilipata changamoto nyingi kama inavyoonekana katika ripoti yetu ya kamati ambapo changamoto nyengine iliopo ni ukosefu wa vitendea kazi katika vitengo vilivyoanzishwa kwa lengo la kutoa mafunzo kwa wanafunzi wanaopelekwa humo ili wanapotoka wawe raia wema.

Katika ziara hiyo kamati ilipata nafasi ya kuzungumza na mahabusu pamoja na wanafunzi waliokuwemo ambapo miongoni mwao walitoa mawazo kwa serikali ambapo kamati imekubaliana nayo na kuiomba serikali iifanyie kazi wazo hilo.

Mhe. Spika, kamati ilipewa wazo la kuishauri serikali kufikiria kuwashirikisha wadau na wawekezaji kuwaruhusu kuwekeza katika miradi ya Vyuo vya Mafunzo kwa lengo la kuvifufua vitengo mbali mbali kikiwemo cha ushoni, useremala na vyenginevyo.

Kamati ilikubaliana na wazo hilo kutokana na ukweli kwamba hivi sasa vitengo hivyo havifikii lengo lililokusudiwa kutokana na ukosefu wa vifaa. Kamati pia inaiomba serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kushirikiana na Wizara ya Nchi (OR) Idara Maalum za SMZ kukipatia Chuo cha Mafunzo Kilimani eneo la ziada liliopo barabara ya Miembeni Mafunzo kwa ajili ya kuendelea na miradi ya uzalishaji mali.

Mhe. Spika, kamati yetu ilitembelea mradi wa ujenzi unaoendelea hivi sasa katika Chuo kipya cha Mafunzo kilichopo Hanyegwamchana ambapo ujenzi huo ni mkubwa na unahitaji fedha nyingi. Kutokana na ukubwa wa mradi huo kamati inashauri wizara na serikali kwa ujumla kufanya utaratibu wa kuuchukua mradi huo wa kutafuta wafadhili watakaosaidia ujenzi huo ambao unahitaji fedha nyingi mpaka kukamilika kwake.

Mhe. Spika, Chuo cha Mafunzo kilichopo Ubago nacho kinakabiliwa na changamoto ya ubovu wa njia ya kuelekea chuoni, deni kubwa la umeme pamoja na ubovu wa vyumba vya wanafunzi. Kamati inashauri serikali

kutatua changamoto hizo pamoja na kufanyia matengenezo vyumba vya wanafunzi na mahabusu ambavyo vingesaidia kupunguza mrundikano wa mahabusu wanaotoka Mkoa wa Kusini katika Chuo cha Mafunzo Kilimani.

Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM):

Mhe. Spika, inatoa pongezi kwa Kikosi cha KMKM kwa uienzi wa hoteli kubwa ambayo hivi karibuni ilifunguliwa rasmi na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya sherehe za miaka 50 ya mapinduzi ya Zanzibar. Pamoja na pongezi hizo kamati inaiomba serikali kusaidia upatikanaji wa vifaa vya hospitali kwa vile hospitali ile ni kubwa na inahitaji vifaa hasa ikizingatiwa kuwa baadhi ya huduma ya hospitali kuu ya Mnazi Mmoja zimehamishiwa pale pamoja na uwezo wa hospitali ile kulaza viongozi wakuu wa kiserikali.

Mhe. Spika, changamoto nyengine za KMKM ni uhaba wa fedha za ujenzi wa Chelezo na mafuta ya kazi za operesheni za dharura. Kamati inaiomba serikali kukipatia kikosi hicho fedha za ujenzi wa Chelezo ambacho kimeshakuwa kikongwe pamoja na fedha za mafuta katika operesheni zao za dharura ambazo mara nyingi zinakabili kikosi kikiwa hakina fedha.

Mhe. Spika, suala la uokozi ni suala ambalo limekuwa na changamoto hapa nchini. Kamati yetu ilipofanya ziara katika Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo ilielezwa kuwa changamoto kubwa iliopo ni ya ukosefu wa vifaa vya uokozi ambapo *wetsuit* pamoja na vifaa vyengine ni vichache sana. Kamati inaiagiza serikali kulichukulia uzito suala hilo kwa kuipatia bajeti ya kutosha Idara hii kwa lengo la kukidhi mahitaji yake vikiwemo vifaa vya uokozi.

Jeshi la Kujenga Uchumi:

Mhe. Spika, kamati ilifanya ziara katika Jeshi la Kujenga Uchumi na kujionea hatua mbali mbali za kimaendeleo zilizofikiwa na jeshi hilo ukiwemo ujenzi wa Skuli ya Ufundi Mtoni. Kutokana na hatua iliyofikiwa hivi sasa katika ujenzi huo, kamati inalipongeza sana Jeshi la Kujenga Uchumi kwa hatua iliyochukua ya kujitolea kujenga skuli ile ambayo itakuwa ni mkombozi kwa vijana wengi Wakizanzibari ambao wengi wao hawana ajira za kudumu.

Mhe. Spika, kutokana na umuhimu wa skuli ile ambayo ulikwenda wewe kuizindua ujenzi wake katika maadhimisho ya miaka 50 ya mapinduzi ya Zanzibar, kamati inashauri wizara na serikali kwa ujumla kulisaidia Jeshi la Kujenga Uchumi katika ujenzi wa skuli ile kwenye bajeti ijayo ya maendeleo

kwa kuwaingizia shilingi milioni mia tatu kwa kila mwaka hadi utakapomalizika ujenzi wake.

Mhe. Spika, kamati pia ilipewa taarifa kuwa kuna vijana ambao wanajitolea kufanya kazi katika jeshi hilo ambapo malipo yao ni shilingi elfu moja na mia tatu. Kwa sasa kuna mpango wa kutaka kuwaongezea posho hilo shilingi elfu kumi na tano. Kamati inakubaliana na wazo hilo na kuwapandishia posho vijana hao kutokana na hali halisi ya maisha ilivyo na kuwapa moyo zaidi ili kuweza kujituma katika shughuli wanazozifanya.

Kamati inatoa angalizo kwa Idara Maalum kuwa mpango unaandaliwa wa kamati kutembelea na kukagua miradi yote ya Idara ya Maalum ili kujua uhalisia wa miradi yenyewe.

Kikosi cha Zimamoto na Uokozi:

Mhe. Spika, kamati ilipokuwa inakagua shughuli za kazi za Kikosi cha Zimamoto na Uokozi ilipewa taarifa kuwa katika vituo vya Uwanja wa Ndege na bandari kuna changamoto nyingi za kiusalama zinazotakiwa kutatuliwa haraka kabla hazijaleta athari kubwa hapo baadae. Kamati inaiagiza Wizara ya Fedha, Wizara ya Nchi (OR) Idara Maalum na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kukaa pamoja na Idara ya Zimamoto na Uokozi kutafuta ufumbuzi wa changamoto za kiusalama katika maeneo ya bandari na uwanja wa ndege.

Kikosi cha Valantia:

Mhe. Spika, imepongeza sana hatua iliyofikiwa na kikosi hicho kwa kuanzishwa kiwanda cha kutengeneza viatu. Kutokana na juhudi hizi, kamati inavishauri vikosi vyote vya Idara Maalum za SMZ kuiga mfano huo wa kubuni mradi utakaowezesha kutatua baadhi ya changamoto ziliopo.

Hata hivyo, kamati inashauri wizara kufanya juhudi za kuwatafutia wafadhili nje ya nchi ili waweze kujifunza mbinu za ziada za kuimarisha kiwanda hicho, ikiwa ni pamoja na kukitafutia vifaa vya kisasa. Mhe. Spika, katika Kikosi cha Valantia kamati ilipewa taarifa kuwa kikosi kinakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa majengo ya ofisi na mabweni kwa makambi mengi ya kikosi pamoja na uhaba na uchakavu wa magari ambayo yanatumika katika shughuli mbali mbali za ulinzi na usalama hapa nchini.

Kutokana na hali hiyo kamati inaiomba wizara kufanya juhudi za makusudi kukisaidia kikosi hiki kuondokana na changamoto hizi hasa katika suala la

majengo ya ofisi na mabweni kwa ajili ya askari wapya wanaojiunga na kikosi hicho.

Mhe. Spika, kuna tatizo la jumla kwa Idara Maalum ambalo kamati inaitaka wizara kulipatia ufumbuzi wa haraka nalo ni kuhusu askari waliopo mafunzoni kuonekana wakidhurura mitaani, wanapoulizwa wanasema wametolewa wakajitafutie chakula halafu warudi makambini kwa ajili ya kulala. Kamati inaiomba serikali kutazama upya utaratibu huu kama upo kwa vile una hatari kwa mambo ya usalama na Idara Maalum.

Wizara ya Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma:

Mhe. Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ilijikita katika kushughulikia maeneo yenye umuhimu mkubwa na changamoto za msingi zinazokabili Ofisi ya Rais Kazi na Utumishi wa Umma kama ifuatavyo:-

Idara ya Nyaraka na kumbukumbu za Kitaifa:

Mhe. Spika, Idara ya Nyaraka imetupwa, ninasema hivi kwa masikitiko na uchungu mkubwa kutokana na hali tuliyoikuta wakati Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ilipotembelea. Idara ipo katika hali ya kusikitisha na kwa mtazamo wa haraka haraka unaweza ukahisi kama sio taasisi ya serikali. Changamoto tulizozikuta katika idara hii ni za hatari za kutisha kwa uwepo wa taasisi yenyewe na ustawi wa kiafya kwa wafanyakazi wake.

Mhe. Spika, wakati Idara ya Nyaraka ni taasisi yenye kuhifadhi urithi wa taifa, picha iliopo hivi sasa ni tofauti na ukweli huo. Hivi sasa Idara ya Nyaraka imefanywa kama vile ni eneo la kuhifadhia vitu vya kale visivyohitajika tena. Eneo lenyewe lipo hali hatarishi kiusalama, jengo dogo ambalo ni finyu halitoshelezi kuhifadhi kwa ufanisi nyaraka nyingi zilizomo. Aidha, kamati ilisikitishwa kuikuta taasisi muhimu kama hii ya nyaraka haina vyombo vya kisasa vya ulinzi kama kamera za kuangaza usalama kwa ukaribu *(CCTV Camera).*

Taarifa za wizi wa nyaraka:

Mhe. Spika, kamati imepata taarifa za kusikitisha kuhusu wizi wa nyaraka muhimu uliojitokeza kwenye idara hiyo. Wizi huo umekuja sambamba na kilio cha kuwekwa vyombo vya usalama *(CCTV Camera)* ambavyo licha ya kupigiwa kelele muda mrefu, wizara imeshindwa kuweka vyombo hivyo mpaka tokeo la wizi wa nyaraka limetokea.

Kamati ina wasi wasi kuwa ulegevu na kusita huko kwa wizara kushindwa kuweka vyombo vya *CCTV Camera* ambavyo bila shaka vyote vingesaidia kubaini wizi huo ni mpango makusudi uliokusudiwa kufanikisha wizi huo.

Mhe. Spika, kamati inapata wasi wasi huo kwa sababu agizo la kuweka *CCTV Camera* lipo kwa muda mrefu, halijatekelezwa na kwa mujibu wa taarifa kutoka idara yenyewe ambapo kamati imepatiwa. Hata Mhe. Rais kwenye mkutano wake wa wizara kwa kila robo ya utekelezaji wa bajeti (Bango Kitita) alishawishi na kusisitiza uwekaji wa vyombo hivyo vya kiusalama. Naye vile vile, agizo lake halijatekelezwa hadi wizi huo wa nyaraka umefanyika.(*Makofi*).

Mhe. Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala haitofumbia macho wizi huu mpaka ijulikane hatma yake. Na ninapenda nichukue nafasi hii kuitaka serikali kupitia wizara hii itoa maelezo ya kina na kuliambia Baraza hili kadhia nzima ya wizi huu ilivyotokea. Mhe. Spika, tunahitaji maelezo katika kadhia hii (*Makofi*).

Mhe. Spika, kamati inatoa maagizo yafuatayo kwa wizara ili kitendo hicho kisitokezee tena. Kuimarisha hali ya usalama wa eneo la nyaraka kwa kuweka *CCTV Camera*, kuandaa haraka mpango wa kuzifanyia ukaguzi nyaraka kila baada ya muda na ripoti ya ukaguzi huu iletwe kama sehemu ya ripoti ya utekelezaji wa wizara kwenye Baraza hili.

Aidha, agizo hili lihusishe taasisi nyengine yenye kuhifadhi nyaraka kama vile Ofisi ya Vizazi na Vifo, Wakfu na Mali Amana na kadhalika. Serikali kupitia vyombo vyake vya usalama kufanya uchunguzi wa tokeo hilo na kila aliyehusika bila ya kumuonea haya achukuliwe hatua zinazostahiki.
Aidha taarifa za uchunguzi huo ziletwe Barazani.

Mhe. Spika, mbali na hali hiyo, kamati ilipata mshtuko mkubwa kuona Idara ya Nyaraka ambayo ni taasisi ya serikali haina fanicha zenye viwango angalau vya kawaida. Ni mara kwanza tokeo kamati hii kufanya ziara katika idara na taasisi mbali mbali za serikali kukuta idara ya serikali ina fanicha zilizofungwa kamba ya katani.

Mhe. Spika, unyonge na upweke wa Idara ya Nyaraka ulishuhudiwa kipindi kamati ilipotembelea na kukuta shughuli nyingi za utekelezaji zimesita na wafanyakazi wamekaa wakiwa hawana kazi ya kufanya. Kamati ilipotaka kujua iliambiwa kuwa tatizo kubwa ni ukosefu wa fedha ambazo licha ya kuidhinishwa kwenye bajeti na Baraza hili, fedha hizo haziingizwi katika Idara ya Nyaraka ipasavyo na kusababisha kusita kwa kazi nyingi za msingi walizojipangia kutekeleza.

Mhe. Spika, ninapenda kulikumbusha Baraza lako kuwa mnamo mwezi wa Julai mwaka 2013 Baraza hili lilipitisha makadirio, mapato na matumuzi ya Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka 2013/2014, ambapo jumla ya shilingi bilioni nane nukta tano ziliombwa kwa kazi za kawaida na maendeleo na Baraza hili lilipitisha.

Kati ya fedha hizo jumla ya shilingi mia tano na ishirini na tano milioni laki tano na sitini na tano zimekasimiwa kutumika katika Idara ya Nyaraka. Hata hivyo, wakati kamati inatembelea idara hiyo, imekuta baadhi ya vitengo vyake havijafanya kazi kwa zaidi ya mwaka mmoja kwa ukosefu wa fedha. Kutokana na hali hiyo kamati inauliza zile fedha zilizopitishwa na Baraza hapa kwa ajili ya idara hii zimepelekwa wapi.

Mhe. Spika, katika hali ya kuvunja moyo kabisa kamati imepata kufahamishwa kuwa Idara ya Nyaraka haina gari hata ya usafiri, gari anayotumia Mkurugenzi wa Idara hiyo ni ya kuazima kutoka idara nyengine ambayo wamepewa hukumu ambazo zipo kinyume na sheria. Ipo kesi ambayo imeshatolewa hukumu, mtuhumiwa wa kesi ya udhalilishaji wa kijinsia amepatikana na hatia na kutakiwa kulipa faini ya shilingi laki nne tu, ambazo shilingi laki tatu zimekwenda serikalini na shilingi laki moja alipewa mtoto aliyeathiriwa na kitendo hicho.

Mhe. Spika, baadhi ya wahusika wengine wa Mahakama wamelalamika sana kuhusu utaratibu wa Mahakama kutoa dhamana bila ya kuzingatia sheria na kupelekea baadhi ya watuhumiwa wanaopewa dhamana kutopatikana tena wanapoachiwa kwa dhamana au kutokufahamika taarifa zao vizuri pamoja na wadhamini wao.

Mhe. Spika, kamati imepata taarifa kutoka kwa baadhi ya wahusika wengine wa Mahakama kuwa utoaji wa dhamana katika Mahakama zetu umekuwa ni kama biashara ya duka inayoingia kipato baadhi ya Mahakimu na Makarani wa Mahakama. Mhe. Spika, kinachosikitisha kamati ni kuona kuwa malalamiko yote haya dhidi ya watendaji wa Mahakama licha ya baadhi yao kufahamika, hakuna hatua zozote zinazochukuliwa na mamlaka za kinidhamu kama vile Tume ya Utumishi ya Mahakama ambayo kwa mujibu wa vifungu vya 36 (4) na kifungu cha 81 vya sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011 ndio yenye mamlaka ya kutilia nguvu, kufuatwa kwa maadili ya utumishi wa umma na hatua za kinidhamu kama maadili hayo hayafuatwi.

Mhe. Spika, kamati imepata malalamiko mengi kwenye eneo hili la Mahakama ambayo mengine kutokana na mipaka ya Kikatiba tutaweza kuyaeleza mbele ya chombo hichi, hivyo kamati inamtaka Mhe. Waziri, kukaa na watendaji wa Mahakama na Tume ya Utumishi wa Mahakama

kuyashughulikia malalamiko haya dhidi ya watendaji wa Mahakama ili kurudisha imani za wananchi wetu kwa Mahakama zetu na mwakani atakapokuja na ripoti ya utekelezaji aeleze hatua zilizochukuliwa.

Kuhusu askari waliopo mafunzoni kuonekana wakizurura mitaani, wanapoulizwa wanasema wametolewa wakajitafutie chakula halafu warudi makambini kwa ajili ya kulala. Kamati inaiomba serikali kutazama upya utaratibu huu kama upo kwa vile una hatari kwa mambo ya usalama na Idara Maalum.

Mhe. Spika, katika hali ya kuvunja moyo kabisa, kamati imepata kufahamishwa kuwa Idara ya Nyaraka haina hata gari ya usafiri, gari anayotumia Mkurugenzi wa Idara hiyo ni ya kuazima kutoka Idara nyengine ya Makumbusho na Mambo ya Kale. Sambamba na hilo, Kamati imepata kufahamu kuwa wakati Makatibu Wakuu na Wakurugenzi kila leo wanasafiri kwenda nje ya nchi kwa ziara za kiserikali, Mkurugenzi wa Idara ya Nyaraka kwa mwaka mzima, ameshindwa kusafiri kwenda hata hapo Kisiwani Pemba, kufuatilia kazi za Ofisi ya Idara kisiwani humo kwa sababu ya ukosefu wa fedha, licha ya Baraza hili kupitisha kasma kwa ajili hiyo, jambo ambalo linasikitisha na kuvunja moyo!

Mhe. Spika, Kamati inachelea kusema kuwa serikali inalitumia Baraza hili kuwa kama muhuri wa kupitisha fedha za matumizi ya utekelezaji wa kazi na malengo ya idara na taasisi za serikali, halafu fedha hizo hazitumiki kwa matumizi hayo yaliyokusudiwa, vyenginevyo kamati inataka maelezo kwa nini Baraza limepitisha fedha kwa ajili ya utekelezaji wa malengo ya Idara ya Nyaraka na hadi hii leo malengo hayo hayajatekelezwa, ikiwemo uwekaji wa *CCTV*, pamoja na mambo mengine niliyokwishayaeleza.

Mhe. Spika, hali ya wafanyakazi wa Idara hii inaumiza na kusikitisha. Mazingira wanayofanya kazi ni hatari kwa afya zao, hali ya hewa ya eneo la uhifadhi siyo rafiki kwa afya za wafanyakazi, vyumba vya kuhifadhia nyaraka havina vipoza hewa (*AC).* Vile vile kitengo cha uhifadhi ambacho kimehifadhiwa dawa za kutibu nyaraka zinazoharibika nacho hakipo katika hali nzuri, na dawa zinazotumika nyingi zimeshapitwa na wakati. Kamati imepata hofu kuhusu mustakbali wa afya za wafanyakazi hao kwani mazingira hayo ni hatari kwa kazi, yanakwenda kinyume na Sheria ya Afya na Usalama Kazini, Sheria Nambari 8 ya mwaka 2005, sheria ambayo tumeipitisha kwenye chombo hiki cha uwakilishi wa wananchi.

Mhe. Spika, kamati inatoa tahadhari kwa serikali kuwa, kama tulivyoagiza kwenye ripoti ya kamati, kamati hii itakuwa ya mwisho kukubali bajeti ya wizara hii, iwapo changamoto hizi hazikutatuliwa kwa haraka. Kamati mbali

mbali zimeshatembelea Idara ya Nyaraka kwa awamu mbali mbali na kukutana na changamoto hizi hizi tulizozikuta, kamati hii haipo tayari tena kuachia hali hii iendelee wakati uwezo wa kuzitatuza changamoto hizo upo.

Mhe. Spika, Idara ya Nyaraka kisiwani Pemba nayo ina changamoto kama hizo, miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na changamoto ya nyaraka nyingi kuharibika kwa kukosekana dawa za kuzitibu (kuzirekebisha), ukosefu wa vifaa vya kuhifadhia (*scanner*), vifaa vya kujikinga vumbi kwa wafanyakazi (*mask*) na kadhalika.

Mhe. Spika, Nimechukua nafasi kubwa katika Wizara hii kueleza mbele ya Baraza lako tukufu, hali halisi inayoendelea kwenye idara hii kwa sababu tu, changamoto zinazoikabili Idara hii ni kubwa na athari yake ni mbaya kwa usalama wa urithi wa historia ya taifa letu, kwani kama alivyowahi kusema mwanafalsafa mmoja wa sanaa ya fasihi kuwa *"...taifa lisilojali na kutunza urithi wa historia yake ni kama vile mti usiokuwa na mizizi"* mwisho wa kunukuu.

Kamisheni ya Utumishi wa Umma

Mhe. Spika, kamisheni imeundwa kwa mujibu wa katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, kifungu cha 116 na utendaji wa kazi zake umefafanuliwa kwa mujibu wa sheria nambari 2 ya mwaka 2011, Sheria ya Utumishi wa Umma. Kamisheni imepiga hatua kubwa na tayari imeanza kutafuta wataalamu wa fani mbali mbali katika kutekeleza majukumu yake ya kitaalamu.

Mhe. Spika, kamati inapongeza juhudi kubwa za Kamisheni ya Utumishi wa Umma katika kuufanyia marekebisho mfumo wa Utumishi wa Umma, ili uondokane na ile dhana ya kufanya kazi kwa mazoea *'business as usual',* Kamati inashauri kuwa mbali na juhudi kubwa za kuelimisha kada ya Utumishi wa Umma, kuhusu uelewa wa Sheria ya Utumishi wa Umma, siyo vibaya yakafanyika majaribio madogo (*trials*) kwa kila kipindi, kwa wafanyakazi wa sekta ya Umma, yatakayofuatiwa na ukaguzi wa mara kwa mara, kupima uelewa wa wafanyakazi kuhusu Sheria ya Utumishi wa Umma na Kanuni zake.

Mhe. Spika, kamati inaitaka kamisheni kufanya utafiti wa haraka utakaosaidia kutatua tatizo la malipo ya mishahara kwa wafanyakazi wa fani moja katika utumishi wa umma, na kutoa mapendekezo yake serikalini kwa mujibu wa sheria. Kamati imeona katika taasisi mbali mbali za serikali, wataalamu wa fani adimu wakihamia katika taasisi nyeti, zenye kazi muhimu lakini maslahi yake madogo, na kukimbilia kwenye taasisi nyengine ambazo kazi zake hazilingani na taasisi wanazotoka lakini malipo yake makubwa. Kama

ilivyoelezwa kwenye ripoti ya kamati na maelezo ya muhtasari wa hotuba hii kwa Wizara ya Katiba na Sheria.

Tume ya Utumishi wa Umma

Mhe. Spika, Tume ya Utumishi wa Umma nayo ipo kwa mujibu wa Sheria Nambari 2 ya mwaka 2011, Sheria ya Utumishi wa Umma. Kamati imefurahishwa na namna ya tume hii inavyoendelea na majukumu yake na hivi sasa ufanisi katika taratibu za ajira umeanza kuonekana kuanzia matangazo ya kazi, maombi, uchanganuzi wa maombi, usaili, ajira yenyewe na vipimo vya afya kwa waajiriwa wapya.

Mhe. Spika, Kamati inasisitiza kuwa tume iwe inashirikiana kwa karibu na kitengo cha usalama cha serikali (*GSO*) kutokana na kasoro ya ucheleweshaji wa ajira unaosababishwa na kukosekana kwa uratibu baina ya taasisi hizi mbili. Aidha, kamati inaiomba wizara kuharakisha kufanikisha ufanisi wa ofisi hii kisiwani Pemba, kwani kamati ilipotembelea Pemba imekutana na changamoto ya kutowepo kwa wafanyakazi wa Tume ya Utumishi, kisiwani Pemba.

Mhe. Spika, kamati inakumbusha utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Waziri wakati wa kikao cha Bajeti 2013/14, ambapo aliahidi kuwa kanuni za sheria ya utumishi wa umma zitakuwa tayari ifikapo mwezi wa Oktoba mwaka 2013, lakini hadi sasa kanuni hizo bado hazijawa tayari. Kamati inaipa muda wizara kuhakikisha kuwa kabla ya kikao cha bajeti, kanuni hizo ziwe zimeshakamilika.

Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

Mhe. Spika, kamati haina shaka na dhana nzima ya kuwa na mfumo wa teknolojia ya Habari na Mawasiliano, lakini inataka kueleza machache katika idara hii. Itakumbukwa kuwa mradi wa "*e- government*" ulizusha mjadala mkali ndani ya Baraza hili, wakati wa kikao cha Bajeti cha 2013/14, hadi baadhi ya Wajumbe wako mahiri wakataka iundwe kamati teule kuchunguza mchanganuo wote wa fedha za mradi wa "*e- government*".

Mhe. Spika, mjadala huo ulipelekea hekima kubwa na busara za Mhe. Spika ilibidi zitumike, ili kuwaridhisha Wajumbe ambapo ulielekeza kuwa suala hili halina haja ya kuundiwa kamati teule, bali kamati za kisekta zichukue juhudi ya kulifuatilia suala hili na kuja kutoa maelezo.

Mhe. Spika, naomba nichukue nafasi hii kuliambia Baraza lako kuwa, licha ya kuomba kupatiwa mchanganuo huo, hadi tunaleta ripoti hii, Kamati ya

Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza lako tukufu, haijapewa mchanganuo huo wa fedha za mradi wa "*e-government*". Hii inakwenda kinyume na Sheria ya Haki, Fursa na Kinga za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Sheria Nambari 4 ya mwaka 2007, ambayo imetoa haki kwa Wajumbe na Kamati za Baraza kupatiwa taarifa wanazohitaji kutoka serikalini.

Mhe. Spika, kamati inakumbusha kuvunjwa kwa sheria hii siyo mara ya kwanza na watendaji wa serikali. Kamati mbali mbali za Baraza zilizokuja kuwasilisha ripoti zao ndani ya Baraza hili, pamoja na Wajumbe zimeshalalamika jambo hili na hakuna hatua stahiki zinazochukuliwa. Kutokana na hali hiyo, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inashawishika kuamini kuwa kuna haja ya ile kamati teule kuundwa, kwenda kutizama hicho kinachotakiwa kisijulikane kwa wananchi, na kuletwa hapa Barazani kikajulikana.

Idara ya Ajira

Mhe. Spika, changamoto ya ajira ni kubwa kwa vijana wetu hasa wanaomaliza masomo. Kamati inatambua juhudi za serikali katika kutengeneza njia mbadala za ajira kwa vijana wetu. Hata hivyo, mikakati hiyo haiwezi kufanikiwa iwapo kama serikali haitaipa msukumo sekta binafsi, ikawa ndiyo mbadala wa tatizo la ajira kwa vijana wetu. Serikali haina budi kuweka mfumo wa ufanisi ambao utazilazimisha sekta binafsi kutoa vipaumbele vya ajira kwa vijana wetu, hususan katika sekta ya utalii.

Mhe. Spika, Kamati inapongeza juhudi za Idara ya Ajira za kuweka mfumo wa ukusanyaji wa taarifa za soko la ajira, ambao umepelekea vijana wengi kupatiwa ajira katika nchi za nje kupitia wakala binafsi. Hata hivyo, kamati inashauri idara kutopuuza changamoto za ajira hizo za nje kwa vijana wetu, ili wasije kuangukia mikononi mwa mawakala ambao wanatumia vibaya fursa hiyo.

Idara ya Afya na Usalama Kazini

Mhe. Spika, majukumu makubwa ya idara hii, ni kusimamia Sheria ya Afya na Usalama Kazini, Sheria nambari 8 ya mwaka 2005. Utekelezaji wa sheria hii bado haujawa na ufanisi, kwa vile idara hii imekuwa Idara rasmi kuanzia mwaka 2010. Kamati inashauri serikali kuiwezesha idara hii kufanyakazi, kwani yapo maeneo mengi ya kazi yenye mazingira hatarishi kwa wafanyakazi, ambayo ni kama bomu linalosubiri kuripuka. Ni vyema idara hii ikawezeshwa kufanyakazi ili kuyakagua maeneo hayo kabla hayajaleta maafa.

Mhe. Spika, dhana kubwa moja wapo ya kuwa na Sheria ya Afya na Usalama Kazini, ni kuzuia majanga kwa wafanyakazi kwenye maeneo ya kazi, kwa lengo la kulinda afya za wafanyakazi pamoja na mazingira salama ya kufanya kazi. Kumekuwa na mazoea katika nchi yetu ya kutochukua hatua kwa ishara au dalili za hatari mpaka pale hatari yenyewe inapotokea.

Mhe. Spika, kamati inasikitika kuona kuwa ipo sheria nzuri ya kulinda afya na usalama kazini, lakini bado nchi yetu ina maeneo mengi ya kazi ambayo viwango vyake vya usalama ni vya kutisha kama vile Idara ya Nyaraka, Vizazi na Vifo n.k ambako kuna harufu mbaya ya karatasi inayoathiri afya za wafanyakazi.

Chuo cha Utumishi wa Umma

Mhe. Spika, Chuo cha Utumishi wa Umma kinaendelea kupata mafanikio katika kukuza taaluma za watumishi wa Umma. Kamati inapongeza kwa hatua zilozifikiwa na inashauri wizara kutanua huduma za Chuo cha Utawala wa Umma Kisiwani Pemba, ili watumishi wa Umma wa Kisiwa cha Pemba wafaidike na huduma za chuo. Aidha, kamati inaiomba wizara kukisaidia chuo kupata fedha za mkopo kutoka *ZSSF* kwa ajili ya kuendeleza majengo ya chuo.

Mhe. Spika, chuo pia kinakabiliwa na changamoto ya mishahara duni ya watendaji na wahadhiri ambao licha ya kuwa na uwezo na viwango sawa na wahadhiri wa vyuo vyengine vya serikali, bado wanalipwa mishahara sawa na walimu wa sekondari. Kamati inashari serikali kuweka viwango vya mishahara vya walimu hao sawa na wahadhiri wa vyuo vyengine ili kuepusha na wao kukimbilia kwenye vyuo hivyo.

Mhe. Spika, kamati inakumbusha na kuitaka wizara kuharakisha malipo ya wajenzi wa majengo ya Chuo cha Tunguu ambao umefanywa na mafundi wa Chuo cha Mafunzo.

Hitimisho

Mhe. Spika, katika kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar, Kanuni za Baraza la Wawakilishi na Sheria nyenginezo, kamati imetoa maelekezo, maoni, ushauri na maagizo yake ambayo tunaamini kuwa yatasaidia katika kuleta ufanisi kwenye utekelezaji wa majukumu ya serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ na Wizara ya Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma.

Mhe. Spika, maelekezo na maoni hayo yalitolewa na kamati, kwa dhamira ya kuwawakilisha vyema wananchi wa Zanzibar na kuona kuwa maslahi ya wananchi hao, kwa mujibu wa sheria yanapewa kipaumbele. Kamati yetu inatumai kuwa maelekezo na maoni yaliyotolewa na kamati kwa wizara hizo, yatazingatiwa kwa lengo la kutoa huduma zilizotukuka kwa wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa kumalizia muhtasari huu, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi, inaushukuru uongozi wa wizara zote zilizo chini ya kamati, kwa ushirikiano mkubwa walioipatia kamati yetu katika kipindi chote cha kazi za kamati kwa Unguja na Pemba.

Kamati inatoa shukurani za pekee kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mhe. Pandu Ameir Kificho, Katibu wa Baraza la Wawakilishi na watendaji wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi, kwa kuiwezesha kamati hii kutekeleza majukumu yake vizuri,lakini zaidi kwa ushauri waliotupatia kamati yetu katika kipindi cha utekelezaji wa majukumu yake.

Mhe. Spika, kamati inawashukuru makatibu wa kamati hii Ndugu Aziza Waziri Kheir na Ndugu Khamis Hamad Haji, kwa kuratibu na kutekeleza majukumu yao ya kuisaidia kamati na Wajumbe wa kamati kwa umahiri mkubwa na wajumbe hao kuweza kutekeleza kazi zao kwa ufanisi.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi).*

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, nakushukuru sana kama kawaida yako kuniona Mjumbe wako na kunipa nafasi hii ya mwanzo, ili kuweza kufungua milango na Waheshimiwa wenzangu na wao kuweza kuchangia kwa ufasaha kabisa.

Mhe. Spika, ...

Mhe. Spika: Msisitizo wetu Waheshimiwa Wajumbe, muda wetu kidogo uko finyu, kwa hivyo tujitahidi twende kwenye *point* moja kwa moja ambazo tumejipangia, na tuutumie muda vizuri kwa maana tufupishe mijadala, ili shughuli zetu zote zimalizike, mbele tuna majukumu mazito ambayo yanatusubiri. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, endelea.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, nakwenda kule kule ambako ulikokusudia kutuambia. Mhe. Spika, mimi naanza kwa Mhe. Mwanasheria Mkuu, nina wazo moja ambalo ni zuri sana na nimeshalisema sana katika Baraza lako hili tukufu katika bajeti, lakini nilifikiria kwenye kamati kutakuwa na maelezo ambayo yataweza

kunifurahisha, lakini mpaka sasa hivi sijaona hicho kitu, naomba nikieleze ili Mhe. Mwanasheria Mkuu anisikie.

Mhe. Spika, nilisema kuwa kutokana na ubadhirifu ambao unafanywa kwa kupitia wawekezaji ambao tunapanda ndege na kwenda kuwachukua na kuwaleta hapa. Kwa hivyo, niliomba kuwepo na mahakama maalum kwa ajili yao. Mhe. Spika, ushauri huu ni mzuri sana, kwa nini tusiweke mahakama hizo, tunawanyang'anya bure hawa wazungu halafu zikienda kesi zinapoteza muda, wanakopa mikopo kule nje, tunajiweka katika sifa mbaya. Hawa wawekezaji wetu tunakwenda kuwachukua nje na kuwaleta hapa, halafu tukifika hapa tunawanyang'anya ardhi na hakuna sababu yoyote, kwa nini tusiwawekee mahakama yao? Hebu tuweke hiyo mahakama, ili tuweke sifa nzuri katika nchi yetu na tuonekane kuwa tunawajali na wao. Tunanuka vibaya sana kutokana na hali ilivyo, tunawanyang'anya sote. Kwanza ukiwa kiongozi na wewe unawajibika.

Mhe. Spika, kelele zangu hizi sasa ndio zitakuwa mwisho kwenye bajeti nitapewa fikra nzuri, nitaambiwa mahakama hiyo itakuwa imo katika matayarisho. Mifano ipo katika nchi za wenzetu hebu twendeni, mifano ipo kwenye nchi nyingi tu. Hebu turuke mara moja, ikiwa tunaweza kwenda kuwachukua halafu tushindwe kuunda mahakama. Naomba sana suala hili lifikiriwe.

Vile vile Mhe. Spika, kwenye ripoti hii ya Mwenyekiti amesema kutokana na nyaraka. Mhe. Spika, juzi tulipokwenda katika suala la kiwanda chetu kipya cha uchapaji, tulipokuwa katika ziara, Mhe. Ali Mzee aliwauliza, nyinyi nyaraka ziko wapi? Mimi nikaona labda siku ile Mhe. Ali Mzee anatupotezea muda tu, kumbe ina mantiki yake na ina busara zake. Hatuzithamini nyaraka za asilia. Mimi nasikitika sana kusikia kuwa nyaraka zimeibiwa na hakuna chochote kilichofanyika.

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais fanya kazi, hebu wakamate tu, haiwezekani leo nyaraka ziibiwe ambazo zina kumbukumbu za nchi yetu, ambapo watu wanatoka nje kwa kuzifuata hapa na kutia pesa za nje, halafu leo mtu azichukue tu kisha tunakaa kimya tu, haiwezekan!

Mhe. Spika, kuna rafiki yangu mmoja ana kikampuni chake kidogo anaitwa Tawfiq, basi kabla hujaingia ndani tu unaonekana, seuze serikali kuweka chombo kama hiki, kweli tunafanya mzaha Mheshimiwa hatujawa *serious* katika utendaji wa kazi. Mhe. Spika, suala hili hatukubaliani nalo ni lazima kuundwe tume ili ifuatilie suala hili la nyaraka zilizoibiwa, kwa nini na nani aliyeiba na mpaka leo Rais hajui, kwenye bango kitita Rais hajui.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, suala hili sio la kulifumbia macho hata kidogo. Halafu ukiiona hiyo ofisi yake mheshimiwa ni bora tuitie katika nyaraka ya kumbukumbu nayo, ile ofisi yenyewe tuitie kwenye makumbusho ya nyaraka ya serikali. Hiyo ofisi yenyewe ukiiona Mhe. Spika, ni lazima ziibiwe kwa hali ile, kwa sababu tumeidharau kwa kiasi kikubwa sana.

Mhe. Spika, naomba suala hili tusilifumbie macho, mimi sikubaliani nalo hata kidogo na wala halinitii dhambini suala hili. Kwa hivyo, mara moja suala hili lifuatiliwe ili lifikie pahala penye muafaka mzuri.

Mhe. Spika, tunakwenda kwenye mahakama, kuna watendaji makarani, masjala na mpaka kufikia kuwapata hao majaji wenyewe. Mhe. Spika, mahakama zetu *alhamdulillah*, kuanzia Majaji Wakuu mpaka wa chini wametimiziwa haja zao na wamefikia katika hali nzuri ya kifedha, seuze hawa makarani unafikiri wasipoteze nyaraka, wakati mtu mshahara wake mdogo. Kinachonichekesha wale makarani wenyewe wana *diploma*, utawakuta majaji wengine wana *diploma*, sijui ni kigezo gani kimetumiwa hapa kuwa huyu asipewe fedha ambayo inakimu kutokana na hali yake na usomi wake. Sijui hawa Utumishi wametumia kigezo gani.

Mhe. Spika, juzi tuliambiwa imeongezwa Shs. 25,000, kweli tunakwenda kuwaongezea Shs.25,000, hii ni hakuna kitu na hatujawa *serious.* Katika kipindi kilichopita nilisema kuhusu makarani wa mahakamani, hawa ni muhimu kabisa, kwa sababu anapomaliza jaji *file* lile anampa karani wake na wakati unampa mshahara mdogo, anakuja mtu na mabilioni ya fedha pale anataka kesi yake ife, unadhani mashara nini Mhe. Spika, lazima litapotezwa *file*, tusifanye mchezo na mambo yenyewe hatuna hizi *CCTV* ndio kabisa itakuwa mchezo umekwisha.

Kwa hivyo, naomba wafanyakazi hawa waheshimike kabisa kutokana na sheria ambayo imewekwa na mahakama siku hizi kwamba huwezi kuajiriwa mpaka uwe na *diploma*, na wafanyakazi *alhamdulillah* wengine wanachukua digirii sasa hivi, karani huyo, asikimbie unadhani akipata pahala, tutakimbiwa kila siku Mhe. Waziri. Keshasikia pahala kuna fedha nyingi atabakia tu pale mahakamani akahangaika tu na karatasi aumie macho, hata siku moja hatokaa.

Mhe. Spika, mimi nasema sheria iwekwe wazi, waachiwe waende wakatafute maslahi, hata kama umemsomesha mwache aende, hutaki kumuhifadhi.

Mhe. Spika, nizungumzie kuhusu changamoto za mahakama zetu. Nasikitika sana kusikia mahakama inakosa karatasi ya kuweza angalau kumuandikia mtu

amri ya kumwita, suala hili linasikitisha sana. Sijui tatizo ni nini, labda niseme ni tatizo la uingizwaji wa fedha, siwezi kusema wizara yenyewe inaweza kuzorota, hapana. Hebu jamani tuyaangalieni mahitaji muhimu ya mawizara husika, tuwape kipaumbele cha kuweza kuwasaidia. Leo mtu anataka kuitwa inatafutwa karatasi ya kuweza kumuita inakosekana, ee! Mwenyezi Mungu, kwa kweli inasikitisha sana, tunaomba suala hili liweze kufikiriwa sana.

Mhe. Spika, twende kwa ma-*assessor*, ma-*assessor* wetu bado fedha ni kilio kabisa, wamepewa fedha kidogo zilizobakia ni nyingi sana, naomba na hili tuwafanyie haraka sana, jitahidi sana Mhe. Waziri ili uweke jina katika wizara yako kwa ajili ya kuwasaidia hawa ma- *assessor*. Wanahudhuria vizuri lakini malipo yao ni kidogo sana. Naomba pesa zao walipwe kwa wakati, wale watu ni maskini na wanakaa mbali, tuwahurumie ndio ajira yenyewe hiyo, Mwenyezi Mungu kawajaalia kuwapa ajira hiyo, basi tuwapeni na wao haki yao, tuwafikirie sana hawa ma-*assessor* katika ripoti hii kutokana na hali halisi ilivyo.

Mhe. Spika, nakubali mahakama inachelewesha kesi na kumbukumbu mbili mimi ninazo ambazo nazijua. Kuna kesi moja ya Mwera, kuna mama mmoja kaunguziwa nyumba yake kwa moto na mpaka leo kesi inakwenda ikirudi, naomba sana mahakimu waangalie umuhimu wa zile kesi zenyewe kuzifanya haraka. Mhe. Waziri naomba kila baada ya muda fulani uwe unaangalia mwenendo wa kesi, kesi zinakuwa zinachelewa na zinafika pahala mpaka mtu anafika kuzaa yule mtoto kesi bado haijatolewa hukumu yoyote. Naomba sana Mhe. Waziri hili suala la *mention* wakati mwengine lipunguzwe kutamkwa, twende na hali halisi.

Mhe. Spika, kuna kesi nyengine iko Mfenesini na hawa wasimamizi polisi wanakwambia kila siku kuwa ushahidi haujakamilika, je tunataka ushahidi wa namna gani ukamilike. Ili kupoteza muda, najua kuna muda fulani ile kesi kila siku ushahidi haujakamilika, Jaji atafika pahala atasema kesi ifutwe, tutakuwa tumeshampotezea haki yule mtu aliyepigwa, kesi ambayo ni shambulio kali.

Mhe. Spika, kwa nini kila siku tunaambiwa ushahidi haujakamilika. Hebu tuangalie hali halisi, rushwa bado ipo, kwa nini unapoteza muda wakati kitu kinaonekana. Naomba suala hili lifikiriwe katika mahakama zetu, hawa watu ambao wanasimamia kwenye baadhi ya kesi nyengine waangaliwe kwa makini na kuwe na nidhamu.

Mhe. Spika, sio kila siku kesi leo *mention*, anakwenda kumwambia Jaji oo!, kesi hii mimi bado sijawa tayari, kwa hivyo iseme tu hivyo hivyo.

Haiwezekani. Mhe. Spika, mimi naomba suala hili lifikiriwe na kuweza kufanyiwa kazi.

Mhe. Spika, nije sehemu ya Idara ya Ajira. Mhe. Spika, hapa ndipo kwenye kilio, vijana wetu wamekuwa ni wengi sana hawana ajira na sisi ndio tutakuja kujibu suala hilo. Hapa nimeambiwa katika ukurasa wa 57, Idara ya Ajira katika vijana 273 wanaume. ee! ina maana hii 273 hivi kweli ndio vijana hawa wamepata nafasi za kazi. Mhe. Spika, hesabu hii sijui ikoje, au macho yangu sijavaa miwani. Hizi namba jamani mlioona naomba munisaidie, wanaume 61 na wanawake 212, hesabu hii sijui ikoje kama ni ya kirumi au ya wapi, siwezi kujua. Tumeambiwa hawa wamepata kazi katika nchi za nje wamekwenda vijana hawa.

Lakini pia nijiulize hapa ndani.Mhe. Spika, hatuko makini katika kuwasaidia vijana, tuseme ukweli na uwazi, hatuko *serious* kabisa, kama laiti tuko *serious* mimi nimeshasema sana katika Baraza hili Mheshimiwa, wahusika twendeni kwenye mahoteli tukafanye *research*. Tuna mahoteli mengi sana, *wallahi* kama tuko *serious* vijana wangemalizika kwenye vi-*jobless*, tungekuwa *serious* vijana ingekuwa sasa hivi mitaani huwakuti, Mhe. Spika, lakini hatuko *serious* tunasema tu. Kuwataka kwetu tunangojea kwenye uchaguzi tu ndio tuwathamini haiwezekani Mhe. Spika, hii ukweli tuseme mimi hapa lazima niseme.

Siku moja mimi kuna mtu mmoja juzi ananambia aa Mheshimiwa kila ukisema hivyo kuna watu wanakuwekea pingamizi jimbo lako watu wakunyime, na waninyime hakuna tatizo; mtoaji Mungu, mimi hanitishi kwa hilo lazima niseme, hatuko *serious* kwa vijana hata siku moja tuseme ukweli. Na iko siku watatupiga, hatuko *serious*, mahoteli hapa yaliyotuzunguka nchi hii ya Zanzibar, hapana Mheshimiwa hili mimi sikubaliani nalo linanitia uchungu sana, Mheshimiwa. Leo tunapewa *data* hizi za kitoto kabisa 284 aaa Mhe. haiwezekani bwana hebu tuwe *serious*.

Mhe. Makamu wa Pili nikikuelekeza wewe ni lazima kwa sababu wewe ndio mtendaji wetu, na nilisema mimi tubadilisheni Katiba keshokutwa ikija hapa tumpe meno Mhe. Makamu wa pili, tumpe meno ndio, aweze kusema sasa hivi Waziri wewe toka Katibu wewe toka, leo hana uwezo kusema hivyo na aseme uone hapo hakuna sheria hiyo, ni mfuatiliaji lakini anashindwa kutoa hukumu kwa sababu hana sheria hiyo. Basi mimi naomba sana Mheshimiwa tutapopanga Katiba yetu mpya tuangalie vigezo hivyo, tumpunguzie kidogo Rais tumwambie sasa mtendaji wako uliyetupa mwache afanye kazi yake.

Mheshimiwa mahoteli sasa hivi yametawaliwa na wageni, *wallahi* ilikuwa ni mzigo mmoja mzito, lakini ni mwepesi sana kwa Zanzibar kuweza kupata

kazi na kuweza kuondosha ugumu huo. Lakini leo nenda katizame. Mheshimiwa leo inasikitisha maana yake Wakenya walivyokuwa wengi mpaka wengine juzi wamekuwa majambazi sasa wanatembea kwenye mitaa yetu na silaha. Sheria hakuna Mhe. Spika tatizo lenyewe. Mhe. Spika, hatutochoka kusema, lakini iko siku ninakuhakikishia Mheshimiwa, vijana watakuja juu kwa kudai haki zao.

Mhe. Spika, ninawambia sana watu wa Idara ya Kazi, sasa hivi Mheshimiwa watu wetu wanafukuzwa kazi kinyume na utaratibu, ninaomba sana. Mheshimiwa kuna Chuo kile cha Utalii tumewasomesha watu wetu ili kuweza kwenda kufanya kazi na uwezo huo wanao, lakini utakuta wanasoma lakini kazi hawapewi. Mheshimiwa sasa hivi sheria tunazo lakini zimo ndani ya *briefcase* zetu, Mheshimiwa watu wanadhalilishwa. Mimi nomba sana ndugu zangu wakija Idara ya Kazi naomba sana.

Mheshimiwa niwashukuru sana ndugu zangu wa vikosi vya SMZ hasa KMKM kwa kutuletea jengo lile zuri sana la kisasa kabisa, niwashukuru kwa hilo na niwapongeze sana na wajitahidi kulienzi ili isiwe baadae badala ya uzuri likachakaa kwa muda wa siku tatu, naomba sana utawala unaohusika ukakamae kwa kuweka sheria kali na kuweza kulitunza.

Mhe. Spika, kamati yetu ilipotembelea Kikosi cha KMKM kuna kitu ambacho tulikiomba na mimi moja nilipewa hiyo, tulisema kupandishwa mishahara ya wafanyakazi wetu wa Vikosi na mpaka Tume ikaundwa lakini vyereje leo sijui ile Tume imeishia vipi naomba Mhe. Waziri kwanza nikusifu sana Mhe. Rais, Mheshimiwa hiyo nafasi pekee Mhe. Spika, ninakuomba sana nisiposema lile jambo nitakuwa Mheshimiwa sikujitendea haki ndani ya nafasi yangu. Mheshimiwa nilitoa wazo kuwa Mhe. Rais aangalie mtazamo wa kuwawekea Vikosi vya SMZ na ninashukuru sana Mhe. Rais hilo kalitenda ni msikivu Mhe. kalikubali na kamtafuta kijana mahiri, kijana bado damu inamwenda na ameanza ziara vizuri kuyatembelea hayo majeshi yetu, lakini la kusikitika Mheshimiwa naomba usiogope Mheshimiwa wangu Waziri watetee na maslahi yao ya mishahara naomba sana hilo.

Lakini la kumalizia Mheshimiwa halmashauri zetu ninashukuru sana Mheshimiwa, Halmashauri ya Kaskazini ‘B’ lakini na wao kuna watu ambao maofisa wa Afya wanapoendewa kule basi wasijitie kutaka kujipendekeza kwenye kamati wakawavuruga watu wengine, watu wengine wakawasifia, sote tunafanya kazi kitu kimoja Mbunge na Mwakilishi tunafanya kazi na tukiitwa tunakwenda wasijipendekeze kwa mtu tu, Mhe. Spika, naomba hiyo maafisa waangalie.

Naunga mkono ripoti hii asilimia mia kwa mia. Ahsante.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, na mimi nikushukuru kunipa nafasi hii nikaweza kuchangia ripoti hii au muhtasari wa ripoti iliyosomwa na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Mhe. Ussi Jecha Simai.

Mhe. Spika, kweli Baraza letu sasa hivi linaanza kukomaa, kwa sababu mwanzo kulikuwa kuna vigogo wachache lakini sasa hivi naona vigogo wanaongezeka. Mhe. Spika, lakini lazima nijisifu, najisifia matunda yangu kwa sababu Mwenyekiti huyu alikuwa Mjumbe wangu wa Kamati.

Kwa hivyo alitumia uzoefu mkubwa ambao niliokuwa nikiufanya katika kamati na kijana wetu sasa hivi amechukua mikoba. Ninamuomba sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais tusihangaike kumtafuta Warioba, nadhani Warioba sasa hivi tunaye, Mhe. Ussi Jecha Simai ripoti yake hii utadhani ile rasimu ya Katiba ambayo aliyoileta Jaji Warioba. Kwa hivyo Mhe. Rais akija akitafuta Warioba huko basi Warioba humu ndani tunaye.

Mhe. Spika, lakini pongezi hizi nataka niwapongeze sana wananchi wa Jimbo la Chaani kwa kweli kumchagua Mhe. Ussi Jecha Simai kuwa Mwakilishi wao ambapo na mimi ni mzaliwa wa Chaani huko, kwa kweli tumefanya kazi nzuri sana. Kijana ni mahiri, taarifa aliyoileta kwa kweli imejaa nyama. Sasa ni wajibu wetu sisi kama Wajumbe kuichangia ili kuweza kuishauri vizuri serikali yetu kutekeleza haya ambayo yaliyoelezwa na Kamati.

Mhe. Spika, baada ya shukurani hizo sasa nataka nianze kuja kwenye ripoti. Mhe. Spika, ripoti imeeleza mambo mengi kupitia Wizara mbali mbali na mimi nitajitahidi nichambue moja baada ya nyengine. Mimi nataka nianze moja kwa moja kama ilivyoeleza ripoti ukurasa wa kwanza mpaka wa tano, Idara ya Mahkama, Mkurugenzi wa Mashtaka na wengine ambao waliohusika katika kurasa hizi.

Mimi kwanza nataka niwapongeze ndugu zetu wa Idara ya Mahkama kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya ya kuweza kusimamia haki za wananchi kwa mujibu wa sheria tulizozitunga hapa Barazani. Lakini pamoja na hayo Mhe. Spika, lazima kuna baadhi ya mapungufu lazima tuambizane kwa sababu mambo haya lazima tuwe tunakumbushana wajibu wetu, sisi tunatunga sheria wenzetu wanatafsiri sheria serikali inatekeleza zile sheria ambazo zilizotungwa.

Sasa kuna ripoti hii ilivyoeleza juu ya udhaifu wa mahakimu wetu wanavyojaribu kutoa hukumu kutofuata zile taratibu. Na kwa kweli inapelekea kwamba baadhi ya wananchi kukosa haki zao kutokana na hukumu ambazo zilitolewa kinyume na utaratibu, kama kesi mfano alizozitoa

Mhe. Mwenyekiti hapa kwamba kuna baadhi ya kesi ambazo za mahkama ambazo wanatakiwa wawepo ma- *assessor* matokezeo yake ma- *assessor* hawakuwepo, kesi imetolewa maamuzi imempa *loophole,* yule mtu aliyetolewa hukumu akawa kazi yake ni rahisi kuweza kukata rufaa ili kui-*dilute* ile kesi. Sasa haya ni mambo ambayo hayakutakiwa hasa yafanyike katika ngazi hiyo ya mahkama.

Kwa hivyo mimi naomba sana wenzetu hawa wanapofanya kazi zao wajaribu zaidi kuangalia hizi sheria, kwa sababu sasa hivi Mheshimiwa wajanja wamekuwa wengi, hawa watu ambao wanahukumiwa wao wanakuwa hizo sheria wanazijua zaidi pengine hata kuliko wale mahakimu wenyewe. Kwa sababu mahakimu wanakuwa wameshajiamini kwa kuwa wamesoma lakini huyu ambaye ana tatizo yeye atatafuta kila njia ya kuweza kutoka.

Vile vile ninasikitika zaidi kwa hizi kesi za udhalilishaji Mhe. Spika. Kesi za udhalilishaji ni kesi ambazo tunazipigia kelele sana kwa kweli ingawa tunayoyazungumza Mhe. Spika, tayari yameshatolewa hukumu, lakini kutokana na zile hukumu zilivyotolewa sivyo hasa zile sheria ambazo tulivyozitunga. Leo kesi ya udhalilishaji mtu ameshaharibiwa leo faini mtu anapigwa laki nne Mheshimiwa maisha ya mtu ameshamharibu kisaikolojia, kwa kweli hali sio nzuri sasa. Kwa hivyo mimi nilikuwa naomba tu wenzetu hawa majaji wajitahidi sana kutimiza ule wajibu wao na majukumu yao ili haki iweze kutendeka. Kwa sababu Mhe. Spika, mnyonge akishadhulumiwa anakimbilia mahkmani, kwa hivyo mahkama inatakiwa itende uadilifu.

Mhe. Spika, bado suala la mahakimu wa mahkama ya mwanzo namuomba sana Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria suala hili nimeshalizungumza sana ingawa alinijibu akasema tayari maslahi yameshazingatiwa lakini bado yale malalamiko yapo. Sasa mimi naomba arudi kukaa nao tena, ninashukuru kwa hatua aliyoichukua kuzungumza nao mahakimu.

Kwa hatua ya mwanzo kwa kiasi fulani waliweza kufanikiwa lakini bado kuna baadhi ya marekebisho madogo madogo waweze kuyafanyia kazi ili na wenzetu hawa kwa sababu Mhe. Spika, kesi nyingi zinakwenda kwenye hizi mahkama za mwanzo, kwa hivyo hao wenzetu wanakuwa na kazi nyingi sana pengine hata kuliko wale majaji wa mahkama kuu. Sasa hawa kama maslahi yao hayakuangaliwa vizuri ndio pale uchakachuaji wa kesi wakati mwengine watu ambao wanaweza wakachomekea chomekea ili kuhakikisha kwamba wanawatengenezea maslahi yao vizuri ili kesi zao ziweze kushughulikiwa vile wanavyohisi wao. Kwa hivyo nilikuwa naomba sana Mhe. Spika, Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria hawa majaji wa mahkama za mwanzo wajaribu kuangalia kama kuna mapungufu yaliyobakia basi waweze kurekebishiwa ili waweze kututolea haki vizuri.

Mhe. Spika, lakini kuna jengine hili la ma-*assessor*, ma- *assessor* wale tunawashukuru tulipowasemea hatua ya mwanzo walipunguziwa kidogo malipo yao, lakini sasa kuna tatizo lilitokezea walilipwa malipo ya mbele yakaachwa yale ya nyuma. Sasa hii ilikuwa inaonesha kwamba labda yale ya nyuma pengine yatakuwa yamesahauliwa kabisa. Kwa hivyo kilio chao hiki ninakileta hapa Mhe. Spika, ili Mhe. Waziri ajue kwamba wale ma-*assessor* bado wanadai zile posho zao ambazo ndio hao ambao wanaweza kusaidia kuendesha hizo kesi pale mahkamani.

Mhe. Spika, lakini vile vile kitu chengine nilichotaka kukisema hasa hawa watu waliopewa dhamana, Mhe. Spika, wakati mwengine zile dhamana watu wanazopewa inakuwa kama mtu kumpa njia ya kukimbia. Sasa mimi naomba sana mtu yeyote ambaye amepewa dhamana akikimbia sasa siku yoyote ambayo anaingia nchini au yule mdhamini wake basi aweze kuwajibika kisheria. Kwa hivyo naomba sana Mheshimiwa kwa upande wetu mahakimu hili wajaribu kulifanyia kazi vizuri, kwa sababu haya tunayoyazungumza ndio kuboresha ili watekeleze zile sheria ambazo tulizozitunga hapa Barazani.

Mhe. Spika, lakini vile vile kama kuna makosa ambayo yanafanyika kama Mwenyekiti wa Kamati alivyoshauri kwenye ripoti, basi ile Tume ya Utumishi ya Mahkama ipo iweze kutenda hiyo haki kwa kuweza kuwajibisha na kuchukua hatua za kinidhamu kwa hakimu yeyote ambaye amekwenda kinyume cha sheria. Lakini baya zaidi Mhe. Spika, hili naendelea tena kulisema, kuna baadhi hasa ya uwekezaji kama alivyozungumza mwenzangu Mhe. Makame Mshimba hata na mimi ninawafiki lile wazo lake, kwamba kuwe na mahkama ingawa tutasema kwamba jamani sasa hivi itakuwa kila sehemu itakuwa ina mahkama zake. Lakini tunaangalia uzito Mheshimiwa, kesi za wawekezaji kesi hizi hazitakiwi zisikilizwe katika utaratibu wa kawaida.

Kwa sababu Mheshimiwa sasa hivi utakuta wakati mwengine unakuta muwekezaji sitaki kumtaja jina kwa sababu nimeshasema sana Mhe. Makamu wa pili wa Rais ameshatoa agizo lishughulikiwe, unamkuta kuna muwekezaji anamuumiza muwekezaji mwengine tena wa kizalendo, halafu yeye moja kwa moja kwa kuwa ana uwezo wake anakwenda mahkamani, anaweka *court injunction* halafu hiyo *court injuction* Mhe. Spika, yaani hakuna siku unaweza ukaikuta *court injuction* inakaa miaka 3, 4, 5 hakuna kesi inayokwenda.

Pengine inaitwa kesi mahkamani yule kwa kuwa ana pesa zake anajua kama sikwenda kesi itaahirishwa wanakuwa wanafanya ubabaishaji kama huo. Lakini je katika ule muda ambao imewekwa ile *court injuction* huyu mwengine ambaye aliyezuiliwa eneo lake asilitumie ataathirika kwa kiasi gani. Sasa hili nilikuwa naomba sana Mhe. Spika, mahakimu wetu hawa

wajaribu sana kuangalia hasa hawa wawekezaji. Leo utakuta kuna wananchi wamechukuliwa maeneo yao watu wanakwenda mahkamani, mwananchi anashindwa kulitumia eneo lake, wale wenye mapesa yao wanaendelea kufanya shughuli zao wananchi kwa kweli wanaathirika mpaka kisaikolojia. Sasa hili nilikuwa naomba sana hasa hizi *court injuction* basi ziwe na muda wake kama ile kesi kama yule anaitwa haendi basi kesi iweze kusemwa yafanywe maamuzi. Kwa sababu masuala haya ya uwekezaji Mheshimiwa kila muda unapokwenda kwa kweli athari kubwa za kiuchumi zinakuwa zinajitokeza.

Jengine Mhe. Spika, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na mimi nilikuwa najaribu kukazia kwamba *scheme of service*, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa kweli izingatiwe kwa sababu ni kweli hali ya maslahi yao kwa kweli hayako vizuri ukiangalia na kada nyengine ambao na wenzao wenye taaluma kama ile yao ya kisheria inakuwa iko sawasawa lakini maslahi yao kwa kweli yanakuwa tofauti. Kama alivyosema Mhe, Mwenyekiti katika ripoti hii kwamba karibu watumishi wanne tayari wameshakimbia na hawa ni wataalamu wa kisheria ambao kwa kweli tunahitaji watulie pale ili waweze kujijenga kiuzoefu.

Kwa sababu Mhe. Spika, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka pale ndio kesi zote, sasa kesi tumewanyang'anya Polisi kusimamia kesi mahkamani, sasa hivi Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ndio inayosimamia kesi zote pale. Kwa hivyo kama maslahi yao yanakuwa mepesi yanayumba yumba hata hizi kesi zetu Mhe. Spika, zitakuwa haziendi vizuri. Kwa hivyo nilikuwa naomba sana Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kuangalia zaidi suala la kuboresha maslahi ambayo ile *scheme of service* ikiweza kufanyiwa vizuri naamini mambo haya yataweza kukaa sawa.

Mhe. Spika, ukurasa wa 6 -7 Mhe. Mwenyekiti katika ripoti yake ameeleza Tume ya Kurekebisha sheria na hapa mimi kuna jambo moja ambalo Mhe. Mwenyekiti amelieleza na mimi nilikuwa nataka kulikazia.

Mhe. Spika, sasa hivi Zanzibar hasa kutokana na ukuaji wa teknolojia na hivi vyombo vya kisasa hasa vya kurekodia Mhe. Spika, kwa kweli sasa hivi aibu sasa hivi imekuwa si aibu tena, aibu zimekuwa zikianikwa mitaani. Mhe. Spika, lakini kitu kinachonishangaza karibuni kuliwahi kurushwa picha kwenye *whatsapp* kwa wale wenye simu ambazo zina *whatsapp* kuna baadhi yao ninafikiri walirushiwa. Watu wanafanya mambo yao wanakubaliana wao wenyewe mmoja anakuwa anamrikodi mwenzake halafu anamkashifu.

Mhe. Spika, kwa kweli mimi sio sheikh lakini niliwahi kupata kusikia hadithi moja kwa sheikh mmoja anasema kama ulifanya kashfa yoyote ikawa ile

kashfa ulibakia nayo wewe mwenyewe tu, basi hata ile hukumu yako inakuwa nyepesi. Lakini ukifanya kashfa halafu ile kashfa ukaenda ukaianika basi adhabu kali inakuwa inakushukia, sasa Mhe. Spika, leo vitendo kama hivi vilivyofanyika, na kwa sababu ilianzwa ya yule mwanafunzi akarikodiwa akafanywa vitendo vibaya ikarushwa hakuna hatua iliyochukuliwa. Na hivi karibuni kuna kijana mwengine tena wanatafutwa wale watu mashuhuri wale akafanyiwa vitendo vibaya ikarushwa hakuna hatua zilizochukuliwa.

Sasa mimi nilikuwa nadhani Mheshimiwa sasa hivi kama tuna mapungufu ya sheria katika kudhibiti hii mitandao mimi nadhani sasa hivi wakati umefika, kwa sababu mambo haya Mhe. Spika, leo tusione yanawatokezea wenzetu kesho yanakuja kutukuta sisi, na sisi tunatakiwa tukitunga sheria hapa tusiangalie maslahi binafsi. Kwa hivyo mwananchi yeyote aliyefanyiwa kitendo kibaya hili jambo linakuwa la serikali, kwa sababu yule ni mwananchi, yule ni raia wa nchi. Sasa leo Mhe. Spika, katika hizi kashfa ambazo zinarushwa kwenye simu hebu tuambiwe kuna kesi gani iliyofunguliwa mahkamani. Kama kuna kesi iliyofunguliwa mahkamani tutanyamaza kimya ili tuiachie mahkama ifanye shughuli zake, lakini kwa kweli kutokana na vitendo vinavyofanywa sasa hivi kwa kweli Mhe. Spika, ni hatari kubwa sana kwa nchi yetu.

Mhe. Spika, hizi dakika zangu tano nitatafuta lile eneo ambalo Mwenyekiti alilizungumza kwa muda mrefu. Mhe. Mwenyekiti nilipoangalia ukurasa wa 14 hapa, Mhe. Mwenyekiti alizungumzia kadhia ya Idara ya Nyaraka na upotevu wa nyaraka za serikali.

Mhe. Spika, Mhe. Mwenyekiti wa Kamati hapa alishauri kwamba kuundwe Tume ichunguze na ituletee ripoti lakini Mhe. Mwenyekiti kwa kuwa hii ripoti imekuja hapa Barazani, hii ripoti ni mali yetu kama Baraza. Mimi nilikuwa naomba Mhe. Spika, tutumie kanuni yetu ya Baraza hii hapa kifungu cha 117 Baraza lako ndio liunde hii Tume. Kwa sababu Mhe. Spika, hii kadhia imefanywa na watendaji wa Wizara, tukisema tuiachie serikali ikachunguze kadhia ile tuna tabia ya kufumbiana macho. Mimi nadhani chombo chako hiki kwa kutumia kanuni hii ya 117 nimeisoma hapa basi Baraza lako tukufu Mhe. Spika, tuunde Kamati Teule tukachunguze kadhia ile na tukachunguze kwa sababu gani. Mhe. Spika, sisi sio kwamba tunachunguza tu ubadhirifu au upotevu wa fedha au matumizi mabaya ya fedha za umma, lakini Mhe. Spika, nyaraka hizi watu wanatajirika kwa kuuza nyaraka za serikali.

Mhe. Spika, hili ukiliangalia kwa kawaida ukisikia nyaraka ya serikali utaona ni kitu chepesi, lakini watu wanaojua umuhimu wa nyaraka za siri za serikali, Mhe. Spika, watu wako tayari kutoa mabilioni ya mashilingi ili kuweza

kupata nyaraka hizi. Sasa leo nyaraka hizi Mhe. Spika, kama kamati imekwenda taarifa hazijulikani.

Sasa mimi naomba Mhe. Spika, kutumia kanuni hii ili tupewe kazi tukaifanye hiyo kazi na hili Mhe. Spika, nataka nilirejee vile vile na lile agizo lako Mhe. Spika. Kwenye Baraza lako lililopita hapa tulitaka kuunda kamati teule kuzungumzia ufuatiliaji wa mradi wa E-*Government* jinsi ya matumizi ya fedha na manunuzi yake vile vile Mhe. Spika, ukatumia busara zako ukaagiza kamati husika iende ikafanye kazi. Mhe. Mwenyekiti ameshaturipotia hapa, kamati imekwenda hakuna kitu ilichopata ni dharau. Mheshimiwa agizo unalolitoa wewe likidharauliwa limedharauliwa Baraza, sisi hatuwezi tukaruhusu Kiti chako kudharauliwa.

Mhe. Spika, kwa hivyo katika hiyo kanuni niliyoitaja na hili litaingia, kwa hivyo utoe kazi kwa kazi mbili, kazi ya Idara ya Nyaraka na mimi naomba Mhe. Spika, tatizo letu sisi tunapounda Kamati Teule mtu anapokwenda kuchuguzwa yeye mwenyewe anabakia ofisini. Kwa hivyo ina maana kama kuna jambo jengine anapata kulirekebisha. Kwa hivyo naomba hapa wahusika aidha Mkurugenzi au mwengine yeyote akae pembeni kwanza tukafanye uchunguzi tulete ripoti. Mhe. Spika, tunataka Baraza lako tukufu liweze kufanya kazi ya wananchi kama tulivyotumwa na wananchi.

Mheshimiwa leo kuna *People's Palace*, kule kuna vile vifaa vya zamani sijui kuna upanga wa mfalme, sijui kuna nini na nini vimeibiwa, rungu la polisi limeibiwa, nyaraka za serikali zimeshaibiwa. Mheshimiwa tutakuja kuibiwa mpaka sisi hapa, leo tumekaa hapa tunasema hapa hakuna hatua iliyochukuliwa. Kwa hivyo Mhe. Spika, naomba sana suala hili kwa kweli tuweze kulifanyia kazi kwa sababu nyaraka za serikali Mheshimiwa ndio siri za serikali. Leo kuna watu nilikuwa ninasikia hapa kulikuwa kuna nchi moja kulikuwa kuna nyaraka wanazitafuta inawezekana walipoona zina ugumu wa kupatikana wakawa-*lobby* watu wetu wakaweza kuzipata, sasa hii tunataka tukalifanyie kazi.

Mhe. Spika, hata ukaona tunakazia tukalifanyie kazi, tayari kuna harufu tushainusa, tupe kazi tukafanye tukuletee ripoti. Mhe. Spika, na naamini ripoti hiyo serikali itakaa itaifanyia kazi tutaweza kufanya mambo mazuri.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache ninaunga mkono ripoti ya kamati lakini vile vile naamini na wenzangu wataunga mkono ushauri nilioutoa katika kuchangia ripoti hii ya kamati. Mhe. Spika, ninakushukuru.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, naomba nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu subhnahu wataala kwa kutujaalia kuwa hai na wazima na

tukaendelea na shughuli zetu hapa, lakini pili Mhe. Spika, nikushukuru na wewe kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia.

Mhe. Spika, ingelikuwa si kwamba leo umesimamia barabara kanuni ya muda nilikuwa nikuombe utumie kanuni ya 58 (6) zile dakika kumi leo uniongeze kutokana na uzito wa yale ninayotaka kuyazungumza lakini nitaheshimu maelekezo ya Kiti chako.

Mhe. Spika, kwanza naomba ninapochangia ripoti hii niungane na Mhe. Hamza kumpongeza na kumsifu sana Mheshimiwa kijana Mwakilishi wa Jimbo la Chaani Mhe. Ussi Jecha Simai. Nilikuwa ninamnong'oneza Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum kwamba tunaona vipaji vikiibuka katika Baraza, ninampongeza sana lakini namuomba isije ikageuka hadithi ya *mgema akisifiwa tembo hulitia maji*. Ule ujasiri wake wa kusimamia alichokiamini auendeleze kwa yeyote na kwa chochote ambacho anakiamini.

Mhe. Spika, mimi nataka niseme jambo moja kwanza la jumla nalo Mhe. Spika, ninasikitika sana kwamba bado serikali haionekani kulipa uzito Baraza hili na kazi zake. Mhe. Spika, hapa leo tunapokea ripoti ya Kamati, na Kamati hii kama ilivyo kamati nyengine ina Wizara tatu, tungetegemea leo Mhe. Spika, pale juu pajae, wapo, si kama hawapo, baadhi lakini uongozi wa Wizara 3 Mhe. Spika, na mamlaka zinazosimamia ingekuwa zote zimewakilishwa pangelijaa, pangelikuwa hapana nafasi pale. Lakini tunasema mara nyingi hili kosa letu sisi wenyewe Wawakilishi hatujaamua hasa kuionesha serikali kwamba chombo chenye mamlaka ya wananchi ni chombo hiki, siku tukiamua Mhe. Spika, tutaheshimiwa.

Mhe. Spika, wakati wa bajeti hahimizwi mtu kuja juu kule, wanapokuwa na mswada muhimu hakuhimizwi mtu lakini chombo hiki sasa kinafanya kazi ile ya kuisimamia serikali, maana kikao ambacho kinapokea ripoti za kamati ndipo tunapofanya kazi hasa ya kuisimamia serikali tunaona hali halisi ilivyo. Ni kweli mawaziri wanawakilisha serikali lakini uzuri tunaona katika mabunge mengi Mhe. Spika, zile Idara, Mamlaka, vyombo mbali mbali vinapochambuliwa basi wenyewe pia wawepo wasikilize kutoka kwa Wawakilishi wenyewe, yaani siku moja tu Mhe. Spika, kwa vikao kama hivi. Kwa hivyo hilo moja mimi linanisikitisha sana.

Lakini la pili Mhe. Spika, ambayo niseme chombo hiki bado hakiheshimiwi ni yale maagizo tunayoyatoa Mhe. Spika. Ukizitizama ripoti na ninazo baadhi hapa za miaka iliyopita, maagizo ambayo kamati imekuwa tukitoa yanajirejea yayo kwa yayo. Sasa Mhe. Spika, mwaka wa kwanza sawa, mwaka wa pili sawa, leo tunaingia mwaka wa 4 tangu serikali hii imeingia madarakani, ikiwa

maagizo mengine tena ni ya kawaida tu yanajirejea yale kwa yale maana yake hayatekelezwi. Mimi siamini kama Wawakilishi sisi humu kwamba labda tunataka kumuandama mtu fulani au tumeshindwa kufanya kazi tunarejea yale kwa yale mimi siamini. Ninaamini yale yaliyoripotiwa yameonekana na Kamati. Na uthibitisho ule Mhe. Spika, mimi nilikuwa Mjumbe wa kamati ya Katiba, Sheria na Utawala katika kipindi kilichopita, sasa kuna kamati mpya ikiwa wanayaona yale yale maana yake ni kwamba hayajatekelezwa.

Kwa hivyo Mhe. Spika, nasema mara nyengine tukisema haya, leo asubuhi pamejitokeza hoja hapa Mjumbe mmoja kasema serikali inatoa ahadi hewa, rafiki yangu Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ akasema serikali haitoi ahadi hewa. Lakini haya ambayo yamo humu ndani ya ripoti Mhe. Spika, mengi yashatolewa ahadi na serikali katika miaka mitatu iliyopita, kwa nini yanaendelea kujirejea, kwamba yatachukuliwa hatua kuwa yatamalizwa. Bado Mhe. Spika, nasema tuna tatizo kubwa sana katika hili.

Mhe. Spika, jengine nimuombe Mhe. Rais, kuna haja tena ya kutizama utendaji wa serikali. Mimi namsifu sana Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, lakini siamini kama tutakuwa na ufanisi hata tukawa na uwezo kiasi gani, kwamba waziri mmoja anakaimu wizara tatu na yake yeye mwenyewe ya nne.

Mhe. Spika, katika kikao hiki Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kakaimu Wizara ya Kilimo na Maliasili, kakaimu Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, tangu jana kakaimu Wizara ya Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma na yake yeye ya nne. Hivi Mhe. Spika, tuna uwezo wa *super man* au *spider man?* Nadhani hili tunapaswa kulitazama sana. Sasa nasema naliunganisha hilo Mhe. Spika, kwa sababu pale yanapotolewa maagizo ya utekelezaji halafu tukarejea yakawa vile vile hairidhishi.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi sasa niende katika maudhui ya ripoti. La kwanza nataka kulizungumzia hili linalohusu wizi wa nyaraka. Mhe. Spika, katika watu wanaothamini historia na nyaraka na mimi mmoja wapo, katika hilo najisifia sana, naweza kutunza nyaraka kuliko hata ninavyotunza pesa hasa ikiwa nyaraka ya kihistoria, ina thamani Mhe. Spika, pengine kuliko hata hicho kiwango cha pesa unachokifikiria labda kina thamani. Vitu vya kihistoria Mhe. Spika, tukitaka kujua uzito wake tuangalie katika nchi za wenzetu, panaponadiwa vitu vya kihistoria wanavyojua thamani yake, tutizame wanavyotia thamani ya vitu vile wakavinunua kwa mamilioni ya pesa.

Mhe. Spika, kwa miaka nenda miaka rudi na katika hili mimi sioni aibu kuwasifu Waingereza walipokuwa wakitawala hapa. Walipojua thamani wakatuanzishia chombo kile jumba la Nyaraka na ni miaka nenda miaka rudi, kwa dahari na miaka Jumba la Nyaraka la Zanzibar lilikuwa ndio jumba bora kwa wingi na ubora wa nyaraka katika eneo lote la Afrika Mashariki na Kati. Siajabu kwa sababu Zanzibar ndipo pahala palipoanzia mambo mengi kuingia katika Baraza la Afrika.

Leo Mhe. Spika, taarifa nilizozipata pembeni pembeni kwamba, kuna ma-*box* sita, ingawa wanaofuatilia wanasema wanaamini hayo labda ndio yaliyogundulika, inawezekana yako ma-*box* mengi matupu ndani yamebakia mafaili, yote yamepotea.

Mhe. Spika, taarifa nilizonazo mimi zitathibitishwa tukija tukifanya hiyo kazi ambayo Mhe. Mwenyekiti wa Kamati kaisema. Ni kwamba katika nyaraka zilizoibiwa ni ile miswada iliyoandikwa kwa mikono, ya maandishi ya kihistoria mengine yaliyoandikwa kwa lugha ya Kiarabu.

Juzi Mhe. Spika, kuonesha uwezo wa chombo kile tukivutana hapa kuhusu Kisiwa cha Fungu Mbaraka, nani hakuthibitisha siku Mwanasheria Mkuu alipokuja kututolea maelezo hapa kwamba ushahidi wote tuliyoupata umetokana na hazina iliyoko katika jumba la nyaraka lile. Leo Mheshimiwa tuliowapa dhamana ya kutulindia wanasimamia wizi katika chombo kile. Mimi nasema hivyo Mhe. Spika, na kwa nini mtu asiwajibike ikiwa kashindwa kusimamia kazi tuliyompa, vitu vinapotea katika dhamana yake!
Mhe. Spika, tulipokuwa sisi Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala sijui wenzangu watanambia kama tulitembelea pale, kuna sehemu tumeambiwa ni *lockup* hata sisi hatukuruhusiwa kutizama kama wawakilishi, leo vipi mtu tu, afike apate nyaraka hizo zipotee katika mazingira ya kutatanisha.

Mhe. Spika, katika hili mimi hata nikisimama kuunga mkono hoja ya kamati teule mara nyingi huwa nishatafakari sana na ningetegemea katika hali ya kawaida nisingelisema tuiachie kamati ya sekta. Lakini kamati yenyewe ya sekta inasemaje, kwa hili iundwe kamati teule ikachunguze. Sasa mimi naliunga mkono kwanza pendekezo hili, lakini hapa pana kazi ya kitaalamu Mhe. Spika, kwa sababu kuzitambua nyaraka panataka mtu ambaye ni mtaalamu wa fani hii.

Karibuni nilipata bahati ya kuzungumza na mmoja kati ya vigogo wa masuala ya historia katika nchi yetu. Anasema kwa bahati wako watafiti waliwahi kupita pale ambao walibahatika kuandaa *index* au faharisi ya baadhi ya nyaraka, inaweza kuwa ni chanzo kizuri cha kujua. Lakini ninavyofahamu

mimi *unless* kama na hilo pia limeibiwa, pale kila kilichopo kina faharisi yake au muongozo unaoonesha katika kila faili kuna kitu gani hivi sasa.

Sasa Mhe. Spika, kuna haja ya kwenda kutizama pengine kama itaundwa kamati teule basi kwa kusaidiwa na wataalamu wa fani ile wakiwa ni sehemu yake kwenda kutizama na kupitia *box* baada ya *box*, nyaraka zote kujua ni nyaraka ngapi zimeibiwa maana mimi sisemi kama zimepotea.

Mhe. Hamza Hassan Juma kasema hapa, kama sikuchelea kuitia matatani serikali yetu mimi ningetaja mpaka jina hapa, lakini kwa kuepusha kuingia katika migogoro ya kidiplomasia anasema kuna nchi moja inatajwa sana kuwa mara nyingi imekuwa ikitafuta kila aina ya njia ili kupata nyaraka ambazo ziko katika nchi hii. Sasa tunaanza kupata wasiwasi kwamba usiwe uwezo wa kifedha unatumika kuwarubuni watumishi kuzifichua nyaraka hizi zikawa zinapotea.

Mhe. Spika, naomba katika hili, nitachukua muda mrefu kidogo kulizungumzia kwa sababu ni suala ambalo thamani yake kubwa sana. Siku Zanzibar ikipoteza ule upekee wa kuwa na udhibiti wa nyaraka hizi basi ile thamani yake katika ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kati umekwisha, umepotea. Sasa Mhe. Spika, tumegundua kuna baadhi ya vifaa ambavyo vilichukuliwa na Wakoloni katika nchi walizokuwa wakizitawala, tena walivichukua wakiwa na mamlaka wakati huo, wamevihamishia katika majumba yao ya makumbusho.

Leo nchi zilizokuwa zimetawaliwa zimedai na zimerejeshewa vitu vile, ziko taarifa katika nchi hiyo kwamba baadhi ya vifaa vya Zanzibar unavikuta huko, nasema tusichelewe katika hili Mhe. Spika, isiwe kwa sababu ya umasikini wetu ikapelekea kupoteza vilivyokuwa vyetu. Tufuatilie kwa sababu kama viko huko tudai virejeshwe katika milki ya Zanzibar, hii ni mali, ni urithi wa kitaifa wa Wazanzibari.

Mhe. Spika, kwa sababu ya muda naona hayo mengine niyaache, naomba hilo niishie hapo na nasema niungane mkono na Mhe. Mwenyekiti, kutaka maelezo ya kina kutoka serikalini juu ya suala hili. Serikali imechukua hatua gani baada ya kutokea hili au ndio kama kawaida yetu basi yataendelea kufanyika mengi na mengine kwa sababu hatujali.

Mhe. Spika, la pili katika Wizara hii ya Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma ni suala ambalo limeripotiwa hapa la Mradi wa *E-Government*. Mhe. Spika, sisi wengine akina Ismail Jussa tunaonekana wakorofi sana katika chombo hiki, kwa sababu tuna hoji mambo yanayohusu matumizi mabaya ya fedha za Wazanzibari ambao wanakwenda hospitali hawana dawa. Ikifika

mwanzo wa mwaka kama huu kila mmoja kiguu na njia anatafutia watoto wake mabuku, kwenda kulipia michango, lakini huku fedha zinatafunwa. Tulizungumza humu ndani kuhusu mradi wa *E-Government*.

Mhe. Spika, mara nyengine wengine wanasema busara zako, sisi mara nyengine tunakulaumu, kama kile kipindi cha bajeti kilichopita katika baadhi ya mambo namna tulivyoyapitisha humu ndani. Lakini sawa tumepitisha bajeti, hili umeliagiza liende katika kamati, Mhe. Spika, hili mimi nikiwa Mjumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala mwenyekiti wangu akiwa Mhe. Ali Abdalla Ali, Naibu Spika, wajumbe wengine wamo tulilidai tukiwa kamati ya sekta kupewa hesabu za *E-Government* hatukupewa.

Huko Wizara ya Fedha tuliandika sisi tukiwa Kamati ya Sekta kuomba mchanganuo wa matumizi hatukupewa, na kama mnakumbuka nilisoma ndani ya Baraza hili barua tuliyoandika mwaka mzima umepita haikujibiwa na hapa serikali ikashindwa kutoa majibu. Sasa umeagiza tena kamati ile ile Mhe. Spika, iende na kamati inakuja kujibu tena leo kwamba haikupewa na hakuna majibu mpaka kiama Mhe. Spika katika hili. Kwa sababu kuna matatizo, kwa nini kama kuna kitu safi kiwe kinafichwa, kinafichwa nini.

Kwa hivyo Mhe. Spika, nadhani sasa utaridhika na sisi kwamba imefika haja ya kuunda kamati teule kwa sababu kama kamati za kisekta zinashindwa tutafanya kazi gani nyengine ya kwenda kuuchunguza mradi huu, kunafichwa nini. Kuna watu wamepata nini katika hili hata ikawa wanaogopa kisijulikane na wananchi wa Zanzibar masikini hawa. Naliacha hilo Mhe. Spika.
Sasa naomba niende katika Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ. Mhe. Spika, jana Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni Mhe. Salmin Awadh alizungumzaia kadhia iliyotekea katika jimbo lake kuhusiana na vitendo vya polisi. Mimi nimesema mara nyingi humu ndani kwamba vikosi vya SMZ ni fahari ya wananchi wa Zanzibar, hilo linathibitika hata katika gwaride likipita pale. Wazanzibari utaona wanafurahi vikipita vikosi vyao. Na vilikuwa vikilalamikiwa sana lakini kumefanyika marekebisho makubwa tunashukuru.

Mhe. Spika, fahari ya wananchi kwa vikosi vyao inakuja wanapotekeleza kazi zao kwa mujibu wa maadili ya kazi zile, Tunawatetea sana humu ndani maslahi yao, lakini ile sifa nzuri ambayo ilipatikana Mhe. Spika, ilichafuka kidogo katika wiki za Sherehe za Mapinduzi.

Mimi niliripotiwa mwanzo nikasema aah, labda maneno ya mitaani tu, kwamba kuna baadhi ya maeneo askari wa vikosi walikuwa wanapita na kupiga wananchi. Nilitajiwa kadhia moja ya Jang'ombe, nikatajiwa kadhia mara mbili mitaa ya Kundemba. Lakini baadae Mhe. Spika, zile siku za

mwisho mwenyewe kwa macho yangu nikashuhudia. Siku moja usiku narudi nyumbani nimo ndani ya gari eneo la Darajani Marikiti, kuna kijana kalazwa chini anapigwa. Kadhia nyengine nikaja nikaikutia Forodhani, hakuna tatizo lolote, kijana kakaa alikuwa anatumia *laptop* yake kaegemea katika lile jumba la watoto yatima pale, hata hujui kumeanza nini anashitukizia kavamiwa na anapigwa tu. Sasa Mhe. Spika, nasema inawezekana ni wachache hawa lakini wanaharibu taswira ya vikosi hivi.

Mhe. Spika, nchi yetu inategemea utalii, mambo kama yale yanapofanyika katika maeneo mpaka wanayopita watalii wakiona hatupeleki ujumbe mzuri. Nimuombe sana Mhe. Waziri kama kuna maelekezo wanapewa wafanye basi anayewapa maelekezo haya hawapendelei mema aache, kama ni utashi wao waelekezwe Mhe. Spika. Nadhani tumefanya jitihada kubwa sana na yeye Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, bahati nzuri alikuwa mjumbe wa Kamati ya Baraza la Wawakilishi chini ya Mhe. Ali Mzee Ali iliyosimamia kuleta Serikali ya Umoja wa Kitaifa na kuleta maridhiano, basi tuoneshe mfano tusije tukarudi kule ambako tumetoka.

Jengine natetea tena maslahi yao, kazungumza Mhe. Mwenyekiti katika ripoti yake, yale yale tunarejea kama nilivyosema. Mhe. Spika, vikosi vinafanya kazi kubwa sana vyovyote vile, wakati sisi tunalala wao wanafanya kazi ya kutulinda. Kwa hivyo, nilikuwa nadhani kumekuwa na malalamiko mengi juu ya haki zao, maslahi yao, mishahara yao kutizamwa upya, fedha zao za likizo, maeneo wanayofanyia kazi, mazingira ya nyumba wanazoishi na sikitaji kikosi kimoja kimoja, takriban vikosi vyote bado kuna matatizo. Mikato ile nategemea chini ya uongozi wa waziri mpya basi atayasimamia.

Mhe. Spika, bahati nzuri Mhe. Waziri alitembelea na najua yeye kasema mengi huko lakini pia na yeye kaelezwa mengi. Basi yale ambayo kayapata ili kutunyima sisi fursa ya kusimama hapa tukayasemea basi yatekelezwe. Mhe. Spika, naomba sana hilo.

Mhe. Spika, mwisho kabisa nimalizie katika Wizara ya Katiba na Sheria kwa ufupi sana. Nilikuwa nina mambo kadhaa nataka kuyazungumza lakini kwa sababu ya muda naomba niseme moja tu, nalo ni lile ambalo linahusu katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano. Nalisema leo zaidi Mhe. Spika, kwa sababu waziri wa sekta hii ni Waziri wa Katiba na Sheria.

Mhe. Spika, naendelea kusisitiza kwamba wananchi wameshatoa maoni yao. Kwa hivyo suala la serikali kuchelea kwamba kujua nini matakwa ya Wazanzibari katika hatua hii ya mwisho haitakuwa kuingilia maoni ya wananchi, mana wananchi washamaliza kutoa maoni yao. Na kwa mujibu wa

Jaji Joseph Sinde Warioba kasema wazi siku alipokuwa akiwasilisha ripoti yake, kwamba kwa upande wa Zanzibar asilimia 60 waliotoa maoni walitaka Muungano wa Mkataba na kwa upande wa Tanganyika asilimia 61 walitaka serikali tatu, wao wenyewe wakaona njia ya kati ya kupita ni kuja na mapendekezo waliyokujanayo.

Lakini zaidi akasema kwa upande wa Zanzibar hata hao waliotetea mfumo wa serikali mbili walitaka mabadiliko makubwa ambayo yasingewezekana katika mfumo ule na zaidi walikuwa wakizungumzia kurejeshwa kwa mamlaka ya Zanzibar. Haya alizungumza Jaji Warioba na tulimsikia sote. Sasa nasema hatua zote tumeshapita Mhe. Spika.

Sasa tunakwenda katika Bunge Maalum la Katiba, hivi pamoja na tofauti zetu kuhusu aina za miundo, lakini yale ya msingi ambayo Wazanzibari tulikuwa tukiyataka na katika chombo hiki tumesimamia mara kadhaa kuyadai kwa umoja wetu, hivi tunakwenda katika Bunge la Katiba bila ya kuwa na muongozo? Nimuombe sana Waziri wa Katiba na Sheria katika hili atusaidie na yeye aliwahi kusimama katika kiriri kile pale tulipomhoji, akasema serikali itaheshimu maoni ya wananchi ambayo ndio haya aliyozungumza Jaji Warioba. Kwa hivyo, nilikuwa naomba Mhe. Spika, tujue tunakwendaje katika Bunge la Katiba.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, nikushukuru sana kwa kupata fursa hii na nasema kwa ripoti hii na uwasilishaji wake naiunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kutoa mchango katika ripoti hii ambayo kusema kweli ni ripoti ndefu na imekusanya mawaziri watatu. Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ na Wizara ya Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma.

Kwa kweli Mhe. Spika, hii ripoti ni ndefu sana na hatuwezi kumaliza habari zote zilizomo humu. Lakini tutajitahidi kadiri ya uwezo wetu kuweza kufanikisha japokuwa kidogo.

Kwanza Mhe. Spika, nataka nianze katika Mahakama ya Mwanakwerekwe. Mheshimiwa, liliopo hapa katika mahakama hii ni mambo yanayojitokeza katika chumba cha Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Chumba hiki hakistahiki kwa binadamu kuweza kuishi ndani na kuweza kufanya kazi. Chumba ni kidogo ambacho hakiridhishi na hakiko katika hadhi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Kwa hivyo, ningependa Mhe. Waziri katika suala

hili aweze kulifuatilia na alione yeye mwenyewe kwa macho yake jinsi watu hawa wanavyoishi katika utendaji wa kazi zao.
Vile vile Mhe. Spika, katika Mahakama hii ya Mwanakwerekwe sehemu ya kuwekea vitu vya ushahidi ndani ya ofisi ile ni finyu sana na vinaweza kurundikana kwa wingi, mwisho panya pia wanakuwemo mle pamoja na uchafu jambo ambalo si zuri na haliridhishi. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri ende akaone kwa macho yake halafu aweze kutatua matatizo yaliyomo katika sehemu ile.

Mhe. Spika, baada ya hilo nataka niendelee katika jengo la Wizara ya Katiba na Sheria. Mhe. Spika, jengo hili ni jipya, limeanzishwa hivi karibuni ambalo ni la ghorofa nane, likiwa na ofisi yake moja chini ya ardhi. Jengo hili limeanzishwa rasmi mwezi wa April, 2012; jengo linajengwa na Kampuni ya *CHINA RAILWAY JIANCHANG ENGINEERING CO (T) LTD (CRJE)*.

Mhe. Spika, mnamo mwezi Novemba, 2013 kampuni imeomba kuongeza muda wa ujenzi. Kwa kweli sababu Mhe. Spika, zilizosababisha kuongezwa muda ni kutokana na ucheleweshwaji wa fedha, yaani malipo hayakupatikana kwa wakati. Kwa hivyo kazi ilibidi kuzorota na wao kazi kuziakhirisha na ikabidi kutafuta kazi nyengine badala yake.

Lakini hata hivyo, jengo limefikia hatua nzuri na kazi zinaendelea lakini pole pole. Sasa Mhe. Spika, nimuulize Mhe. Waziri ni lini fedha hiyo itapatikana ili liweze kukamilishwa jengo hilo kwa haraka.

Jengine Mhe. Spika, katika hili kwa sababu ya ongezeko la muda maana ukiongeza muda kuna matatizo yake. Haoni Mhe. Waziri kwamba gharama za ziada ambazo hazikuwemo katika kipindi cha bajeti zitaongezeka. Hawa wame-*extend period*. Mhe. Waziri atatwambia nini katika suala hili.

Mhe. Spika, baada ya hilo nataka kuzungumzia juu ya Mahakama zote kwa jumla. Mahakama nyingi kwa kweli zina hali mbaya; hali mbaya kiasi ambacho majengo yake ni machakavu na hayaridhishi. Pia ndani ya majengo haya kuna ufinyu mkubwa wa nafasi, na ukiangalia kutokana na nafasi hizo hata yale majukumu ambayo wao wanapangiwa kuyatekeleza mle ndani yanawashinda. Mhe. Waziri, ningemuomba atwambie ni lini majengo haya yatafikiriwa kuwekwa katika hali nzuri?

Mhe. Spika, sasa nataka kuzungumzia juu ya Mahakama Kuu ya Vuga. Katika mahakama hii kusema kweli ina shughuli nzito sana. Mahakama hii ofisi zake ni ndogo ukilinganisha na mahitaji yake. Wakati mahakama zinaendesha shughuli zake basi mahakama nyengine hubidi kuondoka na kuwapisha Mahakama ya Rufaa. Sasa utakuta mahakama ile inataka

kuendesha shughuli zake na hii inataka kuendesha inabidi ziwe kama gari za daladala kule mjini, ile inaingia ile inatoka. Hili linakuwa ni tatizo kubwa sana na humo humo utakuta mna Mahakama ya Watoto ndani ya jengo hilo. Kwa kweli hairidhishi kiutendaji na baya zaidi, wakati mwengine hubidi watendaji wengine kuondoka na kuchukua likizo kwa ufinyu wa nafasi.

Mhe. Spika, baada ya hilo nataka nizungumzie Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka upande wa bajeti. Ofisi hii Mhe. Spika, nayo imekabiliwa na ufinyu wa bajeti. Mimi niseme dhahiri kwamba ofisi hii bajeti wanayopata ni ndogo sana kiasi ambacho hushindwa kutekeleza majukumu yao au malengo waliyojipangia. Ukizungumzia wale mawakili wa ofisi hii ndio utaona ile hali ngumu ya ofisi hii na watendaji.

Watendaji hawa wana majukumu makubwa sana katika utendaji wao wa kazi. Kesi za jinai huwa ni nyingi katika kuzifuatilia, kuziandaa, kuzisimamia, jambo ambalo linachukua muda mrefu hata ule muda wa mapumziko hawana. Kilio chao kikubwa wanalia maslahi yao ni madogo kabisa. Hayafanani na viwango vyao vya kielimu na kiuzoefu. Jambo ambalo si zuri, ikiwa wizara hii watu wa aina moja, wenye shughuli nzito kama hizi ikawa maslahi yao ni madogo, wengine wenye viwango sawa vya elimu ni makubwa haliridhishi wala halifurahishi, linatia choyo au wivu ndani yake.

Kwa hivyo Mhe. Spika, nasema hawa watendaji walipwe kwa mujibu wa taaluma zinazofanana. Hili litakuwa jambo zuri. Kwa hivyo, hili suala tunamuomba Mhe. Waziri alifuatilie aone ile hali halisi iliyopo.

Mhe. Spika, sasa nataka nizungumzie jengo la Ofisi ya Tume ya Kurekebisha Sheria. Mhe. Spika, jengo hili kusema kweli kwa sasa hawana ofisi, halina nafasi, liko finyu na kila mtu anajua kutokana na shughuli zao zilivyokuwa nzito hata uwekaji wa yale mabuku yao na kila kitu chao utakuta pakuweka hapana. Kusema kweli iko haja ya kuweza kupatikana jengo jengine jipya. Ninachomuomba Mhe. Waziri, tume hii wapate nafasi haraka haraka kuingia katika hilo jengo jipya litakalopatikana na wao wajisikie na waweze kupanga mipango yao vizuri kabisa.

Mhe. Spika, baada ya hilo la tano nizungumzie juu ya biashara, wakala wa usajili wa biashara za mali. Katika suala hili huu usajili wa ukusanyaji wa mapato niseme tu kwa ufupi kwamba katika ofisi hii mapato kwa kweli ni mbovu sana. Kwa hivyo, ningelimuomba Mhe. Waziri kwamba mfumo huu wa ukusanyaji wa mapato kwa sababu ni mbovu ambao ndio sababu kubwa unaopelekea kukosa mapato, huo mfumo wenyewe ni mbaya, ni mbovu, hauridhishi, na ndio unaosababisha katika sekta hii watu kukosa mapato.

Kwa hivyo, nimuulize Mhe. Waziri ni lini mfumo mzuri ulio rasmi wa usajili utarekebishwa, kwani tuelewe kwamba msajili ni mmoja tu hakuna wasajili wengine, wote wadogo wadogo wanatakiwa wachukue mapato yao kutoka katika usajili ule.

Mhe. Spika, baada ya hilo mimi nilitaka nizungumzie hapa hapa katika hiyo Ofisi ya Msajili. Kwamba kuna hili suala zima la *IT* (*Information Technology)*.

Mhe. Spika, katika mambo ambayo yanajitokeza katika ofisi hii hawa watu ni muhimu sana na wanahitajika katika kila wizara. Lakini jambo lililojitokeza katika sekta yake ni kwamba maslahi yao hayafanani na wenzao kama wao walioko katika sekta nyengine. Hapa Mhe. Spika, nilitaka nizungumzie suala kwamba hawa wanakwenda katika sekta binafsi. Wanapokwenda kule mshahara wao unakuwa mkubwa kuliko sekta hizi za upande wa serikali.
Kwa hivyo, hili linasababisha katika sehemu hii ya *IT* kukimbiwa. Kwa hivyo, Mhe. Spika, kwa suala hili ningemuomba Mhe. Waziri ajitahidi kufuatilia ili kupatikane maslahi ambayo yanaweza kufanana kwa wote.

Niseme kidogo tu kwa Ofisi Kuu Pemba, kuna ufinyu wa bajeti. Na kwa mfano kipindi kilichopita waliweza kupata pesa kidogo sana kiasi milioni mbili tu, ambazo hizo zimeweza kugaiwa kwa vitengo vinne. Kila kitengo kiliweza kupata laki tano, jambo ambalo haliridhishi. Ningemuomba Mhe. Waziri alione hilo ofisi yake ilioko Pemba na baadhi ya vitengo vinashindwa kufanya kazi zao kwa ubora zaidi.

Mhe. Spika, ninalotaka kuzungumza sasa hivi ni suala zima Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Kitaifa. Mhe. Spika, hapa niseme kwa udhati na sisi tumevunjika moyo na hali ambayo tunaiona katika sehemu hii. Hawa wanaofanyakazi hapa, mfano wake labda ni kama watoto wa kambo katika serikali hii. Hawaulizwi kitu, watu wako mbali wana matatizo mengi.

Kitengo hiki cha nyaraka hawana vitendea kazi. Kama hawajapata vitendea kazi hivyo watu hawa wanakaa bure. Ofisi inafunguliwa asubuhi saa 2 wanaondoka 9, wanakwenda zao hawajafanya kitu hata kimoja.

Kwa hivyo tuwapeni likizo wende zao majumbani. Maana hapana kazi madawa hakuna, mpaka madawa yatakapokuja ofisi itakuwa wazi na watakuja kufanyakazi zao.

Jengine ambalo linajitokeza katika ofisi ile ni kwamba kuna ubovu wa thamani za ofisini. Hali ambayo hairidhishi utasema labda ofisi ile imetupwa, haina Mkurugenzi. Thamani ni mbovu jambo ambalo hata mengine

kuzungumza kwa ofisi ile si vizuri. Kwa mfano, hata lile kapeti lilotandikwa limeshakatika vipande vipande. Jambo ambalo la kusikitisha ni kwamba ile ni Idara ya Serikali lakini wanashindwa kuweza kupata fedha.

Mhe. Spika, ofisi hii pia ni chafu utasema labda imehamwa. Hilo ni jambo la msingi Mhe. Spika. Lakini zaidi ambalo linanisikitisha ni ile hali zile kumbukumbu za nyaraka zinawekwa. Kunakosekana kipoza hewa cha ofisi ile. Kinachojitokeza ni unyevu unyevu wa nyaraka na joto jingi sana lililokuwemo katika ofisi ile. Matokeo yake zile nyaraka zinapata unyevu unyevu na zinakuwa zinaanza kuvimba na kuharibika.

Kwa upande wa wafanyakazi wanashindwa kufanyakazi kutokana na joto lililomo katika chombo kile. Kwa hivyo, joto linaathari pande zote mbili; linawaathiri wafanyakazi na linaathiri zile nyaraka zilioko kule. Hizi ni nyaraka za kitaifa zinahitaji kutunzwa na kupewa usimamizi wa hali ya juu.

Mhe. Spika: Msheshimiwa muda wako umemalizika nakushukuru sana.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Ahsante Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kwa kunipatia nafasi.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Spika, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uzima na uhai leo hii. Tuko hapa kujadili maagizo ya kamati kwa wizara mbali mbali ambazo kamati ya Katiba na Sheria inazisimamia.

Mhe. Spika, kwanza niwapongeze Mawaziri kwa kazi nzuri ambazo walizozifanya na hatua ambazo wamezichukua ili kuona kwamba yale maagizo ambayo kamati yametoa yanafanyiwa kazi.

Pili nimpongeze Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Katiba na Sheria kwa kazi nzuri aliofanya. Kwa kweli kura zeti za kumchagua yeye hazikwenda kombo. Mhe. Spika, kwa kuanzia mimi naona bora nianze na Wizara ya Katiba na Sheria. Naomba nianze na Mahakama zetu. Mhe. Spika, kumekuwa na malalamiko mengi sana mahakama zetu kwamba hazifanyi kazi zake kwa ufanisi. Pamoja na changamoto nyingi ambazo zinakabiliana nazo pia kuna ubovu wa majengo ya mahakama zetu.

Mhe. Spika, nathibitisha hili kutokana na hotuba ya Mwenyekiti ambayo amejaribu kuainisha sehemu mbali mbali ambazo Mahakama inaonekana ziko chini katika utendaji wake. Ukiangalia Mhe. Spika, hotuba imesema kwamba kuna utendaji mbovu wa majaji. Hukumu zimetolewa kinyume na sheria,

dhamana zinatolewa bila ya kuzingatia utaratibu na kupelekea baadhi ya watuhumiwa wanaopewa dhamana kutopatikana tena.

Hotuba ya Mwenyekiti imediriki kusema kwamba utoaji wa dhamana katika Mahakama zetu umekuwa ni kama biashara ya duka. Na hii yote inasababishwa na rushwa ambayo zimetawala katika mahakama zetu.

Mhe. Spika, mahakama ikumbuke kwamba utoaji wa haki inahusisha taasisi nyingi za serikali kwa mfano kama *DPP* na Polisi. Sasa mahakama ikifanya kazi zake kwa kutegemea rushwa, kwa kweli wanazipa tabu hizi taasisi nyengine ambazo zinaisaidia mahakama katika kutoa haki.

Mhe. Spika, najiuliza kwamba huku mahakama kufanya inavyotaka yeye kunafanya ni kusababishwa na uhuru ambao imepewa kwamba haiwezi ikaingiliwa na kitu chochote na ndio maana wanafanya jinsi ambavyo wanavyotaka wao kufanya?

Mhe. Spika, sisi sote tumepewa uhuru wetu katika kufanya kazi zetu. Lakini kuna *check and balance* pamoja na kwamba tumepewa uhuru katika Katiba. Sasa mimi nafikiri huu uhuru ambao mahakama imepewa wao kufanywa kama waungu watu *astaghfirullah,* nafikiri ndio kunafanya mahakama kufanyakazi kwa jinsi inavyotaka.

Mhe. Spika, hata ukiangalia hotuba ya Mhe. Mwenyekiti, utaona jinsi gani hata yeye alikuwa anaogopa kuizungumzia hii Mahakama. Kwa mfano ukurasa wa nne na wa tano unasema kwamba:

"Mengine kutokana na mipaka ya kikatiba sitaweza kuyaeleza mbele ya chombo hiki"

Sasa ile *exclusive* ambayo tunazipa mahakama zetu ndio inapelekea na kufanyakazi kwa jinsi wanavyotaka.

Mhe. Spika, lakini kuna chombo hiki ambacho kinasimamia utendaji wa hawa Waheshimiwa wa mahakama. Chombo ambacho kinatakiwa kiwe kinaangalia. Sasa sijui kama kinafanya kazi au kipotu, sifahamu! Lakini mimi naona ule uhuru ambao umepewa sasa umekuwa mkubwa sana kiasi ambacho wenyewe wanafanyakazi wanavyotaka.

Mhe. Spika, kuthibitisha hilo ukiangalia tathmini ya kesi katika Ripoti za Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi. Ukurasa wa 31 utaona kwamba jinsi gani mahakama hazifanyi kazi ipasavyo. Kwa mfano kesi zilizofunguliwa katika baadhi ya mahakama zikiwemo za kipindi cha oktoba

na Disemba. Mahakama ya Mkoa kwa mfano Mwera zipo kesi 71 ambazo kati ya hizo ni kesi moja tu ambayo imetolewa hukumu.

Lakini pia ukiangalia Mahakama za Mikoa kuna kesi 203. Lakini kesi 27 ndio zimefunguliwa na zimetolewa hukumu ni 4 na nyengine 4 zimeondolewa na kesi 3 zimeshinda. Ukiangali ile *trend* ya mahakama zinavyofanyakazi. Kwa kweli hizi mahakama haziridhishi utendaji wake. Kutokana na hilo Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri alichukue kwa makini agizo la kamati lililomtaka kwamba Mhe. Waziri kukaa na watendaji wa mahakama na Tume ya Utumishi ya Mahakama, kushughulikia malalamiko. Kwa sababu inaonekana hali ni mbaya kuliko maelezo.

Mhe. Spika, mimi sitosema mengi kwasababu ni Mjumbe wa Kamati hii nitapitia pitia tu na ninawaachia Wajumbe wengine ili na wao watoe mapya katika wizara hizi.

Mhe. Spika, nikitoka hapo naomba niingie kwenye Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Mkurugenzi wa Mashtaka Mhe. Spika, kuna malalamiko sana ya ufinyu wa bajeti pamoja na kwamba tunaambiwa hali ni kwa wizara zote na taasisi zote. Lakini kuna maeneo ambayo unaangalia na unaona kabisa kwamba hawa wamezidi kunyimwa hizo pesa. Wenyewe siku hizi wanasema hakuna keki kuna kisheti. Lakini hicho kisheti kikigaiwa basi kila mtu apewe na sukari sio wengine wanapata na sukari na wengine wanapata unga mtupu.

Mhe. Spika, nikitoka hapo pia naomba niendelee katika Ofisi hii ya Mkurugenzi wa Mashtaka niichangie kuhusu mishahara ya *State Attorney* wa *DPP*. Mhe. Spika, *State Attorney* wa *DPP*, kwa kweli wana kazi nzito na kuthibitisha hilo ukiangalia tu *trend* ya hizi kesi ambazo zinazoingia na kutoka, utaona kwamba wao wana kazi kubwa kuliko ambayo hawa makahakimu wanafanya. Kwa hivyo, Mhe. Spika, tunaomba sana watu wanaohusika na mishahara waliangalie hilo.

Lakini Mhe. Spika, nitakuwa mpungufu wa shukurani kama sitopongeza Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kazi nzuri ambayo wameifanya ya kukamilisha ujenzi wa jengo lao jipya na hatimae kuhamia katika jengo hilo.
Mhe. Spika, nikitoka hapo naomba sasa niingie katika Wizara ya Kazi na Utumishi wa Umma. Kwa kuanzia Mhe. Spika, naomba nianze na maagizo ya kamati kwa wizara ya kazi.

Agizo namba 4 kamati inashauri ofisi zote za serikali zikamilishe matayarisho ya matumizi ya Mkonga wa Taifa ili na sisi tuweze kwenda na wakati na pia kuzidisha ufanisi katika kazi. Shauri lilipokelewa muda mrefu Mhe. Spika.

Lakini mpaka sasa ukiangalia bado Mkonga huu haujaanza kutumika licha ya pesa zilizopatikana na gharama kubwa kutumika.

Tumefikiria sasa hivi ingekuwa taasisi za serikali zinanufaika na Mkonga huu. Lakini nakumbuka tangu kamati ile tunaambiwa kuwa wizara zinajitayarisha kuweka vile vifaa ambavyo vitatumika katika huu Mikonga. Lakini mpaka leo halijakamilika. Hivyo naomba wizara ziharakishe zoezi hili tuanze kutumia Mkonga huu wa Taifa ambapo kutampungua gharama za kutumia *internet* katika maofisi yetu.

Mhe. Spika, naomba niingie katika Idara ya Nyaraka. Idara hii Mhe. Spika, kwa kuanzia nitaanza na idara yenyewe kabla sijaingia katika wizi wa nyaraka. Mhe. Spika, ile idara ni kama imesahaulika sifahamu ni kwa sababu ya eneo ilipo kwamba imejificha ficha hawaioni serikali au vipi. Lakini idara imesahaulika sana yule mzee *wallahi* mtamuuwa Mwenyezi Mungu amuweke. Tayari ameshapata maradhi lakini kesi za kazi zitampelekea amalizike kutokana na idara ile kutoendelezwa na serikali. Mhe. Spika, sasa hivi ukienda utaiona kama makumbusho tu.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa naomba tu labda isajiliwe nayo iwe kama sehemu ya kumbukumbu. Mhe. Spika, tangu enzi za kamati ile nakumbuka ya Mhe. Naibu Spika, tumekuwa tukipigia kelele sana baadhi ya mambo ambayo tulikuwa tukienda tukiyaona pale katika idara na hasa hili agizo la kuwekewa pale *CCTV*. Kutokana na hili mimi naomba niunge mkono hotuba ya Mhe. Mwenyekiti iliyosema kwamba kupotea kwa nyaraka zile labda ilikuwa ni makusudi. Tangu kamati ile tumekuwa tukipiga kelele sana kuhusu *CCTV camera.* Tulikuwa tunaambiwa maelezo tofauti katika kamati ambayo ilikuwa kipindi kile yalikuwa yanatia moyo, kwamba unaona labda kesho *CCTV camera* zitawekwa.

Mhe. Spika, cha kusikitisha kwamba mpaka leo hazijawekwa *CCTV*. Mimi naseme kilichowakuta wache kiwakute ni makusudi. Kwa sababu kamati inasema na wizara ilikuwa inayafumbia macho. Mhe. Spika, basi sisi kamati wasitusikilieze maana kazi yetu kubwabwaja. Lakini hata Mhe. Rais na yeye pia alitoa agizo pale sehemu ya nyaraka papatiwe *CCTV camera*. Si la kamati wala Mhe. Rais watu wanafanya wanavyojitakia wenyewe.

Mhe. Spika, kwa kuwa mimi ni mjumbe wa kamati sitokuwa na mengi. Lakini naunga mkono Wajumbe wenzangu waliosimama na kusema kwamba iundwe kamati iende ikachunguze juu ya kadhia hii. Kwa sababu ni kitendo cha makusudi kama kamati ilisema na mwenye nchi kasema kwa nini agizo hili halikutekelezwa.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja hii. (*Makofi*).

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ndogo na mimi nikaweza kutoa maelezo yangu kuhusiana na ripoti hii ambayo imewasilishwa hapa na Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, leo bahati mbaya sana hali yangu si nzuri kabisa, lakini kutokana na umuhimu wa mambo mawili ambayo ninayaona, hivi hivi nilivyo niyaseme kidogo.Lakini kabla ya yote nimpongeze Mhe. Mwenyekiti wa kamati kwa hotuba yake, imesisimua na niwapongeze Wajumbe wa Kamati kwa kazi nzuri ambayo wameifanya.

Mhe. Spika, tumeona namna ya utekelezaji wa maagizo mbali mbali ambayo Waheshimiwa Mawaziri hapa wametueleza namna maagizo yalivyokuwa na namna walivyotekeleza. Naiomba kamati ifatilie utelekezaji huo. Kwa sababu utekelezaji unaweza kuwepo kwenye maandishi. Lakini ukija kuona kwenye hali halisi ikawa ni sifuri. Kwa hivyo, tumepokea utekelezaji. Lakini fatilia namna ya utekelezaji wenyewe uhalisia.

Jengine Mhe. Spika, nije katika Idara ya Mahakama. Idara ya Mahakama tumepata maelezo yake na changamoto zilizopo. Ni changamoto nyingi ambazo zinazungumzia suala la ubovu wa mahakama. Na kama wezangu walivyotangulia kusema kwamba changamoto hizo kila wakati zinajirejea. Masuala haya tumekuwa tukiyazungumza lakini tunaendelea kuyazungumza kwa sababu ndio shughuli yetu.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir anasema kwamba tunaonekana tunabwabwaja, imekuwa kazi yetu kusema na tutaendelea kusema *inshaallah* Mwenyezi Mungu pengine iko siku atatuwezesha ili kuona matatizo yanaondoka. Idara hii ya Mahakama Mhe. Spika, ni idara ambayo inategemewa sana kuona kwamba inatoa haki. Lakini kumekuwa na malalamiko mengi juu ya utekelezaji huu wa shughuli za Kimahakama na utowaji wa haki.

Kwa hivyo, niwaombe sana wenzangu wa mahakama hawa watimize wajibu wao. Kwa sababu leo wapo duniani na kesho hawapo. Na sisi waislamu peke yake tunaemuelekea ni Mwenyezi Mungu. Lakini kwa kuwa tuko duniani basi tunao mahakimu wanaoweza kuhukumu na kutoa hukumu. Sasa watumie hekima zao na busara zao kuona kwamba kile wanachokihukumu au ile hukumu wanayoitoa basi inatoka ndani ya nyoyo zao na vile wanavyoona wao, kuliko kubadilisha hukumu kwa utashi au kwa sababu ya rushwa, kwa hivyo wajitahidi.

Lakini hapa nimwambie Mhe. Waziri wa Sheria kwamba kama anakumbuka aliniahidi wakati wa bajeti juu ya matatizo ya mwananchi wangu aliedhulumiwa pale mahakamani nyumba yake na akaniahidi kwamba atalishughulikia jambo hilo. Na mpaka leo hajalishughulikia na yule aliedhulumiwa anakwenda mahakamani na kurudi hapati majibu. Sasa nataka kumwambia Mhe. Waziri, rafiki yangu, kwamba bajeti inakuja nakusudia kuondosha shilingi katika bajeti, nampa tahadhari mapema ana miezi sita alishughulikie jambo hili. Nitaondosha shilingi kwenye mshahara wake na sitorudisha shilingi hiyo katu.

Niko makini katika hili siwezi kuona mwananchi wangu anadhulumika, nimesema nitumie nafasi hii nimwambie alishughulikie. Najua tutapiga kura katika bajeti na nitawaomba Wawakilishi wenzangu wanisaidie. Katika hili kuona mshahara wa Waziri tunauzuia. Kwa sababu kama mtu kumdhulumu mwenzake ni vizuri basi na yeye ataona uchungu wa kudhulumiwa haki yake, hilo nataka kumwambia Mhe. Waziri.

Jengine katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka tumeona changamoto hapa. Katika Ofisi yenye changamoto nyingi ni Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka. Moja ni maslahi ambapo wenzangu wamelizungumza kuna haja ya kuangalia maslahi ya ofisi hii. Kwa sababu hapa ndipo tunapoanzia kesi inayotakiwa kufikishwa mahakamani. Kwa hivyo, hawa na wao wanahitaji kuangaliwa sana na wamekuwa wakilalamika kila siku. Kwa hivyo, tuiombe sana serikali jambo hili waliangalie sana, ili ofisi hii iweze kufanya shughuli zake vizuri.

Eneo la mwisho Mhe. Spika, ni juu ya eneo hili la nyaraka ambalo nalo limenipelekea nisimame hasa. Mhe. Spika, kumekuwa na wizi wa nyaraka. Nyaraka nyingi zimeibiwa na kuna mbinu na hila nyingi za kuchukuwa nyaraka na eneo lile ni muhimu. Kuna malalamiko mengi humu ambayo yameelezwa ikiwa ni pamoja na ukosefu wa *CCTV* . Taarifa tuliyokuwa nayo kwamba Idara hii ya Kitengo cha Kupambana na Rushwa ambapo kiko chini ya Mhe. Waziri wa Utawala Bora. Kimekwenda na kimefanya kazi pale na kimegundua wizi wa nyaraka nyingi sana na taarifa hizo nnazo. Lakini ningemuomba sana Mhe. Waziri wakati utakapokuja kufanya majumuisho hapa wakati wa jioni, aje atupe taarifa ya taasisi ile ilivyokwenda kuchunguza pale. Ili wananchi wajue na serikali ijue.

Nakubalina na hoja na Mwenyekiti wa Kamati na Wajumbe wote kuunda kamati itakayoweza kuchunguza jambo lile. Kwa sababu pale nyaraka hazinunuliwi zinachukuliwa. Kuna watu wanakuja na mikoba ya fedha, wanatoa fedha, wanachukuwa nyaraka wanaondoka. Kwa hivyo, hili ni jambo la hatari Mhe. Spika. Kama taasisi ile tutaendelea kuachia vile, kesho na keshokutwa pale kutakuwa hakuna kumbukumbu yoyote.

Kwa hivyo, naunga mkono hoja ya kuundwa kamati japokuwa kamati ripoti zake hazifanyiwi kazi ipasavyo. Lakini lazima uchunguzi ukafanywe na taarifa zisomwe hapa. Ili kila mmoja ajue.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, naunga mkono hoja ya ripoti hii niwatakie kila la kheri ahsante sana.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nawashukuruni kwa kazi nzuri mnayoifanya. Waheshimiwa Wajumbe Wanawake kuna tangazo moja. Mhe. Mwenyekiti wa UWAWAZA ameniomba nitoe tangazo kwamba Waheshimiwa Wajumbe wanawake wabaki humu ndani kuna maneno kidogo anataka kuwaambia mara baada ya kuakhirisha shughuli zetu.

Baada ya hayo Waheshimiwa Wajumbe niakhirishe kikao hiki hadi saa 11:00 barabara jioni leo.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliakhirishwa mpaka saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, kabla ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha kuingia katika Baraza lako hili tukufu tukiwa na hali ya uzima. Lakini pia, nichukue nafasi hii Mhe. Spika, nikushukuru wewe kwa dhati kabisa kwa kunipatia tena nafasi hii.

Mhe. Spika, na mimi nitakuwa mwizi wa fadhila kama sikuisifu Kamati hii pamoja na Mwenyekiti wake ambaye ni mtoto mdogo, lakini mahiri, ripoti imepangika na imeingia nyama za kutosha.

Sasa Mhe. Spika, nitatoa dondoo maana yake mambo mengi yameshazungumzwa, lakini na mimi nitasema tu kidogo.

Kwanza Mhe. Spika, mimi kutajwatajwa Rais kwa kitu ambacho hakimhusu, kwa kweli hatumtendei haki. Mhe. Spika, Rais ana mtiririko wake wa uongozi. Amechagua Mkuu wa Serikali, amechagua Mawaziri, amechagua Makatibu Wakuu, Wakurugenzi, Makamishna, sasa hawa ndio wanaomsaidia Rais. Lakini tusimtajetaje kumfanya kama Rais ndio mtendaji wa shughuli zote, asingekuwa na mtiririko wake wa madaraka. Hilo nilisema kwa dhati kabisa.

Lakini jengine sheria tunazipitisha hapa Mhe. Spika, niseme tu nimwambie Mhe. Waziri, kwamba namuomba afanye *survey* ya hali ya juu kabisa au afanye *review*. Sheria nyingi Mhe. Spika, zimeshapitwa na wakati, lazima tukae kitako tubadilike twende na wakati. Kwa sababu tumewasikia Wajumbe mbali mbali hapa wamezungumza kuhusu suala hili.

Hebu Mhe. Waziri, akae kitako na vitengo vyake vyote, ahakikishe kwamba wanazipitia sheria Wizara kwa Wizara ambazo nyengine ni kwamba zimeshapitwa na wakati, basi tuzibadilishe twende na wakati. Maana kuna sheria nyengine sijui za toka mwaka 1800 sijui na ngapi, mwaka 1900 sijui na ngapi. Sasa hivi kwa kweli mabadiliko yameshaingia na wakati wake wa mabadiliko karne ya 21 wakati wa sayansi na teknolojia.

Lakini Mhe. Spika, na mimi nitilie mkazo ucheleweshwaji wa kesi kwa kweli unatupa matatizo, na saa nyengine mtu anakwenda anaambiwa njoo kesho kwa sababu mwenzake hakufika, lakini hafanywi chochote yule. Sasa hizo sheria sijui Mhe. Waziri, atakuja kutueleza hapa, ni matatizo yepi ambayo yanakumbana na hii ucheleweshwaji wa kesi.

Lakini pia, Mhe. Spika, mimi nasikitika sana mambo yaliyoingia sasa hivi huu mtandao wa udhalilishwaji kijinsia hasa watoto wa kike na wa kiume. Kesi mtu anapelekwa hospitali anapatikana kila kitu. Sasa hebu tuambiwe kuna nini hapa katikati kwamba mtu ameshatumia maisha yake ameshazaa, ameshajukuu, lakini anamchukua mtoto wa mwenziwe anamharibia maisha yake halafu hiyo fidia ni ya kichekesho.

Mhe. Spika, naiomba serikali kupitia kwako wewe Mhe. Waziri, tuweke sheria kali ya kuwa mtu asimharibu mtoto wa mwenziwe ambaye hajafika makamo, na hata akifika makamo kama bado hajabaleghe, basi achukuliwe hatua na amhudumie, au serikali imhudumie mpaka mwisho wa maisha yake kama yule hafai tena. Kwa sababu kuna wengine hawafai Mhe. Spika, wanawaharibu vibaya.

Mhe. Spika, jengine niwaambie watendaji wetu hebu hizi sheria tunapozitunga zikishakutiwa saini, basi tuzifuatilie. Lakini tuta, tuta, tuta, hata sijui tuta gani hilo. Maana yake tutachukua, tutafanya, sijui ni tuta gani hilo ambalo urefu wake halichupiki kwamba sheria hatuzitekelezi na ufuatiliaji wetu hatuutekelezi.

Mhe. Spika, niwaombe wenzangu sisi ndio watungaji sheria, basi kama sisi ndio watungaji sheria tuzitukuze zile sheria na sisi wenyewe tuzifuate. Mhe. Spika, ni mtu mmoja ambaye ninaogopa sana kukiuka sheria, kwa sababu mimi nimo humu ndani ndio mtungaji wa sheria. Naogopa sana, na hata

nikihamaki, basi ujue nimefanyiwa kitu ambacho kwa kweli hicho hakistahamiliki. Lakini naridhia sheria kwa sababu sisi ndio watungaji wa sheria.

Sasa Mhe. Spika, nije suala jengine wenzangu wamesema sana hapa kuhusu habari ya nyaraka na mimi nataka nitilie mkazo tu. Tusiwasamehe, uchunguzi ukipatikana kama watu wamepatikana na hatia, tusimsamehe mtu kwa ulafi wake, achukuliwe hatua kali za kisheria. Naomba sana Mhe. Spika, hili nilisema na mimi nilitilie mkazo.

Watu wamesema hapa limeibiwa sijui upanga wa polisi, na sisi hili rungu letu linalala huko huko. Mhe. Spika, tuweke tahadhari na hilo rungu letu la Spika la Baraza la Wawakilishi lisije nalo likapata mashaka. Nimesema hilo nilizungumze ili na sisi tuchukue tahadhari.

Lakini la mwisho kabisa Mhe. Spika, niseme kwamba lazima haki itendeke. Wenzangu wamezungumza vizuri na mimi naomba kutilia mkazo kwamba haki itendeke. Kwa sababu kumeingia mtindo na huu nasema mimi ni mtandao ambao kwa kweli sijui hao wenzetu watanisamehe wanasheria, na hao walioko huko wanaohukumu makesi haya. Lakini nasema haki itendeke tusifanye kitu ambacho Mwenyezi Mungu hayuko pamoja nacho.

Ukimtendea haki mwenzako, basi ujue na wewe utatendewa haki, lakini ukimnyima haki yake mwenzako, basi ujue na wewe kuna siku Mwenyezi Mungu atakunyima haki. Kwa hivyo, nilisema nizungumze hayo Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima na mimi niseme naunga mkono ripoti hii mia kwa mia. Ninawaomba wenzangu waunge mkono hii ripoti kwa sababu haikuficha kitu imeeleza ukweli ndani yake. Mhe. Spika, na mimi nisingetenda haki kama sikuchangia, lakini dondoo zote zimeelezwa na wenzangu waliotangulia. Kwa hivyo, na wale wenzangu ambao wamezungumza na mimi nawaunga mkono. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Ahsante sana, nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii adhimu ya kuchangia machache yaliyopo mbele yetu.

Awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma aliyetujaalia kufika hapa tukiwa wazima wa afya na kuweza kuendelea na shughuli zetu.

Baada ya hapo nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi kuweza kuchangia katika Wizara hizi tatu pamoja na hotuba yenye ripoti kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

Mhe. Spika, wakati Mwenyekiti wa Kamati alipokuwa akitoa ripoti yake kumejitokeza kwamba kuna changamoto nyingi ambazo kwa kweli ukiziona au ukizisikia kidogo zinatia wasiwasi mkubwa. Moja katika hilo ni kwa upande wa Mahakama.

Mhe. Spika, tunaelewa kwamba Mahakama zetu zina matatizo ya ufinyu wa ofisi, ubovu wa majengo, uhaba wa vifaa, pamoja na ukosefu wa usafiri na kadhalika. Lakini inasikitisha zaidi ikiwa kesi haziendi au kesi kusitishwa kwa sababu ya ukosefu wa karatasi ni aibu. Mhe. Spika, nasema hivyo kwa sababu ripoti hii ndio inavyosema. Kuna kesi ambayo ilisitishwa kwa sababu ya ukosefu wa karatasi. Na hilo ni la ajabu kwa sababu ndani ya Baraza hili tumepitisha bajeti ya Wizara hii na bila shaka ndani ya bajeti hiyo vimo vifaa ambavyo vinatakiwa kutumika katika Mahakama. Sasa Mhe. Waziri, akija hapa atueleze vizuri kwa nini matokeo kama haya yanatokea ndani ya Mahakama kwa sababu sio jambo la kawaida.

Mhe. Spika, jengine ni kwamba katika ripoti imeonesha jinsi gani wananchi wanalalamika kuhusu utendaji wa Majaji ambao wamepewa jukumu la kutoa hukumu za haki ndani ya Mahakama zetu, lakini hukumu zile zinavyotolewa inaonesha dhahiri kwamba uwezo wa Mahakimu hawa ni mdogo. Haiwezekani leo kesi ya udhalilishaji kwamba mtu anahukumiwa kwa faini ya shilingi laki nne. Na kama kuna Jaji ametoa hukumu hiyo hafai kuwekwa ndani ya taasisi ya Mahakama.

Mhe. Spika, juzi tulikuwa tunashuhudia kuona namna hisia walizotoa Waheshimiwa Wajumbe jinsi ya kesi za udhalilishaji zinavyowaumiza. Na sote tumekubaliana kwa pamoja kwamba hakika suala hili limekuwa ni suala la mtambuko kila mtu ana hisia nalo. Leo Jaji ambayo sheria inasema kwamba mtu yeyote anayefanya jambo hili, basi hukumu yake ipo, lakini sio ya faini. Sijawahi kusikia dunia nzima kwamba mtu anayemdhalilisha mtoto analipa faini. Unalipa faini ya nini? Mhe. Waziri, tutataka maelezo kwa hili.

Mhe. Spika, tatizo jengine ambalo limejitokeza ndani ya ripoti, mimi namshukuru sana, namsifu sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati hii. Ripoti yake aliyoitoa kwa kweli ni ripoti inayotupa picha halisi ya Mahakama zetu zilivyo hakuficha kitu. Nampongeza sana pamoja na wanakamati wote. Kesi nyingi zinacheleweshwa hususan hizi kesi za udhalilishaji.

Mhe. Spika, mimi na wewe hivi karibuni tulipokwenda Pemba tulizungumza na Mashekhe wa Pemba Kusini, tukawaambia tusaidiane kwenye hili, kwa sababu hili ni tatizo kubwa, hili ni tatizo la kitaifa, tunusuru watoto wetu kwenye haya majanga. Mhe. Spika, unakumbuka walivyojibu wakaturudishia

sisi wakasema sisi tunafanya jitihada zote, lakini zikifika katika maeneo fulani kesi kama hizi, hazina hukumu wahusika tunawaona wanatembea barabarani.

Leo ripoti hii Mhe. Spika, inasema wazi kabisa kwamba dhamana zinatolewa kama njugu zinauzwa biashara, tatizo. Kwa hiyo, haya mambo si rahisi kumalizika ikiwa kama tutakuwa na Majaji ambao kwa kweli hawafanyi kazi zao kama inavyostahiki hawafuati sheria. Tatizo litakuwa halimaliziki.

Mhe. Spika, tunajua na watu wengi wanajua kwamba tatizo kubwa ni rushwa. Kwa kweli ndio maana inayosababisha katika taasisi hizi kesi kuchelewa au hizo ambazo tunasema kwamba badala ya mtu kuhukumiwa kutokana na sheria anaambiwa toa shilingi laki nne halafu nenda nyumbani kalale, ina maana kwamba endelea tena kufanya. Na tatizo ni kwamba hawa watu hawajui Mhe. Spika, nasema kwa uchungu hawa watu hawajui kwamba tatizo huyu mtu akifanya mara moja atarudia kufanya tena, litakuja kukufika wewe ambaye uliyemwambia akakae nyumbani. Hafanyi mara moja, hawa watu wanakuwa wana matatizo. Sasa leo tunapowaruhusu na tunapowaachia hivi kirahisi rahisi Mhe. Spika, tusione tu kwamba hili limemfika mtoto wa fulani au fulani, litakuja kuzunguka likufikie wewe ndani ya nyumba yako utasemaje?

Kwa hiyo, Mhe. Spika, nasema tena Mahakama zetu kwa kweli zina matatizo na zinatuumiza. Mhe. Waziri, sijui kama hiki kitu mnacho, lakini hebu tuanzishe *bureau* maalum ambayo itakuwa inasikiliza malalamiko ya wananchi kuhusu masuala hayo. Na wewe mwenyewe ndie utakayekuwa msimamizi mkuu kwa sababu hili ni tatizo. Mhe. Spika, sitaki kupoteza muda wangu mkubwa wa kusema, lakini linaniuma na kila mmoja wetu linamuuma. Mhe. Spika, naomba sana Mhe. Waziri, hili alisimamie na suala zima la kuanzishwa *bureau* ambayo itakuwa inasikiliza malalamiko ya wananchi. Kuhusiana na masuala mbali mbali yanayohusu kesi, basi uyasimamie mwenyewe ili iweze kufanya kazi, labda hapo haki inaweza kutendeka.

Mhe. Spika, jengine ambalo nataka kulizungumzia ni Tume ya Kurekebisha Sheria. Mhe. Spika, ripoti imeeleza kuna matatizo mengi na matatizo hayo yanasababisha masuala mengi ya sheria na kazi nyingi za ofisi hii kutofanyika. Mhe. Spika, kuna taarifa moja ambayo imetolewa na ripoti hii hasa ikihusiana na suala zima la kurekebisha sheria na kuanzisha sheria nyengine.

Mhe. Spika, tatizo ambalo linajitokeza sasa hivi sheria zetu nyengine haziendi sambamba na ukuaji wa teknolojia. Mhe. Spika, hivi sasa watu wanaitumia teknolojia kwa kufanyia mambo maovu. Sote sisi mashahidi, mengine tumeyaona na tumeyasikia, lakini watu wale hawawezi kuchukuliwa hatua.

Hakuna sheria ambayo inaweza kumfunga mtu yule kwa kutumia vile vifaa akaweza kuchukuliwa hatua ya kisheria.

Mhe. Spika, kuna matatizo makubwa ndani ya jamii yetu, kuna watu wengine wanachukua picha na kuzisambaza na kuweza kumkashifu yule mtu, lakini hamkashifu peke yake, anamkashifu na wazee wake, anamkashifu na majirani zake na anaikashifu jamii nzima ya Zanzibar kwa sababu hatujui picha zile zinafika wapi. Zinakwenda kwenye mitandao zinarushwa na bila shaka akasema hiki kitendo kimefanyika Zanzibar ni aibu kwetu sote. Mhe. Waziri, hili lisimamie, sheria ziwepo ziwabane watu hao waogope kufanya mambo hayo.

Mhe. Spika, jengine ambalo nilikuwa nataka kulizungumzia ingawa wenzangu wengi sana wameligusia ni suala zima la nyaraka. Mhe. Spika, tunaelewa nini maana ya nyaraka na umuhimu wake, sio kwamba ni makaratasi tu ambayo yanawekwa, lakini ule ni utajiri, ile ni historia ya nchi, ya taifa. Leo na kesho sisi tutakuwa hatupo, lakini nyaraka ndio zitakazoeleza. Nyaraka zile ambazo nyingi zimepotea hapa Zanzibar zina historia nzito inayohusu Zanzibar, leo watu wanakwenda kuzichukua nyaraka zile kwa *interest* zao wenyewe wameuza, wengine wamepata pesa wametajirika, lakini mwenye hasara ni sisi Wazanzibari sote. Sasa vizazi vyetu vijavyo vinakosa historia ile.

Mhe. Spika, mimi nilipata bahati kama miaka mitano iliyopita nilikwenda Ujerumani nikaenda kwenye sehemu ambayo wanahifadhi nyaraka zao kulikuwa na historia ya Zanzibar kubwa na kwa bahati nzuri kulikuwa na Waziri pale pale alisema nyaraka hii Zanzibar haipo. Kulikuwa na historia ambayo ni ya miaka mia moja nyuma iliyopita, inahusu uhusiano wa Ujerumani na Zanzibar, namna wafanyabiashara walivyokuwa wanakuja Zanzibar kuchukua bidhaa.

Bidhaa nyengine zilikuwa zinatoka Tanzania Bara zinakuja hapa zinachukuliwa zinapelekwa. Bidhaa za karafuu, pembe za ndovu, na bidhaa nyingi na mpaka mikataba ya biashara hizo. Yote hayo ni utajiri ambao Zanzibar sisi tunatakiwa tuwe nao. Leo nyaraka kama ile na imehifadhiwa vizuri Mhe. Spika, mpaka na sahihi za wafalme na kila kitu.

Mhe. Spika, la mwisho naomba nizungumzie suala la Baraza la Manispaa nimeliona hapa, wamepata gari nawapongeza sana kwa kweli, lakini bado mji wetu mchafu na sijui wamejipanga vipi kuhakikisha unakuwa msafi. Kwa sababu kero kubwa ilikuwa ni kwamba hatuna gari za kukusanyia taka, leo gari zipo kwa nini bado mji mchafu. Kwa hiyo, Mhe. Wazir, akija hapa atwambie na kama gari hazijaanza kazi kwa nini? Kero kubwa sana kwa

sababu kuna takataka mjini Unguja ni kuchafu na wala hayataki tochi ukipita unaona.

Mhe. Spika, mwisho kabisa nilikuwa nataka kuzungumzia suala zima la Chuo cha Mafunzo. Nimeona katika ripoti, Mwenyekiti anasema kwamba Chuo cha Mafunzo kulitolewa ushauri wa kuwaruhusu wawekezaji wawekeze katika miradi iliyoko kule. Hilo halijafanywa. Namuomba Mhe. Waziri, akija hapa atueleze kwa nini halijafanywa.

Lakini hata na mimi tulipokuwa kwenye Kamati yetu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa tulilizungumzia hilo na mara nyingi tulikuwa tunakwenda katika taasisi hizi tunakuta kwamba vifaa ambavyo vinatumika katika miradi mbali mbali kwa kweli vimechakaa na havisaidii kitu. Sasa Mhe. Waziri, akija hapa namuomba sana atueleze ni lini au ni hatua gani ambayo tayari ameshaichukua kuhakikisha kwamba wawekezaji na wao watapata fursa ya kuwekeza katika maeneo hayo.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo machache, nakushukuru tena kunipa nafasi na naiunga mkono ripoti ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Katiba, Sheria na Utawala kwa asilimia mia moja. Nakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Mhe. Mgeni Hassan Juma, tunakushukuru sana kwa mchango huo. Waheshimiwa Wajumbe kama kawaida yetu kwenye shughuli zetu huwa tunafikiwa na wageni mbali mbali na leo hii tumefikiwa na wageni ambao wapo juu pale. Nao ni Waheshimiwa Wabunge wa Baraza la *TAITA TAVETA*, yaani *TAITA TAVETA COUNTY ASSEMBLY* kutoka nchini Kenya. Waheshimiwa Wabunge hao wanaongozwa na Spika wa Baraza hilo ambaye ni Mhe. Maganga Meshack, namuomba asimame. Pamoja na Mhe. Naibu Spika ambaye ni Mhe. Cryspus Masaga. Yupo *Majority Leader* Mhe. Solomon John. Na yupo *Minority Leader* Mhe. Ronald S.

Mhe. Spika: Waheshimiwa wageni hawa jumla yao ni 45, viongozi ndio hao, lakini wamefuatana pamoja na Katibu wa Baraza hilo, mpambe yaani *Seargent at arm* na watendaji wengine 7. Wote kwa pamoja naomba wasimamie kusalimiana na Waheshimiwa Wajumbe. (*Makofi*).

Ahsante sana Waheshimiwa Wajumbe hao ndio wageni wetu kwa leo. Wenzetu Waheshimiwa Wabunge kutoka majimbo mbali mbali ya Kenya wanatabia wanapokuja hapa Zanzibar, huwa wanakuja kuwatembelea ndugu zao hapa Zanzibar ili kuonana nao na waone namna ya shughuli zetu zinavyokwenda. Waheshimiwa Wabunge karibuni sana. Ahsanteni sana.

Mhe. Abdalla Mohamed Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi jioni hii kunipatia fursa ya kusema machache katika ripoti hii ya mwaka ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Mhe. Spika, kwanza ningependa tu kumkumbusha mwalimu wangu wa siasa Mhe. Ismail Jussa Ladhu, asubuhi hapa alilalamika kwamba Baraza hili halipewi hadhi na serikali, labda nimkumbushe tu kwamba Baraza hili linapewa hadhi na Katiba na kama tutasubiri kwamba Baraza hili lipewe hadhi na serikali, basi itafika siku jua litakalotokea magharibi na kutulia mashariki hadhi hiyo haifiki. (*Makofi*).

Ninafikiri tu tufike wakati *back practice* na ninafikiri kipindi kifupi kilichopita wenzetu wa Bunge la Jamhuri wa Muungano wa Tanzania walitufundisha na hili tulichukue kama ni *case study*. Kwa hivyo, Mhe. Ismail Jussa Ladhu, kama unatarajia kama kwamba tutapewa hadhi na serikali, hilo mimi sifikirii, Katiba inaturuhusu sisi kujipa hadhi wenyewe.

Mhe. Spika, kama walivyoeleza wenzangu ripoti hii ni nzuri, lakini tusiiache tu hivi hivi bila ya kuitonesha kidogo. Mhe. Spika, mimi ninataka kidogo niingie katika Idara ya miundo ya taasisi utumishi na maslahi ya watumishi wa umma.

Mhe. Spika, ripoti imeeleza kwamba katika utekelezaji kumekuwa na marekebisho ya mishahara na kama sisahau katika mpango wa makadirio na matumizi yaliyopita, Baraza lako tukufu liliidhinisha bilioni 17 kwa ajili ya marekebisho ya mishahara. Mhe. Spika, kumekuwa na malalamiko mengi kwamba mara hii haikujulikana, ni utaratibu gani uliotumika, labda tulirudia kwa wazee tu, tukasema kwamba nyoongeza huenda funguni. Kwa hivyo, wale waliokuwa na fungu kubwa, basi wakaongezwa makubwa zaidi na wale waliokuwa na fungu dogo, basi wakaongezwa padogo zaidi.

Mhe. Spika, ni masikitiko kusema kweli kwa sababu sikujua mpaka hivi sasa mimi. Je, kulitumika utaratibu gani wa kuongeza mishahara hii. Namuomba Mhe. Waziri, atakapokuja kwa vile watumishi wengi wana kilio kwa hili, angetupa utaratibu hasa, je, mafungu haya au nyongeza hii imetumika kwa utaratibu gani.

Mhe. Spika, nyongeza iliyopita tunajua kwamba walitumia vigezo vya elimu, lakini mara hii ninashangaa kwamba kulikuwa na *flate rate* ya ishirini na tano elfu kwa wale wa ngazi za chini, lakini ngazi ya juu sikujua imetumika nini. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri, aje atueleweshe ni utaratibu gani uliotumika mara hii au kulikuwa na formula ya kuongeza mishahara. Kwa sababu wengine tunasikia walikuwa wameingiziwa *risk allowance*, wengine hakuna *risk allowance*. Kwa hivyo, sijui kulikuwa na utaratibu upi.

Ninafikiri Mhe. Spika, Mhe. Waziri, amenifahamu ili kuondoa longolongo za watumishi wa umma na ilifikia wakati ninafikiria wengine walipanga. Wazungu wanasema; *to go on strike*, lakini ilitokea fununu kwamba Mhe. Rais, labda aliwaomba awasubirie mpaka Januari, leo tupo tarehe 25, sijui Januari inamalizika lini na zimebakia siku ngapi za kutoa ufafanuzi kuhusu suala hili. Ningemuomba Mhe. Waziri, akatupa ufafanuzi wa kina kuhusu suala la nyongeza za mishahara.

Mhe. Spika, jengine ninalotaka kulizungumza ni utaratibu wa ajira. Hapa imeelezwa kwamba kigezo cha mwisho ni kutumia *GSO*, wala Kiingereza sijui na sijui urefu wake ni nini. Lakini kitengo hiki kimepewa mamlaka ya kuwachunguza watumishi wa umma ili uajiriwe unahitajika upite hapo.

Lakini unapopitia hapo kinachoangaliwa zaidi kwa ripoti hii ni kwamba unaangaliwa kama cheti chako aidha umekipata kwa uhalali au sio uhalali, kwa sababu imegundulika kwamba baadhi ya nchi zinatoa vyeti ambavyo havina uhalali.

Sasa mimi ninafikiria pia sheria inasema kwamba inapotokea ajira kazini, inawajibika wizara husika ya Utumishi ya Umma itangaze kwamba kutakuwa na nafasi katika wizara fulani na wanatakiwa watu wenye sifa Fulani waombe nafasi hizo. Lakini la kushangaza Mhe. Spika, baada ya kufanya usaili huo, matokeo hatuyajui. Kwa hivyo, mimi nina wasi wasi kwamba kitengo hichi kinakwenda zaidi ya kuangalia cheti na sijui kitengo hichi kitakuwa kina utaalamu gani wa kujua kwamba huyu ana utaalamu kweli, fulani achukuliwe zaidi ya kile cheti au vipi. Nina wasi wasi kwamba tutakosa wataalamu kwa kuangalia mazingira kama hayo peke yake.

Sasa mimi ningeomba wizara ili suala hili liwe la uwazi, basi sijui Mhe. Waziri, atatumia njia gani ya kututoa wasi wasi, kuona kwamba kitengo hichi hakiangalii zaidi ya suala hilo la vyeti. Mimi ningependa tu Mhe. Waziri akatoa sasa, kwa vile wale wametangaza katika gazeti au katika vyombo vya habari kwamba wanatakiwa waliokuwa na sifa fulani fulani, basi baada ya *interview* na wale watakaokosa na wale watakaopata na zile sifa zao na ubaya wao, basi pia wakaekwa wazi ili tukaridhika roho zetu kwamba hawa na wao wamekosa kwa sababu moja mbili, na hawa wamepata kwa sababu moja mbili. Ninafikiri Mhe. Waziri, akanifahamu na ningemuomba akalitolea ufafanuzi suala hilo.

Mhe. Spika, jengine ninataka kulizungumzia ni suala la majanga au wakati wa kutokea maafa. Ripoti imezungumza kwamba hivi sasa kuna boti tano ambazo zimenunuliwa kwa ajili ya kuokoa au kwa ajili ya zoezi lolote litakalotokea wakati wa maafa. Mhe. Spika, uzoefu unaonesha kwamba hasa katika bandari

ya Mkoani kuna boti, lakini yanapotokea maafa yoyote boti ile huwa mara nyingi haiwezi kufanya kazi kwa sababu waliopo pale wanakuwa aidha hawana mafuta, yaani petroli ya kuwawezesha kufanyia shughuli zake.

Sasa mimi ninafikiri uwepo tu wa boti hizi tano, si lolote si chochote kama itakuwa hazijawezeshwa kwa ajili ya kufanyia kazi hizo. Sasa ningeomba tu kwamba boti hizi zitumike kikamilifu na kutumika kwake ni kupatikana kwa nyenzo hiyo ya nishati ya mafuta ambayo itawawezesha wao kufanya kazi.

Ninashukuru kwamba wakati wowote inapokuwa operesheni ya uchumaji wa karafuu, basi wakati wowote boti hizi hazikosi mafuta. Lakini linapomaliza zoezi hili, basi Mhe. Spika, tunapokwenda kutoa ripoti kwamba kuna tokeo fulani, unaambiwa kuna upungufu wa nishati ya petroli. Naomba hili Mhe. Waziri, akaliona na mara nyengine lisitokee tena.

Mhe. Spika, ripoti pia imeeleza kwamba kutakuwa na utanganisho wa Vyuo vya Mafunzo kwa ajili ya watoto na watu wazima. Lakini kila mwaka inakuwa ni mtiririko wa maneno tu, kubadilisha maneno, tutabadilisha basi. Ninafikiri sasa ipo haja ya hivi sasa kuona kwamba suala hili ni muhimu na sijui kwa ripoti hii Mhe. Spika, inatuonesha kwamba kwa sehemu ya Unguja tayari zoezi linafanywa la ujenzi wa nyumba hiyo, lakini kwa sehemu ya Pemba bado. Sasa sijui Mhe. Waziri, anatwambia nini kwa sababu umuhimu ni sawa kwa sawa.

Sasa ikiwa huku kumeonekana upo umuhimu, basi na kule ningemuomba Mhe. Waziri, suala akalifanya kwa wakati mmoja ili kuondosha ule usumbufu wa watoto kukaa pamoja na watu wazima.

Mhe. Spika, jengine ni upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa. Mhe. Spika, nalo hili ninafikiri ni suala la kuliangalia. Tukielezwa hapa kwa makaratasi utaona ukenda huko vizazi na vifo asubuhi, ukifika saa moja na nusu, ikifika saa nne cheti chako utakipata. Lakini Mhe. Spika, ukweli sio huo. Ukweli hivi sasa upatikanaji wa vyeti ni mgumu. Ningemuomba Mhe. Waziri, hili akaliona kwamba upatikanaji hata kwa yule ambaye katimiza masharti yote ni mzito. Kwa hivyo, nalo hili akalifanyia kazi haraka sana ili walio na haki hii wakapatiwa mapema mno.

Mhe. Spika, kwa hayo machache, ninakushukuru na ninaunga mkono hoja. (*Makofi*).

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Ninakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa na mimi fursa hii ya kuzungumza machache katika ripoti hii ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

Awali ya yote, nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu na nimtakie rehma Mtume wetu Muhamad (SAW) kwa kutujaalia tukakutana hapa tukiwa ndani ya hali uzima na afya njema.

Lakini ninataka nichukue fursa hii Mhe. Spika, kuzishukuru wizara tatu ambazo ni wizara zinazosimamia Kamati hii ya Katiba, Sheria na Utawala kwa mashirikiano makubwa ambayo kuwa wanaipa kamati hii na ndio maana ikafika leo wakaweza kuwasilisha ripoti hii ambayo kuwa imegubikwa na changamoto nyingi za kiutendaji.

Lakini Mhe. Spika, kwanza kabisa ninataka nisema kwamba ripoti hizi tatu ambazo zimewasilishwa hapa, changamoto nyingi ziliomo, basi ni ukosefu wa bajeti finyu ambayo zinapelekwa katika wizara hii. Mhe. Spika, hii ndio changamoto kubwa ya ukosefu wa fedha na ndio maana yakaweza kujitokeza ambayo yamejitokeza hapa.

Mhe. Spika, kila taasisi unayokwenda changamoto hiyo ni changamoto ya kitaifa. Kile walichoahidiwa kupewa inafika pahali hawapewi. Sasa sijui utekelezaji huo utakwenda vipi bila ya pesa. Unafika pahali ukenda kwenye taasisi hata ile huduma ya kulipia umeme haipo. Sasa sijui ofisi hiyo itaendeshwa vipi. Kwa hivyo, mimi namuomba Mhe. Waziri wa Fedha, wizara wanapozipangia zile bajeti, basi hizo ndogo zinazopatikana basi zipelekwe kwa wakati na kama hakuna uwezekano huo, hakuna haja ya kutangazwa bajeti ambayo inayofika pahali haifiki kwa yale mahitaji yanayokusudiwa kutekelezwa na wizara hiyo. Kwa hivyo, ninamuomba Mhe. Waziri wa Fedha, hizi aziangalie sana masuala mazima ya bajeti.

Mhe. Spika, mimi ni miongoni mwa mjumbe wa kamati hii, lakini na mimi ninasema niweze kutoa mchango wangu mdogo, kwanza kuiunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia. Lakini kwanza nianze na hii Wizara ya Katiba na Sheria, wizara ambayo imezungumzwa sana hasa katika suala zima la Mahakama na mifano mbali mbali imetolewa.

Mhe. Spika, haya yote ni mambo ambayo tumeyapata ndani ya wizara hii. Kwa hivyo, Mhe. Spika, ninamuomba Mhe. Waziri, suala zima la Mahakama zetu uadilifu haupo, akitaka asitake, rushwa zimetawala, lakini na uadilifu haupo.

Mhe. Spika, umetolewa mfano wa kesi ya udhalilishaji. Lakini mimi ninataka nimpe mfano wa gereza moja la hapa Kilimani tulililokwenda tukatembelea. Pale tulitembelea tukawaona wafungwa mbali mbali, pia, tulikuwa tukiwahoji suala zima la kupelekea kufikia pale. Lakini tukafika kuna wanawake watatu. Miongoni mwao mmoja mwanamke yule tulimuhoji, lakini la kusikitisha

alitueleza pale na machozi yanamtoka, kuwa alifika pahali kuwa kesi yake kumalizika kabisa, kwa sababu ameshatolewa faini isiyopungua milioni mbili.

Lakini la kushangaza Mhe. Spika, kwenda na kurudi mwanamke yule alikwenda akachukuliwa akafungwa, na faini ameshatoa ambayo kuwa kesi imeshamalizika. Sasa hili linasemekana pengine ndani ya faili ilikuwa mtu yule afungwe, lakini kwa udanganyifu pengine ya mtendaji fulani akafika pahali akamwambia pengine ukitoa shilingi milioni mbili ina maana kesi yako imeshamalizika.

Sasa hapo Mhe. Waziri, uadilifu upo wapi. Mwanamke yule anasikitisha na anahuzunisha. Sasa Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria ,ni jukumu kubwa ulilonalo la kutoa haki na pengine wengine watu wanyonge ndio waliomo mule, uadilifu mwengine wowote wakubwa huwakuti pale, hata wakafanya ubadhirifu gani. Lakini unaowakuta pale ni watu wanyonge. Kwa hivyo, na wao wanatakiwa wafanyiwe haki ijapokuwa wana makosa, lakini saa nyengine wasionewe kupita kiasi kama hicho.

Mhe. Spika, jengine kwenye ripoti hii ya Wizara ya Kazi na Utumizi wa Umma kuhusu Idara ya Sera, Mipango na Utafiti. Kuna agizo nambari moja ambalo kuwa kamati naomba Mhe. Spika, ninukuu hii agizo hili. Kamati ilitaka kujua mchanganuo wa pesa zilizotumika katika kukamilisha mradi wa *e-government*, kwani zile ni kodi za wananchi. Hivyo, kuna ulazima zikawekwa bayana ili kila mwananchi ajue ni kiasi gani mchango wake umehusika katika mafanikio ya Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Lakini utekelezaji wake wamesema hivi watu wa wizara, kuwa wizara yetu haikuwa msimamizi mkuu wa mradi huu, bali iliyokuwa ikisimamia ni Wizara ya Fedha ndio iliyokuwa msimamizi mkuu. Hivyo, Mhe. Mwenyekiti, naiomba kamati yako iendelee kuwasiliana na Wizara ya Fedha ili kupata mchanganuo mzima wa matumizi wa mradi huo. Kwa hivyo. Mhe. Spika, inaonesha hii bado haijatolewa ufafanuzi katika utekelezaji. Kwa hivyo. tunaomba huyo Waziri husika.basi aweze kutupatia ufafanuzi ili tuweze huo mchanganuo unaotarajiwa.

Mhe. Spika, jengine ni Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu ya Taifa. Mhe. Spika, watu wote wameshazungumza hapa, lakini jambo la kusikitisha sana idara hii jinsi inavyotupa na serikali. Mhe. Spika, idara hii hairidhishi na kwa kweli ninaweza kusema imesahauliwa kabisa, hapana liliopo katika idara hii na idara hii ni muhimu kwa serikali yetu.

Idara hii inaweza kupata wageni mbali mbali ambao watakaoingia pale kwa kutafuta kumbukumbu zilizo muhimu za nchi yetu. Leo Mhe. Spika, ile idara

ukiingia mule hata dakika tano ukaweza kukaa ukapekua-pekua. Hamna vitendea kazi, yule mkurugenzi aliyekuwepo pale maskini ni mtu mzima, kaekwa pale hata gari hapana, wakati wizara nyengine zina gari hazipungui tano, sita. Wizara nyengine kila mwaka wanabadilisha fanicha ndani ya maofisi yao, lakini idara ile haitambulikani, viti vyao wamefungwa kamba.

Sasa nilisema hizo wizara nyengine ambazo kuwa kila mwaka wanabadilisha fanicha, lakini kwa nini hizo wanazobadilisha wao hawapelekei wao kule. Kwa kweli inasikitisha wale wafanyakazi tuliokwenda kuwakuta wanaonesha huruma, yaani wanakaa pale kwa ajili ya kuwa wapate ile riski tu, lakini kwa kweli haitambulikani kama ni idara ya serikali hasa.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri, hili tunakuomba sana na wizara yako hii pia inahusika na idara ya usalama wa kazini, upo usalama pale, upo wapi? Wakati yeye mwenyewe hiyo idara yake haipo katika hali ya usalama na wafanyakazi wake, atakwenda kuona idara nyengine kutafuta huo usalama ndani ya kazi? wakati yeye kitengo chake tu pale hawezi kushughulikia wakawa na usalama wale wafanyakazi wanaofanya kazi. Kwa hivyo, lile ni jambo la kusikitisha, tena la kuonesha huruma, wametupwa kule sijui kwa kuwa hawapo maeneo ya mjini au vipi. Kwa kweli ni jambo la kusikitisha ...

Mhe. Spika: Una dakika 5.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Akaa! Mhe. Spika, kama nina dakika 5 nina langu moja ambalo kuhusu Kikosi cha Zimamoto, mimi naona nimepata muda mdogo sana.

Mhe. Spika, katika Kikosi hiki cha Zimamoto ninamuomba Mhe. Waziri, bado ni tatizo katika eneo letu la Mkoa wa Kaskazini Pemba, hakuna kituo cha Zimamoto, jambo ambalo linalopelekea tunapotokewa na mafaa hupata usumbufu mkubwa. Juzi matokeo tumeyaona yaliyotokea kule Shumbamjini na wapi kule.

Na kwa bahati nzuri suala hili Mhe. Waziri, tulilieleza tulivyokutana na kuna mtendaji wako mmoja akasema kwa kuwa tatizo liliopo kule walikosa kiwanja cha kujengea ofisi hiyo ya kuweka kituo cha zimamoto. Si kweli Mhe. Waziri. Mimi nilimuuliza Mkuu wa Mkoa, nilipomuuliza akaniambia hawajasema kweli kwa sababu yeye kasema kawapa kiwanja Wete na kawapa kiwanja Micheweni eneo liliopo kulipokuwa na redio jamii.

Kwa hivyo, yule mtendaji wako, ina maana siku ile aliidanganya kamati na hili suala twende tufanye siku tupate twende au lifuatilie wewe, hakujakosekana kiwanja cha kujengwa ofisi ya zimamoto. Mhe. Spika, ni

tatizo. Mhe. Waziri, tunakuomba sana suala hili ulishughulikie ili angalau ile Wilaya ya Micheweni kwa sababu hata hiyo mipango miji yenyewe haipo kule. Kwa hivyo, tunakuomba Mhe. Waziri, suala hili ulishughulikie ili kuweza kupata kituo katika eneo letu la Micheweni.

Mhe. Spika, kwa hayo machache naunga mkono asilimia mia. (*Makofi*).

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Ahsante sana Mhe. Spika, awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kukutana katika hali ya uzima na afya njema katika jioni hii ya leo.

Na pia, nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia ripoti ya Katiba, Sheria na Utawala. Lakini nitakuwa mwizi wa fadhila, pia nimpongeze mwenyekiti wa kamati hii kwa umakini wake mkubwa aliouonesha katika Baraza hili leo na wajumbe wake kwa ripoti yao nzuri walioileta hapa Barazani. Kwa kweli ninawashukuru sana kwa ripoti yao nzuri.

Mhe. Spika, mimi ninataka nigusie sehemu mbili au katika wizara mbili; Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum vya SMZ.

Lakini Mhe. Spika, nianze kwanza kuhusu suala la Mahakama. Na ninataka nianzie kwa Mahakama iliyokuwepo Makunduchi. Mhe. Spika, Mahakama hii iliyokuwepo Makunduchi hali yake ni mbaya, kwa kweli ninaweza kusema hata haiwezi kufanyiwa kazi kwa sasa. Sasa iweje leo tunakuta tunahukumu watu wanakuja na kesi mbali mbali wakati Mahakama ile haipo katika mazingira mazuri ya kufanyia kazi kwa binadamu.

Lakini tujiulize hawa wanaohukumiwa kweli watakuwa na imani na ile Mahakama ile Mhe.Spika. Tukiacha na Mahakama ile ya Makunduchi tuje kwenye Mahakama nyengine zote zilizokuwepo hapa Zanzibar. Wajumbe wengi wamechangia suala hili la rushwa. Mimi sitaki sana kuchangia sana suala la rushwa, lakini niseme tu kidogo Mhe. Spika, suala hili linazidi siku baada ya siku. Ninaweza kusema katika miaka hii rushwa kupita kiasi, imekuwa kama biashara sasa hivi.

Mhe.Spika, tukichukua mfano mdogo juzi juzi Mhe. Waziri, alisema hapa zimekamatwa karibu kilo 30 za unga *heroin,* lakini cha ajabu hatumjui aliyekamatwa unga nani. Mhe. Hamza Hassan Juma, alisema jana hapa kwa nini asijulikane huyu mletaji bidhaa hizi akapata adhabu ikawa fundisho kwa wale wengine ambao wanaotaka suala hili hapa au biashara hii haramu ya madawa ya kulevya.(*Makofi*).

Mhe. Spika, baada ya kuacha hapo, sasa ninataka kidogo niingie kwenye kisiwa chetu cha Pemba. Mimi nimepata bahati mara tatu au nne kwenda Pemba kutembea hasa kwenye kamati zinapotokea kufanya kazi kule na kuona hali ya Pemba hali halisi ilivyo. Mhe. Spika, ninaweza kusema wenzetu wa Pemba wapo katika hali mbaya na sijui muda wote huu tunakuwepo wapi kuwasaidia wenzetu ili kuweza kufanya kazi vizuri kwenye mawizara na idara.(*Makofi*).

Mimi nianzie kwenye suala la bajeti Mhe. Spika, ninakumbuka kila nikenda katika wizara, bajeti zao zinakuwa ni ndogo, hupelekea hata zile kazi zao kuzorota kufanya inakuwa haziwezekani kabisa kwa sababu bajeti yao ni ndogo sana, wanashindwa kukidhi hali yao ya mahitaji. Lakini nitoe mfano mdogo halisi kabisa ambao mwenyewe nimeuona wa kamati yangu tulipokwenda katika Wizara ya Mahakama ya Ardhi ipo katika wizara yetu Mhe. Spika.

Tumekwenda kwenye Mahakama ya Ardhi yule Jaji anazungumza anasema yeye hata gari ya kupanda hana. Ile gari anayoitumia yule Jaji wa hapo, spana mkononi. Kwa kweli inatia huzuni sana Mhe. Spika, bajeti zao ni ndogo sana. Naomba Mhe.Waziri, aziangalie vizuri bajeti hasa upande wa Pemba kidogo hali zao sio nzuri na mambo yanakwenda vibaya sana kwa hali yao wanayokuwa nayo.

Lakini nije kwenye mfano mwengine Mhe. Spika, Jaji Mkuu wetu wa Zanzibar, ninasikitika sana akenda Pemba hata ile gari ya kuja kumpokea inakuwa haipo. Lakini ukifuatilia na ukiuliza unaambiwa hakuna gari ya kuja kumpokea Mhe. Jaji Mkuu, baada ya gari yake moja ile hakuna gari nyengine. Kwa hivyo, naomba Mhe. Spika, suala hili liangaliwe, kwa sababu Jaji Mkuu ni kiongozi mkubwa katika nchi yetu, ni lazima apewe heshima ya hali ya juu, kwa sababu ni muhimili mkuu katika nchi yetu hii, kwa hivyo naomba atakapokwenda Pemba Mhe. Jaji Mkuu awe na gari angalau zisipungue tano ziweze kumpokea.

Mhe. Spika, vile vile suala la usafiri wa Jaji Mkuu, naomba gari japo moja itoke Unguja iende kule wawe nayo kule, angalau wasaidiwe hawa wenzetu wa Pemba ili waweze kufanya shughuli zao kwa vizuri kabisa. Atakapokuja Waziri wetu kufanya majumuisho, naomba aniambie suala hili linakuwa vipi hata Jaji Mkuu hawezi kupokelewa na gari nyengine zaidi yake yeye. Kwa hivyo, naomba ufafanuzi kwa suala la gari Mhe. Spika.

Mhe. Spika, katika kutembea kwangu Pemba na kamati yangu nilipata kutembelea hii mahakama ya Kengeja Pemba, kwa kweli inasikitisha sana Mhe. Spika. Hawa wafanyakazi wa mahakama yetu ya Kengeja hata posho

hawapati, kama makarani wanashindwa hata kukidhi mahitaji yao madogo madogo, sasa kwa nini hawa wafanyakazi wetu hawapatiwi posho la kuweza kutimiza mahitajio yao. Kama ninavyojua wenzetu wa Pemba maisha yao yako duni sana Mhe. Spika, kama hawajapata posho basi sidhani kama wanaweza kufanya hizo kazi zao kwa ufanisi mkubwa, hasa kazi hizi za mahakama ni kazi kubwa za kuwahukumu watu na kuwafunga. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anipe ufafanuzi kwa nini hawapati posho zao kwa wakati hawa wafanyakazi wetu wanaofanya kazi Pemba.

Mhe. Spika, suala jengine kwa wafanyakazi wetu wa mahakama ni miezi 14 hivi sasa kutolipwa mishahara mipya wakati miongozo ilikwishatolewa katika Baraza la Wawakilishi na Mhe. Waziri ulitaka walipwe. Kwa hivyo, naomba ufafanuzi zaidi kwa hawa wenzetu mishahara mipya walikuwa waongezewe lakini mpaka leo hawajaongezewa, sijui inakuwa vipi mpaka leo wanapata mishahara ile ile ya zamani, kwa kweli inakuwa haiwatoshi, malalamiko yanakuwa makubwa na hakuna kinachokidhi kwa maisha ya sasa hivi.

Mhe. Spika, vile vile suala la walinzi wa mahakama wana shida sana kulinda zile mahakama kwa vile hawapati posho na wao, hata posho la muda wa ziada wa kazi hawapati. Kwa hivyo, Mhe. Waziri suala hili naomba uniambie na ufafanuzi mzuri unipe.

Mhe. Spika, kwenye mahakama hii ya Kengeja kwenye upande wa vifaa, hata mtu akija kuandika ripoti pale, lile *file* la kuandikia ripoti halipo, sasa sijui mahakama hii itakuwa inaendesha vipi Mhe. Spika, kwa kweli bora ingefungwa au ingekuwa haipo tungejua, lakini iwe hakuna *file* halafu analetwa mtuhumiwa pale hakuna kinachoweza kuandikwa inakuwa haileti sura nzuri.

Vile vile Mhe. Spika, nije kwenye Wizara ya Nchi (OR)Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ. Kwanza nimpongeze sana Waziri Mhe. Haji Omar Kheri kwa umakini wake mkubwa na kwa kujitahidi sana katika kipindi kifupi cha kuchaguliwa kuwa waziri wa wizara hii, lakini juhudi zake zinaonekana, nampongeza sana.

Pia niwapongeze sana hawa ndugu zetu wa KMKM kikosi maalum cha kuzuia magendo. Mhe. Spika, hawa vijana wetu wanafanya kazi sana na wanajitolea bila ya kujali muda wao na wakati wao, lakini Mhe. Spika, inasikitisha sana hawa vijana wetu, katika bajeti ya maendeleo ya mwaka katika hiki kikosi cha KMKM cha magendo hakikuwepo kwenye bajeti. Sasa Mhe. Spika, naomba kuuliza kuhusu hili suala la hawa askari wetu kwa nini wasitiwe kwenye bajeti wakati wana kazi kubwa? Mfano mzuri tu Mhe. Spika, hawa askari wetu wa KMKM tuwapongeze sana kwa juhudi kubwa

walizoonesha wa kujenga ile hospitali kwa nguvu zao wenyewe na zaidi kwa kujitolea. Mimi nawapongeza sana kwa sababu ile hospitali Bububu imetusaidia sana, badala ya kuja mjini lakini sasa hivi tunaishia pale kwenye ile hospitali na kuweza kupata huduma nzuri.

Vile vile niwapongeze na madaktari wote wa KMKM kwa taaluma zao nzuri na kwa kujitolea na kupata sifa nzuri pia kwa wananchi, lakini naomba serikali iwachukue hawa askari wetu na kuwapeleka nje kwa ajili ya taaluma zaidi ya kidaktari, ili wapate ujuzi zaidi hawa vijana wetu na waweze kutusaidia.

Mhe. Spika, kama tunavyojua lile jengo la hospitali bado halijakamilika, hivi sasa kuna vitu vingi bado havijapatikana. Kuna *ICU* bado, *theatre ward* bado, wodi ya wazazi haijakamilika vizuri Mhe. Spika, na sehemu ya meno ipo lakini haijakamilika vizuri.

Mhe. Spika, serikali ni lazima iwaingizie bajeti hivi vikosi vyetu vya SMZ, kwa sababu wanajitahidi sana. Mimi mwenyewe nilipoona juhudi zao basi niliwapa jenereta moja la kutumia hospitali pale. Vile vile sasa hivi wanayo *ambulance* pale nimejitolea kwa ajili ya wananchi pamoja na huduma za pale zifanyike vizuri. *Ambulance* ile wanayo na tunaitumia kwa mashirikiano na wananchi wote. Kwa hivyo, nawashukuru sana, lakini naomba na serikali itie mkono wake zaidi.

Mhe. Spika, kama tunavyojua hivi juzi alikuja Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuzindua hospitali ile Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete. Namshukuru sana na alitoa ahadi nyingi sana za kutusaidia pale hospitali, kwani vifaa vingi vile ni vya gharama kubwa na kwa kweli sisi wenyewe tutakuwa hatuwezi kuvinunua, lakini kwa kushirikiana na Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Zanzibar na sisi viongozi, pamoja na kikosi cha KMKM basi tutaweza kupata vifaa hivi ambavyo vitasaidia sana wananchi wetu hasa wa Jimbo la Bububu na wananchi wa sehemu mbali mbali wanaweza kufaidika na hospitali hii.

Pia Mhe. Spika, bado kuna changamoto nyingi sana, zikiwemo *X-Ray machine*, vitanda, *ultrasound* na majiko hayo yote bado. Kwa hivyo, nilikuwa naomba Mhe. Spika, suala hili alitilie mkazo Mhe. Waziri ili tupate ruzuku au ile bajeti ya maendeleo tuweze kutiliwa kila mwaka kwa ajili ya askari wetu wa KMKM, kwa sababu wanaangalia maslahi ya wananchi wote wa Zanzibar, kama unavyojua hospitali hii sasa hivi ni kubwa kwa Zanzibar na wananchi wengi wanakuja hapa kwa ajili ya matibabu.Hata ukienda pale saa za asubuhi kwa kweli Mhe. Spika, utaona huruma watu wanakaa mpaka nje na mpaka wanapigwa na jua, watoto na wajawazito wanapata tabu sana. Hata hiki kikosi

chetu cha KMKM wameamua kujenga sasa hivi kipaa pale ili kuongeza ile hospitali iweze kuwa na huduma nzuri.

Mhe. Spika, pia hii hospitali hata kukamilika bado kunahitajika karibu milioni 800, lakini milioni hizo 800 hata ukitizama sio nyingi, lakini zikipatikana fedha hizi basi ile hospitali itakuwa nzuri kabisa, itakuwa ni ya maana kwa Zanzibar na itasaidia mzigo wa Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Vile vile Mhe. Spika, kwa masikitiko makubwa nijiulize hii Hospitali ya KMKM Kibweni, kwa nini isipewe dawa kutoka Wizara ya Afya. Huu mwaka wa tano Hospitali hii haijawahi kupewa dawa hata siku moja, ya kusaidiwa kutoka Wizara ya Afya. Namuomba Mhe. Waziri akija anifafanulie kwa nini hatupewi dawa kutoka Wizara ya Afya, anisaidie suala hili nijue ili tuweze kupunguza huu mzigo au kuna tatizo gani tupate kujua.

Mhe. Spika, nije kwenye suala la ndugu zetu wa KMKM ambapo wenzetu hawa ni muhimu sana na wanatusaidia kwenye masuala mengi hasa ya uokozi, lakini nasema wana changamoto nyingi, wako tayari kufanya kazi lakini vifaa hawana, hasa hivi vifaa vya kuokolea watu. Mfano kuna vifaa vya kuokolea watu kama *wear suit* wanazo lakini ni kidogo havitoshi kabisa, kuna boti za uokozi hawana, *speed boat* pia hawana Mhe. Spika. Naomba serikali iwaangalie kwa jicho la huruma hawa vijana wetu, kwani wanajitahidi sana kwa kazi hizi za uokozi na mambo mengine ya magendo na kwa kila kitu hawa vijana wetu wako makini sana.

Vile vile Mhe. Spika, vifaa vya mawasiliano kama *radio call* hakuna vya kutosha kwa ajili ya mawasiliano, endapo ikitokezea dharura yoyote kama wakihitajika, hivyo naomba na hizi *radio call* wazipate hao vijana wetu.

Mhe. Spika, katika kitengo cha uokozi,

Mhe. Spika: Unazo dakika tano.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Ahsante Mhe. Spika, namalizia dakika mbili tu. Mhe. Spika, kitengo hiki cha KMKM kinahitaji usafiri, kunapotokezea vurugu pahala basi Mhe. Spika, inakuwa hata kuweza kufika kwenye tukio inakuwa inachukua muda kwa sababu usafiri hawana. Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Spika, hata kwa mkopo hawa ndugu zetu wa KMKM wapewe, wanunuliwe gari, wanaweza kulipa kidogodogo hawajataka bure. Maana yake mtu ukisaidiwa na wewe ujisaidie kidogo. Kwa hivyo, wanataka hata mkopo nafuu wapewe ili waweze kununua japo gari na waweze kufika katika matukio pakitokea vurugu au pakitokea chochote basi waweze kufika kwa haraka sana.

Mhe. Spika, pia naiomba serikali iwaingizie bajeti ya maendeleo hawa ndugu zetu wa KMKM. Mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Bububu tunaunga mkono ripoti hii kwa asilimia 101. Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi).*

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Spika, awali ya yote na mimi nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Subuhanahu Wataalla, kwa kutujaalia jioni hii kuwepo katika Baraza letu kwa ajili ya kutekeleza majukumu yetu ya kitaifa.

Pia nachukua nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia machache katika ripoti ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Vile vile na mimi nisiwe mchache wa fadhila, nimpongeze sana Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa namna alivyowasilisha waraka wake kwa umahiri na kwa umakini kabisa.Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo na mimi nianze mchango wangu kwenye mahakama zetu za Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa kweli ni masikitiko makubwa kama walivyosikitika baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe katika michango yao juu ya ucheleweshaji wa haki za wale wanaopelekwa mahakamani kwa muda marefu.

Mhe. Spika, suala hili linasikitisha sana. Kwa nini ziwe kesi zinasuasua namna hii. Mhe. Spika, nikinukuu ukurasa wa 31 katika kitabu cha ripoti za kamati za kudumu kuna maelezo yanasema hivi;

"Kesi zilizofunguliwa katika baadhi ya mahakama zikiwemo na za kipindi cha Oktoba - Disemba".

Mhe. Spika, hili ni jambo la kusikitisha sana maelezo yanaeleza kwamba Mahakama ya Rufaa kuna kesi tano, lakini zilizopatiwa ufumbuzi ni kesi mbili, Mahakama Kuu kesi 40 lakini zilizopatiwa ufumbuzi ni kesi 2, mahakama ya mkoa wa Mjini kesi 203, Mahakama ya Mkoa Mwera kesi 71 kuna kesi moja tu ndio iliyopatiwa ufumbuzi. Mfenesini kuna kesi 14 hakuna hata moja iliyopatiwa ufumbuzi kwa maelezo kwamba Jaji wa mahakama hii ana likizo.

Mhe. Spika, kwa kweli hili ni tatizo na ni tatizo kubwa na la kitaifa. Kwa hivyo, tunamshauri sana Mhe. Waziri suala hili aliangalie ili kila mwenye haki apewe haki yake, kushtakiwa sio tatizo, tatizo ni kurundikana kesi kwa muda mrefu bila ya kutolewa maamuzi.

Mhe. Spika, nikienda katika ukurasa wa 32, kuna maoni na maagizo ya Kamati. Mhe. Spika, nitanukuu maoni nambari mbili;

"Kamati imesikitishwa sana na maelezo iliyopata katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, kuhusiana na tetesi kuwa baadhi ya mahakama zetu kwa kupitia majaji ambao uteuzi wao ulileta mtafaruku mkubwa, kutoka katika chama cha wanasheria Zanzibar, ambao walitoa waraka kwa Mhe. Rais kwa kupitia uteuzi wao kutokana na sababu mbali mbali, zikiwemo za ulaji wa rushwa, uwezo mdogo wa nafasi walizokabidhiwa na mengine".

Mhe. Spika, rushwa itatuua hapa Zanzibar. Kwa kweli nampa pole sana Mkurugenzi Mkuu aliyeteuliwa hivi karibuni, wa kusimamia taasisi hii ya kuzuia rushwa na uhujumu uchumi, kwa sababu rushwa hivi sasa inaonekana kama ni haki. Rushwa jamani ni adui wa maendeleo, ni adui wa maisha na ni adui wa Zanzibar. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri kwa maoni haya ya kamati nambari mbili, na nitasoma tena maoni nambari tatu, haya ayaangalie kwa kina na atupe maelezo, kwa nini kuna usemi huu ambao umezungumzwa wa kutokana na chama cha wanasheria Zanzibar.

Mhe. Spika, kuna kero nambari tatu inasema hivi hapo katikati mwisho;

"Hali hiyo inatokana na uhalisia uliopo wa sheria ya ushahidi iliyopitishwa mwaka 1917 kupitwa na wakati".

Mhe. Spika, tunaomba suala hili lifanyiwe marekebisho ili sheria ziendane na wakati tulionao.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo niende katika Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana katika ukurasa wa 36. Mhe. Spika, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana imekabiliwa na changamoto nyingi, miongoni mwa changamoto hizo zinazema hivi;

Kamati ilielezwa kuwa Kamisheni ya Wakfu inakabiliwa na changamoto ya baadhi ya wananchi kutofahamu maana halisi ya mali za wakfu, jambo ambalo husababisha migogoro katika baadhi ya familia.

Mhe. Spika, hapa niiombe Kamisheni ya Wakfu itoe elimu kwa wananchi, ili kusiwe na mgongano kati ya mali ya wakfu na mali za watu ambao hawakuweka wakfu.

Mhe. Spika, nikiendelea na changamoto ya pili inaeleza kamati ilivyofanya ziara kisiwani Pemba. Ilielezwa kuwa mashamba mengi ya wakfu yamechukuliwa na Wizara ya Kilimo na Maliasili. Kwa mfano shamba la Mgagadu limechukuliwa na hadi kamati ilipotembelea ilipewa taarifa kuwa kesi hiyo ipo kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, nafikiri mali zote za wakfu zina nyaraka zake, kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri pamoja na kwamba kesi hii ipo kwa Makamu wa Pili wa Rais, lakini ifuatiliwe ili shamba hili lirudi katika wakfu na litekelezewe yale ambayo yamewekwa na yule mwekaji wa shamba hili katika wakfu.

Mhe. Spika, kwa kweli inasikitisha sana kwamba mashamba ya wakfu yanachukuliwa na wizara za serikali. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri suala hili alifanyie kazi ipasavyo, ili shamba hili lirudi katika Kamisheni ya Wakfu na vile vile liweze kutoa huduma zile ambazo zimekusudiwa na wawekaji wa wakfu wa shamba lile.

Mhe. Spika, nikitoka hapo niende katika Wizara ya Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma, katika ukurasa wa 51.

Mhe. Spika, Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Kitaifa. Suala hili limezungumziwa na Wajumbe wengi sana, kwa sababu kuna mambo ambayo yanaumiza na yanasikitisha. Mimi nazungumza kwa mujibu wa kitabu hiki katika ukurasa wa 52. Kamati imeoneshwa nyumba ya kuishi iliopo ndani ya eneo la Idara ya Nyaraka, uwepo wa nyumba hiyo unahatarisha usalama wa eneo hilo, ambalo kutokana na unyeti wake linatakiwa liwe linahifadhiwa katika viwango vikubwa vya usalama.

Mhe. Spika, inasikitisha sana kwamba nyumba hii ya raia ambayo ipo karibu na ofisi ya idara hii ipo muda mrefu na nafikiri imeshalalamikiwa katika kipindi kirefu kilichopita, ni kwa nini mpaka leo nyumba hii inadumu kuwepo? Mhe. Spika, baada ya wizara kuonana na muhusika wa nyumba hii na kumpangia eneo jengine la kukaa na kumlipa fidia kwa mujibu wa nyumba yake. Mhe. Spika, nyumba ile inaendelea kuwepo, na leo tunasikia kwamba nyaraka zinaibiwa, kuna kitu hiki na hiki. Wafanyakazi ofisi yao haitoshelezi, kwa nini mpaka leo nyumba hii inaendelea kuwepo? Hili ni jambo la kawaida tu. Serikali haishindwi kabisa kuonana na mwenye nyumba hii na baadae kumtafutia eneo jengine ili aweze kuondoka katika eneo lile, watu wa Idara ya Nyaraka wapate eneo lao kwa vizuri na kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Spika, nikiendelea na Idara hii ya Nyaraka nizungumzie kuhusu ukosefu wa wataalamu wa lugha mbali mbali. Mhe. Spika, kwa kuwa zile ni nyaraka za kitaifa, basi kutakuwa kuna nyaraka za lugha mbali mbali, mpaka leo serikali imeshindwa kuwaajiri watu wenye uwezo wa kuzungumza lugha mbali mbali ili wanapofika wageni au hata sisi wenyewe kuzijua nyaraka zile kwa mujibu wa lugha zilizoandikwa. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri suala hili alifanyie kazi, ili watakaofika pale watoshelezwe kwa mujibu wa lugha yoyote ile ambayo imeandikwa katika waraka uliohusika.

Mhe. Spika, niendelee na maoni ya maagizo ya Kamati. Maoni ya kwanza ya kamati yanasema hivi, katika ukurasa 53. Kwa kuwa changamoto hizo ni za muda mrefu, na kwa kuwa kamati mbali mbali zimeshapita na kukuta baadhi ya changamoto hizo hizo zilikuwepo na mpaka sasa zipo. Kamati hii inaiagiza wizara. Ninachokizungumza hapa ni kwamba hili neno kamati hii inaiagiza basi limeandikwa kwa herufi kubwa, maana yake ni kwamba kamati hii inasisitiza sana kwamba wizara ichukue hatua juu ya changamoto mbali mbali ambazo zinaonekana katika idara hii.

Mwisho Mhe. Spika, niiombe wizara na nikuombe wewe Mhe. Spika, kama maoni yalivyotolewa na baadhi ya Wajumbe kwamba iundwe Kamati Teule, ili kuchunguza mapungufu yaliyojitokeza katika suala zima hili la kuibiwa nyaraka. Naomba suala hili lifanywe, kwa sababu kufanya hivyo ni kukidhi haja ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wananchi wa Zanzibar.

Kwa hayo machache naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi jioni hii kupata nafasi ya kutoa maoni yangu machache juu ya ripoti hizi ziliopo mbele yetu.

Mhe. Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwepo hapa tukiwa wazima, hatimaye niwapongeze mawaziri wawili waliowasilisha ripoti zao hapa. Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ na Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria ambaye ametokezewa na mkasa, nimuombee dua Mwenyezi Mungu amlinde kwa hili na jengine lolote. Kasalimika kwenye gari ya ng'ombe na kwenye ndege, Mwenyezi Mungu amzidishie kumuokoa.

Mhe. Spika, pongezi pekee za dhati zaidi zimuendee Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala, Mwanasheria Ussi Jecha Simai. Huyu ni mwanasheria chipukizi na leo katuonesha kuwa kweli yeye ni mwanasheria. Kwa hivyo, nampa pongezi zangu za dhati na aendelee kuwa muadilifu na mfuatiliaji wa kazi katika kamati yake yoyote aliyopangiwa kuiongoza.

Mhe. Spika, mimi nitaanza mchango wangu kwa (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Nitaanza na Baraza la Manispaa.

Mhe. Spika, pamoja na jitihada nyingi Baraza hili inayochukua kuweka mji wa Zanzibar kuwa ni safi, lakini bado ile harufu ya kuwa unaingia mjini ipo.

Kwa sababu mji wetu una sifa moja, sisi ambao tunatoka Chukwani, tunapoteremka daladala pale ambapo tumepangiwa tuteremke kwa kusumbuliwa, basi ukisogea kidogo unapata harufu mbaya, kwa hivyo najua kwa sasa naingia mjini.

Kwa hivyo, cha kusikitisha ni kwamba ukiingia mjini unasikia harufu mbaya isiyopendeza na ukitoka unasikia harufu njema. Kwa hivyo, ishara ya kuingia katika mji wa Zanzibar ni kupata harufu isiyopendeza. Suala hili ningemuomba Mhe. Waziri aendelee kupigana nalo ili mji upate hadhi yake ya mji, mji uwe tofauti na choo.

Mhe. Spika, Baraza la Manispaa kazi iliyofanya ya kusambaratisha daladala pale Darajani, hata kama ni zuri kiasi gani, lakini inaleta usumbufu na inaendelea kuleta usumbufu kwa wasafiri wanaotoka na kuingia katika mji wetu. Nadhani serikali ilikuwa haijajitayarisha, niseme kama ilikurupuka tu kuwafukuza watu pale waondoke, serikali kwanza ingejipanga. Leo mtu anakwenda bandarini anatokea njia hii ya Chukwani, anakwenda kupanda gari katika Baraza la Wawakilishi la zamani, ana twika zake anakwenda kule. Kwa kweli hapa serikali haikuwafikiria wananchi wake, kwa sababu haikujipanga iliamua tu. Ingekuwa vyema serikali kwanza ingetafuta hivi vituo vikae wapi. Halafu kituo chengine kiliopo baada ya Ofisi Kuu ya CCM pale, kuna msongamano mkubwa sana wa magari, tena msongamano uliokuwa mbaya sana, kwa sababu daladala nyingi zinaingia sehemu ile. Kama ilifanywa kuwa watu wasisongamane pale Darajani waende kule ni sawa, lakini kama lengo ni kuondoa msongamano basi kule umefanywa msongamano ambao ni mbaya zaidi, kwa sababu watu wanasongamana na halafu wanakwenda masafa marefu kufikia pale wanapohitajia.

Mhe. Spika, ile kauli aliyotuambia Mhe. Waziri kuwa gari itateremsha pale halafu iondoke sio ya kweli, kwa sababu gari haiji Darajani ikateremsha. Mimi napanda daladala sana nateremshwa Baraza kongwe la Wawakilishi na nikaenda Darajani kwa miguu. Kwa hivyo, ile kauli kuwa gari itateremsha halafu iondoke kwa kweli haitekelezwi, daladala zinawateremsha huko huko na halafu watu wanatembea, kitu wanachopata faida watu ni kwamba wanafanya mazoezi ya lazima lakini sio ya hiyari. Hii ndio kazi ya Baraza la Manispaa hivi sasa na matokeo yake yako hivyo.

Mhe. Spika, mimi pamoja na vyovyote vile naweza kutembea, lakini wako waliokuwa hawawezi kutembea, na serikali kwa bahati nzuri kwa upande wa serikali imeamua hivyo.

Mhe. Spika, nije kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani, kwetu Kengeja kuna kwahala kunaitwa kwa Guruwe, huku liko daraja la zamani la kiasili

ambalo hivi sasa ni bovu halipitiki, na hii ni njia wanafunzi wanaotoka kuna kijiji kimoja kinaitwa Mto Mkuu wanapita kuja Skuli Kengeja siku za masika, kwa kweli wanapata usumbufu kwa sababu daraja hili ni bovu. Bajeti ya 2011/2012 ilitajwa kwamba daraja hili limetengewa fedha kwa matengenezo, lakini licha ya kutengewa hata harufu hiyo fedha haikufika kule kwahala sijui hicho kilichotengwa kilienda wapi. Kwa hivyo Mhe. Spika, daraja hili lina umuhimu wake kwa sababu ni njia ambayo si ya gari ni njia ya miguu lakini daraja ni muhimu kwa sababu liko tokea enzi na enzi kuna haja ya kufanyiwa matengenezo ili liweze kupitika.

Mhe. Spika, nije katika Chuo cha Mafunzo na nizungumzie vile vile cha kule Kengeja. Kengeja tunacho Chuo cha Mafunzo na wanayo mashamba makubwa tu ya kulima, lakini Mhe. Spika, kwa kuwa hiki ni chuo wale waliohatiani pengine watakuwa ni wanafunzi na wale askari pengine watakuwa ni walimu. Kwa hivyo chuo hiki kina walimu wengi zaidi kuliko wanafunzi. Sasa nipongeze kwa hilo kwa ule uhalifu kidogo umepungua. Kwa sababu walimu ambao ni askari ni wengi kuliko wanafunzi. Kwa hivyo mashamba haya kwa kweli hayafanyi kazi kikamilifu. Mhe. Spika, kwa kuwa kabla serikali hawajahodhi mashamba haya kuyapeleka kwenye Chuo cha Mafunzo yalikuwa watu wanalima na kuzalisha mpunga, ningeomba mimi sasa kwa kuwa kazi inayofanyika pale ni ndogo kulingana na mashamba yaliyopo, ni vyema hiki chuo pale kikahamishwa na yale mashamba wakarudishiwa wananchi ili waendelee kulima. Nadhani tukifanya hivyo tutakuwa tumewasaidia wale wananchi pale kupata sehemu za kulima.

Halafu nimeambiwa hapa kuwa Chuo cha Mafunzo kiajiri wataalam wa kilimo na mifugo, lakini Mhe, Spika sio wataalamu wa kilimo na mifugo tu kwa sababu chuo hiki kinafanya kazi mbali mbali ikiwemo ya kilimo, ambayo ndio kubwa kuliko zote, mifugo hata ujenzi.

Kwa hivyo waajiri wataalamu wa fani zote hizo kwa sababu kimeletwa chuo ili yule aliyetiwa hatiani pale iwe ana taaluma ya kwenda kufanya kazi ya kuweza kujitegemea. Sasa wafunzwe wanafunzi kazi mbali mbali ili wakifika pale waweze kujitegemea sio kilimo tu, wanafunzwa hata ujenzi hasa hizi Idara Maalum za SMZ kwa ujumla zote zinafanya kazi za ujenzi. Sina hakika kuwa wamejisajili katika bodi husika zinazohusiana na mambo haya au wanajenga kwa sababu wanajua tu kujenga. Ninamuomba Mhe. Waziri anisaidie kwa sababu kujenga nyumba na mambo mengine kunahitaji utaalamu wa kutosha inaweza kuwa utaalamu wa kutosha upo lakini kama ikija ikatokezea ajali ya jengo fulani kuporomoka je hivi vikosi vitaweza kujitetea vipi juu ya majanga ya aina hiyo yakitokezea.

Mhe. Spika, nikizungumzie kikosi cha Zimamoto kiliopo uwanja wa ndege wa Pemba. Kikosi hiki pale ndio ofisini pao, na pale ndio nyumbani pao lakini wanalala kwenye vitanda ambavyo havina godoro juu ya mabao tu ya vitanda vile. Sijui kwa nini wale ni wafanykazi wamekaa kama wanaoadhibiwa badala ya kuwa wanafanya kazi, wamekaa kama ambao wanatiwa adabu, ningeiombaWizara husika iwapatie japo magodoro iwatandikie pale wale ni askari wetu. Mhe. Waziri hili silipangi na yote niliyosema sijayapanga ninazungumza tu, tulikwenda katika kamati hivi juzi tukaingia na kama wamewekewa basi itakuwa ni muda mfupi baada ya kuondoka sisi kamati, lakini hawa kwa kweli wakiamka mbavu zinawauma.

Mhe. Spika, niende kwenye hizi nyongeza za mishahara iliyopita. Mhe. Spika, wafanyakazi wote wa kawaida wanalalama kuwa nyongeza hii hawaijui walivyoongezwa na mimi nilipokuwa nachangia bajeti nilitaka kujua kuwa nyongeza hii imekwenda kwa asilimia ngapi? Lakini Waziri hakutaka kutoa ufafanuzi kama amewaongezea kwa asilimia kadhaa, kumbe ilikuwa nyongeza hii ni ya wakubwa tu, hao wengine walidokezewa dokezewa tu, ndio maana serikali ikakataa kata kata kusema tumeongeza mshahara kwa asilimia fulani.

Mhe. Spika, mwendo huu wa serikali wa mara hii kwa kweli haukuwa mzuri. Kuna wafanyakazi ambao ni wa muda mrefu karibu watastaafu zaidi walimu *scheme of service* yao haijawa tayari, leo mwalimu wa miaka 30 na mwalimu aliyeajiriwa miaka 2 nyuma pengine uhusiano wao wa maslahi ni mdogo tu, ningeiomba serikali iwaonee huruma watumishi wake, iwatononoshe ili na wao wajihisi kuwa wanafanya kazi katika nchi yao. Na kero hizi ndogo ndogo wale ambao nyoyo zao kidogo fupi ndio wanasoma na hatimaye wakaondoka. Mhe. Spika, ili kuwalinda, kuwahifadhi, kuwadhibiti, wasomi wetu, ni vyema tuwape maslahi ambayo kwa kima fulani yatawafanya kuwa wasiwe na haja ya kuondoka. Kama serikali ilivyofanya kudhibiti magendo ya karafuu kwa sababu mtu anayekwenda magendo anakwenda kwa mazoea tu, lakini bei aliyopata ni nzuri. Na wafanyakazi waondoke kwa mazoea tu kuwa hawataki kukaa lakini wasiondoke kwa ajili ya maslahi duni.

Nadhani kwenye dakika tano nimeshatumia nne, naona zimemalizika. Ahsante sana.

Mhe. Marina Joel Thomas: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi kuchangia ripoti hii. Mhe. Spika, ninachukua fursa hii kuwapongeza vikosi maalum vya KMKM, JKU, Mafunzo, Polisi kwa kushiriki kikamilifu katika sherehe za mapinduzi kutimia miaka 50 hongereni sana vikosi.

Nitazungumzia kuhusu suala la mrundiko wa mahabusu. Ripoti ya kamati imeeleza kuna mahabusu 187 ambao wanahitaji mahitaji mbali mbali. Na katika ripoti imeeleza kwamba idadi hii ya mahabusu inapelekea Idara kuwa na mzigo mkubwa wa kuwalisha na kuwahudumia na mahitaji mbali mbali, jambo ambalo Idara inakuwa na bajeti ndogo wakati mahabusu wanaongezeka siku hadi siku. Kwa hivyo ninamuomba Mhe. Waziri iwatengee bajeti ya ziada kwa ajili ya Idara hii ili iweze kuwahudumia vizuri mahabusu hao.

Mhe. Spika, suala zima la utungaji wa kanuni na sheria za utumishi. Kutokana na ripoti ilivyoelezwa inaonekana kwamba kanuni bado hazijatungwa. Kwa hivyo ninakuomba Mhe. Waziri muda uliobaki ni mdogo kutimia bajeti ijayo kwa hivyo ninakuomba hili suala ulifanyie kazi ipasavyo.

Jengine kuna changamoto mbali mbali ambazo zinakabili hivi vikosi vyetu vya Idara Maalum KMKM, JKU, Mafunzo, Valantia ambavyo ikiwemo changamoto ya uchakavu wa mashine, changamoto za kiusalama, suala la mabweni hayo yote Mhe. Waziri tunakuomba kwa moyo wa dhati kabisa uyafanyie kazi, kwa sababu vikosi vina changamoto nyingi. Na ukiangalia tulipokwenda pale *airport* Pemba kama Mhe. Mohammed alivyosema Kikosi cha Zimamoto pale wana changamoto ambayo suala zima la hali ya mazingira kwa kweli hairidhishi.

Mhe. Spika, kuhusu sera ya sheria ya serikali za mitaa hii kila siku, ninakumbuka sijui kama si mwaka wa nne, wa tano huu inazungumzwa, lakini hadi hivi sasa bado tuko katika mazungumzo. Kwa hivyo ninamuomba Mhe.Waziri basi ifanyiwe kazi hii sheria ili kuondoa ule muingiliano wa majukumu. Sasa hivi ukiangalia baadhi ya Wizara au Taasisi zinaingiliana majukumu kutokana na kutokuwepo kwa sheria hii. Kwa hivyo Mhe. Waziri ninakuomba ulifanyie kazi kwa sababu ishakuwa ni siku nyingi, suala hili la Sera ya Sheria ya Serikali za Mitaa.

Suala la wataalamu katika Idara ya Nyaraka, wenzangu wamesema Idara ya Nyaraka ina changamoto nyingi ikiwemo mazingira halisi ya kazi, uchakavu wa vifaa na pia imezungumzia suala la wataalamu wa lugha. Idara ile ni muhimu kwa sababu inatunza nyaraka nzito za serikali na inatembelewa na wageni tofauti wa nchi mbali mbali. Kwa hivyo watengwe hawa wataalamu wa lugha ili iweze kuwasaidia wale wageni ambao waliotoka katika sehemu tofauti na iweze kuwa na hadhi hii Idara ya Nyaraka.

Mhe. Spika, kuhusu halmashauri za Wilaya kuna changamoto kuhusu sheria ambazo zimepitwa na wakati, hii napelekea hata kutoa maamuzi ambayo mengine yanakuwa ni tofauti kutokana na sheria ambazo zipo na adhabu zilizotolewa ni ndogo kuliko hilo kosa lenyewe. Kwa hivyo ina maana sheria

zikifanyiwa marekebisho katika halmashauri za Wilaya itaweza kuwasaidia hata yale maamuzi kutoa katika hali ya uhalisia na uhakika. Na pia suala zima la utaalamu katika halmashauri za Wilaya nalo pia ni changamoto, halmashauri nyingi wataalamu wanakuwa kidogo, kwa hivyo nalo Mhe. Waziri ulifanyie kazi.

Kuna suala zima la ukosefu wa hospitali katika kambi za Ubago, Kengeja na Kangagani na imeelezwa katika ripoti, kambi kama hizi kwa kweli ni muhimu kuwepo na vituo vya afya au hospitali, kwa sababu wanakaa watu wengi na wanahitaji huduma mbali mbali za kiafya. Kwa hivyo Mhe. Waziri na hili nalo lifanyiwe kazi ili ziweze kuwasaidia hawa wanaoishi katika kambi endapo likitokea tatizo lolote waweze kusaidiwa.

Jengine la mwisho Mhe. Spika, kuhusu deni la umeme. Imeelezwa kwenye hii ripoti katika chuo cha mafunzo kuna deni la umeme karibu milioni 98 na katika maelezo imesema deni hili limetokana na askari wastaafu ambao wamestaafu. Kwa hivyo naomba Mhe. Waziri na hili nalo lipate maelezo. Naunga mkono hoja.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana na mimi kunipa fursa jioni hii ya leo kuweza kuchangia mawili matatu juu ya ripoti hizi ambazo zimewasilishwa kwetu. Mhe. Spika, kwanza napenda kuchukua fursa hii vile vile kuwashukuru sana Wizara hizi tatu ambazo zimewasilisha ripoti yake siku ya leo, lakini pia ninawashukuru na kuwapa shukurani za aina yake Kamati ya Sheria na Katiba ikiongozwa na kijana wetu mahiri ndugu yetu Ussi Jecha Mwakilishi wa Jimbo la Chaani pamoja na wana kamati wenziwe ambao wamefanya kazi hii kwa kina na kwa umakini wa hali ya juu kabisa.

Mhe. Spika, mengi yamezungumzwa nisingependa kuchukua fursa hii kurudia rudia yale ambayo yalikuwa yamezungumzwa. Lakini tu nilikuwa napenda kutoa wito kwenye serikali, Mhe. Spika, ningependa kuwaambia viongozi wetu ambao ripoti hii leo imewasilishwa na baadae itakuwa katika himaya zao kwa ajili ya utekelezaji, watengeneze utamaduni wa kufanya tathmini ya kila wakati na muda ambapo kuna matukio na mambo ambayo yanawasilishwa mbele yetu kwa ajili ya utekelezaji. Ningependa tungekuwa na utaratibu huu wa kufanya tathmini ili tujue tulikotoka, tulipo na tunapotaka kutarajia kwenda baadae.

Mhe. Spika, hapa pamezungumzwa katika maeneo mengi kwa Wizara hizi tatu ambazo zilikuwa zimezungumziwa mimi kwa upande wangu ningependa kuingia katika maeneo matatu.

Eneo la kwanza ni katika eneo la Mahkama. Wengi wamelizungumza eneo hili lakini ningeliomba tu mahkama ni kimbilio la wanyonge wote, lakini kwa utaratibu ambao tunakwenda nao kwa sasa hivi wananchi wetu wanapata tabu sana kupata haki zao katika eneo hili la mahkama. Ningeliomba serikali ifanye utaratibu wa makusudi kabisa kuona kwamba yale mambo na malalamiko na kesi ambazo zinawahusu wananchi hususan wanyonge zishughulikiwe na ziweze kwenda kwa mujibu wa taratibu na haki iweze kutendeka kwa mujibu wa sheria.

Jambo jengine ambalo ninaomba kuzungumzia Mhe. Spika, ni suala zima la agizo namba 15. Mhe. Spika, katika agizo namba 15 ambalo linahusu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, hapa palikuwa na ujumbe wa kupatiwa watendaji au wafanyakazi katika maeneo haya kwa ajili ya kuleta ufanisi katika maeneo ya visiwa vyetu vya Pemba na Unguja.

Mhe. Spika, katika ufanisi unaotaka kuletwa katika mamlaka haya na ndio maana serikali ikafikia maamuzi ya kuongeza wafanyakazi, kubwa kwa upande wa Baraza la Mji linahusiana na hali halisi ya usafi wa mji wetu. Mhe. Spika, kusema kweli mimi ninawapongeza sana Baraza la Mji la Unguja na Pemba pamoja na halmashauri zake kwa kazi wanayoifanya kusafisha barabara zetu, ni kazi nzuri na ya kupigiwa mfano. Lakini hapo hapo tuna kazi kubwa sana ya uchafu katika maeneo yetu katika mitaro yetu na misingi yetu hii imekuwa ni kero na kadhia kubwa sana katika mamlaka hizi za miji pamoja na halmashauri zake.

Ningeliomba sana serikali ikae chini na iangalie utaratibu wa kuweza kuondosha kadhia hii ambayo kwa sasa imekuwa kama ni jambo la kawaida. Mhe. Spika, majumba yetu haya ya maendeleo hususan maeneo kwa mfano ya Mtemani, Madungu, Kilimani, Kikwajuni, Michenzani, Gamba na maeneo mengine ambayo mzee wetu Rais wetu Abeid Amani Karume ametujengea majumba ya maendeleo haya, lakini kwa sasa majumba haya kusema kweli hali yake ni ngumu mno Mhe. Spika. Sasa ningeliomba serikali ichukue juhudi za makusudi kabisa kuhakikisha kwamba tunasaidiana kuona kwamba usafi unarudi katika maeneo ya nyumba hizi na kuondokana na maradhi ya maambukizi ambayo wakati wowote yanaweza kujitokeza na watu wetu wakaweza kupata matatizo ya hapa na pale.

Jengine Mhe. Spika, ni haya ambayo wenzetu walikwishaanza kuzungumzia juu ya Taasisi hii ya Nyaraka. Kusema kweli Mhe. Spika, sisi wengine tumeshtushwa tuliposikia taarifa kwamba kuna nyaraka ambazo zilikuwa zimepotea katika mazingira yasiyoeleweka. Hili ni jambo la hatari, ni jambo la kutisha na ni jambo ambalo serikali inatakiwa ikae kitako kuangalia ni namna gani, na ni hatua gani zitachukuliwe kuhakikisha kwamba suala hili

linakomeshwa na wale ambao wanahusika na haya wanachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Spika, baada ya kwisha kuongea katika maeneo hayo sasa nije katika maeneo ya agizo namba 3 ambapo hapa palikuwa panazungumzia suala zima la maaskari hususan katika Chuo cha Mafunzo Pemba kuweza kupatiwa mafunzo. Ningeliomba sana suala hili lisiwe kwa Chuo cha Mafunzo tu Pemba, bali kwa vikosi vyote vya SMZ, vikosi vyote viweze kupatiwa mafunzo na kuweko na utaratibu wa kuangalia juhudi za askari wetu ambao wanajitolea, wanafanya kazi vizuri na baadae waweze kupandishwa vyeo kwa mujibu wa juhudi zao ambazo wanazichukua na tuweze kupata utaratibu mzuri wa kubadilishana madaraka, kila ambapo mkubwa anaondoka yuko mwengine ambaye anaweza kuja kukamata nafasi ile na uwezo wake wa kielimu na ufanisi wa kazi uwe unalingana na uhalisia uliokuwepo.

Baada ya maelekezo hayo kwa vile taarifa hii imekwisha kuchangiwa na watu wengi sana na maagizo yametoka mengi sana, na maoni yametoka mengi sana, nirejee tena kuiomba serikali ikae, izingatie na iyafanyie kazi maagizo haya kwa nia na lengo la kusaidia kuendeleza serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Baada ya hayo ninaunga mkono taarifa hii kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ (Kaimu Waziri wa Kazi na Utumishi wa Umma): Mhe. Spika, awali ya yote kwa dhati kabisa nataka nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha jioni hii ya leo kusimama tena hapa mbele ya kiriri hiki na kutaka kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya mambo machache miongoni mwa mengi ambayo yamezungumzwa.

Pili Mhe. Spika, nikushukuru wewe kwa kunipa fursa hii ya kuweza kutoa ufafanuzi huu. Mhe. Spika, na mimi nataka niungane na Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu ambao wamechangia kwa hisia kubwa sana juu ya mambo ambayo yamejitokeza katika Ripoti ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi ndugu yangu Ussi Jecha Simai ambayo ameiwasilisha leo asubuhi, na Wajumbe wamepata nafasi ya kuweza kuichangia. Na mimi nataka nimpongeze ndugu Ussi Jecha Simai kama Mwenyekiti wa Kamati ameeleza yale ambayo Kamati inatakiwa iyafanye ya kufanya utafiti kwa niaba ya Baraza la Wawakilishi. Na utafiti huo ameufanya kupitia Wizara zetu ambazo tumewasilisha utekelezaji wa Ripoti yetu, kama Wizara zetu zingeweza kumbania au kuibania kamati yake kumpa taarifa baadhi ya mambo ambayo ameyaripoti asingeweza kuyaripoti.

Hiyo ni kusema kwamba serikali na Baraza hili wanazungumza lugha moja; ya kuona kwamba wananchi wa nchi hii wanatumikiwa na wanapata haki zile ambazo serikali na wale waliowatuma wanawashughulikia.

Kwa msingi huo kama nilivyotangulia kusema Waheshimiwa Wajumbe wengine mtanisamehe sana hasa wale mliokuwa mnasema kwamba mnamtaka Waziri aje atoe maelezo.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa utaratibu wetu sidhani kama ninatakiwa nijibu kila kitu ambacho kimezungumzwa hapa. Kwa sababu mimi kama Kaimu Waziri wa Kazi na Utumishi wa Umma nimeeleza yale ambayo niliagizwa na Kamati katika kipindi cha mwaka 2012/13 na leo kuna maagizo mengine ambayo kamati itatupatia, na hayo tunatakiwa tuje tuyaripoti vile vile katika mwaka 2015 katika mwezi wa Aprili iwapo kama hatutokezewa na jambo la dharura kama hili ambalo limetutokezea safari hii, ndio maana tumekuja kuripoti sasa mwezi wa Januari. Kwa sababu tunajua tuna shughuli pevu ya kwenda kwenye Bunge la Katiba ndio maana ratiba yetu imerudi nyuma.

Sasa Mheshimiwa nimshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ameanza kusema mambo manne muhimu ambayo mimi nitayatolea ufafanuzi, na nitakapoyatolea ufafanuzi ina maana na kila Mjumbe ambaye ameyachangia masuala haya basi nitamuomba aridhike badala ya kutaja jina la mtu mmoja mmoja kwa sababu ya wakati.

Jambo la kwanza Mhe. Mwenyekiti wa Kamati alilolizungumzia ni suala la utungaji wa kanuni za Sheria ya Utumishi wa Umma. Na akasema kwamba jambo hili liliahidiwa kwamba litakuja kuwasilishwa Kikao cha Oktoba. Nataka nilithibitishie Baraza lako Tukufu kwamba bado ninakumbuka kwamba mimi mwenyewe nilikuwa nimesema ningewasilisha kwenye Kikao kile cha Oktoba, utekelezaji wa utungaji au uundaji wa Kanuni za Utumishi wa Umma.

Lakini Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ambapo kuna mtu alitaka lazima anyanyuke yeye akasema mpaka bajeti ya mwakani hili jambo lingekuwa tayari, ndio ahadi ambayo ninaikumbuka wakati ule mimi hasa sikuwa nikikaimu bali nilikuwa Waziri muhusika wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Napenda niliarifu rasmi Baraza Tukufu la Wawakilishi kwamba kanuni hizi sasa ziko tayari zimeshapitishwa rasmi, na kazi inayoendelea sasa ni kuzichapisha ili ziweze kufanya kazi kama vile ilivyokusudiwa. Na ieleweke kwamba kanuni hizi hazikucheleweshwa kwa sababu tu, lakini zilihitaji ushiriki wa watu wengi zaidi. Kanuni hizi tofauti na kanuni nyengine zozote kwamba unajifungia waziri na watendaji wako peke yenu mnazimaliza, hapana, zilihitaji ushiriki wa watu wengi zaidi na ndicho kilichosababisha

ucheleweshaji. Lakini hata hivyo, serikali kupitia wizara hii imeweza kuzitunga hizi kanuni na sasa ziko tayari kwa matumizi ya kusaidia sheria ile ya Nam. 2 ya Utumishi wa Umma.

Jambo jengine ambalo limezungumzwa ni suala la wizi wa nyaraka na limezungumzwa kwa hisia kubwa na mimi pia nimelipokea kwa hisia kubwa. Serikali vile vile imelipokea kwa hisia kubwa na sio kwamba imelipokea hapa kama serikali hailijui, serikali inalijua kwamba wizi umefanyika wa nyaraka za serikali zilizokuwa zikitunzwa kwenye nyumba yetu ile ya nyaraka pale Kilimani.

Baada ya kutokea tukio hili serikali ilichukua hatua ya kutafuta chanzo cha wizi wa nyaraka hizi, bahati nzuri serikali vile vile kupitia wizara husika iliwachukulia hatua wale ambao wamehusika na kadhia hii. Kwa upande wake serikali imechukua hatua kwanza za kinidhamu kama watumishi wa umma, lakini pili imechukua hatua za kuwafikisha kwenye vyombo vinavyohusika kwa kosa jengine la jinai la wizi wa hizi nyaraka za serikali.

Ni kweli nyaraka muhimu kama walivyosema baadhi ya Waheshimiwa, Mhe. Salmin Awadh Salmin amesema, Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Ismail Jussa Ladhu na ametaja aina ya nyaraka zenyewe. Jambo hili limetokea na ni kweli kabisa wako watu wanahusika ambao serikali inao mkononi. Na kwa sababu ya kipelelezi narejea tena kusema, isingekuwa rahisi mimi kutoa taarifa ya mambo ambavyo yanaendelea na yalivyokuwa. Lakini wako watu wamekamatwa ambao wameshawishiwa, kwanza walishawishiwa watu pale pale wakakataa bahati mbaya kuna baadhi ya watu wao wakakubali wakaingia kwenye mtego huu.

Kwa hiyo, serikali inalifanyia kazi na ni kweli kabisa Mamlaka ya Kuzuwia Rushwa nayo imelifuatilia hili jambo na inaendelea nalo. Alitakiwa Mheshimiwa anayehusika na masuala ya Mamlaka ya Rushwa atoe taarifa, lakini mimi nadhani sio sahihi kutoa taarifa za uchunguzi wa Mamlaka ya Rushwa hapa sasa hivi. Lakini sisi kama serikali tunalikubali kwamba hili jambo limetokea hatuna sababu ya kulificha, na kwa sababu serikali wenyewe tumeshaanza kulichukulia hatua.

Jambo hili linahusishwa pengine limefanywa kwa makusudi na kutokufungwa kwa mitambo ya *CCTV*. Mimi sidhani kama hivyo ndivyo ilivyo, ukosefu wa kufungwa mitambo ya *CCTV* nakubaliana na Wajumbe wengi waliosema kwamba kuna haja ya kuiangalia bajeti ya taasisi hii na umuhimu wake ili haya matukio yanayotokea yasiweze kutokea tena. Na nakubaliana na wale wote waliozungumzia suala la *CCTV* kwamba lina umuhimu wake katika taasisi kama hii, ambayo pengine ingeweza kutupa uhalisia wa mambo badala

ya kutuhumu na kufikiria mambo. Kama tukio lililotokea juzi Uwanja wa Ndege *CCTV* imesaidia. Kwa hivyo na jambo hili kama ingekuwepo *CCTV* ingesaidia zaidi.

Katika hili Mhe. Spika, tutaendelea kuwasiliana na Wizara ya Fedha kuona kwamba bajeti tuliyoiomba kwa ajili ya *CCTV* inapatikana, ili iweze kufungwa na kuweza kujihakikishia ulinzi zaidi katika eneo hili muhimu sana kwa hatma na maisha ya nchi yetu ya Zanzibar. Na vyanzo vipo, vyanzo vya wizi vipo, serikali imeshaanza kuvijua lakini tuviache vyombo viweze kuendelea na kazi yake.

Suala jengine ambalo limezungumzwa na Mwenyekiti ambalo limeungwa mkono na Waheshimiwa karibu wote waliochangia hapa ni suala la uchambuzi wa matumizi ya fedha za mradi wa *E-Government*. Nakubali kwamba kwa busara zako Mhe. Spika, na busara za Baraza hili tulikubaliana kwamba jambo hili lishughulikiwe na kamati ya kisekta.

Mimi nataka nitoe angalizo kidogo kuhusu unaposema Kamat ya kisekta. Kweli Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ndio kamati ambayo inaisimamia Ofisi ya Rais Kazi na Utumishi wa Umma, lakini kamati hii haisimamii Ofisi ya Fedha na Uchumi ya Zanzibar. Sasa inawezekana pengine Kamati hii ya Kisekta ya Katiba, Sheria na Utawala, sina hakika kama wamepeleka maombi baada ya maamuzi yale kwa Wizara ya Fedha ambayo waziri wake yupo hapa. Lakini ni kweli majibu ambayo yamo kwenye utekelezaji wa maagizo ya Wizara ya Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma, haiwezi kutoa mchanganuo kwa sababu yenyewe sio iliyosimamia mradi.

Sasa kama Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa wakati ule najua iliwahi kupeleka, lakini kwa sasa hivi mimi nadhani kamati za kisekta zinazoweza kufanya kazi jambo hili kupitia Wizara ya Fedha, sisemi kwamba kamati nyengine haiwezi kuhoji suala linalohusu wizara nyengine, lakini ilikuwa kamati *proper* hasa ilikuwa ni Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuihoji Wizara ya Fedha na Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika. Lakini nao Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala waiombe sasa Wizara ya Fedha itoe mchanganuo huu.

Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuwahoji Wizara ya Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma kwenye uendeshaji wa mradi ule wa *E-Government* ni haki yake kabisa kujua *progress* inavyoendelea. Kwa hivyo, mimi ushauri wangu ni kwamba jambo hili huu ni kama ushauri tu wa Wizara ya Kazi na Utumishi wa Umma na yakitakiwa maelezo Mhe. Waziri wa Fedha mwenyewe yupo hapa, kama kweli kuna ugumu wa kuweza kuzipata hizo taarifa au namna gani.Wizara ya Fedha ndio iliyohusika na mradi huu, kwa

hiyo yenyewe ndio inayoweza kuhusika na mchanganuo wa fedha au matumizi ya fedha za mradi huu.

Suala la kuunda kamati teule kwa maeneo yote mawili. Sisi serikali tumefanya katika maeneo tunayostahiki kufanya. Sasa mimi sina uamuzi wa Baraza hili kusema kwamba nakubali au nakataa, hiyo itategemea sasa uongozi wako wewe Mhe. Spika. Kama unakubaliana na hoja hizo sisi kama serikali hatuna tatizo kwa sababu hakuna tunachokificha, kama kuna jambo limefanyika wapo waliohusika watachunguzwa. Sisi kama serikali kwa upande wetu tunaendelea na kazi zetu za kufanya uchunguzi kwa wale tunaowashuku kama wamefanya hivyo. Kama Baraza likihisi nalo linataka liende likafanye kazi hiyo ni maamuzi yako Mhe. Spika, hilo mimi sina tatizo nalo.

Jambo jengine ambalo limezungumzwa na Waheshimiwa wengi, suala la kuwepo kwa wataalamu wa nyaraka nami nadhani nakubaliana nalo kwamba serikali itafanya hiyo kazi ya kuwaajiri wataalamu na kwa sababu sasa hivi ni *right time* ya kuweza kufanya hizo ajira, kwa sababu ajira nadhani tumeanza kuisikia tume imeanza kutangaza. Kwa hivyo, kama taasisi ya nyaraka nayo ilipeleka maombi ya kuajiri watumishi basi itafanywa hivyo na tume itafanya hivyo, kama ikihitajika kuona kwamba wao hawakuwa na hayo maombi, na sidhani kama hawakuwa na maombi.

Katika eneo hili Mhe. Spika, la Kazi na Utumishi wa Umma ningependa nizungumzie maeneo haya matatu makubwa ya muhimu, ambayo ndio wamekuwa yakitawala sana mjadala wetu wa Baraza la Wawakilishi.

Nimpongeze Mhe. Asha Bakati Makame vile vile pale aliposema kwamba kama kuna mambo yanatuhusu mawaziri na watendaji tuambiwe sisi asihusishwe Mhe. Rais, japokuwa yeye ndie mkubwa wetu, mpaka jambo liwe la Rais linakuwa ni jambo kubwa sana.

Mhe. Spika, palizungumzwa pia kuhusu lile suala la *E-Government* na Mhe. Wanu Hafidh Ameir na Mhe. Ismail Jussa na wengine, kuhusu mafanikio au utekelezaji wa mradi wa *E-Government*, hivyo kweli huu mradi unafanya kazi? Nataka nilithibitishie Baraza lako tukufu kwamba mradi huu tayari unafanya kazi. Taasisi nne zimeshaunganishwa na zinatumia mtandao wa *E-Government* kwa maana ya huu mkonga wa taifa.

Taasisi hizo ni pamoja na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara ya Fedha, *ZRB* na Idara ya Vitambulisho. Taasisi zote 86 kwa upande wa Unguja zimeshafikishiwa ule mkonga karibu na maeneo yao ili waweze kununua vifaa wafunge na waweze kutumia mkonga huu. Jukumu la kununua hivi

vifaa viwili *switch* pamoja na *firewall* ni jukumu la kila taasisi, taasisi nne zimeshanunua hivi vifaa na ziko tayari kuunganishiwa huu mkonga wa taifa ili waweze kupata huduma hiyo.

Taasisi hizo Baraza la Wawakilishi limeshanunua na saa yoyote kuanzia sasa itaunganishwa ili iweze kufaidika na huduma hii, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Wizara ya Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma pamoja na Kamisheni ya Utalii. Kati ya taasisi zilizopitishiwa mkonga huu taasisi 86 tayari taasisi 77 zimekamilishiwa utaratibu kulingana na makubaliano yetu na Kampuni ya *ZANTEL* ambazo ni sawa sawa na asilimia 90 ya taasisi hizo, na taasisi tisa bado hazijafikishiwa huduma hizi kupitia makubaliano yetu na *ZANTEL* sawa na asilimia 10.

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe suala la mkonga wa taifa na matumizi ya serikali mtandao kwa maana ya *E-Government,* tayari limeanza kufanya kazi na tunatoa wito kwamba wizara na taasisi nyengine zifanye hima ili ziweze kutumia huduma hii.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo nataka nikubaliane na michango mingi ambayo imetolewa inayohusu Wizara ya Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma. Kwa yale ambayo sikuyatolea ufafanuzi nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wasubiri katika utekelezaji wa bajeti ama wasubiri katika utekelezaji wa yale maagizo ambayo kamati imetupa, vyenginevyo yote yale nikianza kuyatolea ufafanuzi narejea kusema yale yale niliyoyasema jana itakuwa tunafanya *duplication* ya mambo. Sasa kwa niaba ya Waziri wa Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma naomba niwasilishe hayo. Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunisikiliza.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena nataka nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuja kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya mambo machache sana ambayo yamezungumzwa hapa na nitumie *style* ile ile kwamba mambo mengi yaliyozungumzwa hapa mengine kikanuni nisingetakiwa niyaseme. Kwa sababu haijafika hata miezi mitatu mengine nimeyatolea majibu kwenye maswali na majibu ya Baraza la Wawakilishi, lakini leo hapa yamejitokeza tena.

Waheshimiwa Wajumbe mtanisamehe sana katika hilo, nisingependa mimi kuwa wa mwanzo kuvunja kanuni za Baraza hili. Sasa kama wanataka majibu ya hayo mengine wanisubiri baada ya miezi mitatu waniulize maswali nitawajibu.

Mhe. Spika, nimshukuru tena Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na kamati yake kwa jumla, lakini niwashukuru na niwapongeze sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kutoa maoni yao kuhusu mambo mengi ambayo yamejitokeza katika hoja mbali mbali za wajumbe.

Jambo la kwanza ambalo limejitokeza leo na ambalo limezungumzwa na wajumbe kama kawaida yangu sitaki kuwataja wale waliochangia, ni suala la maslahi ya vikosi na wapiganaji. Nataka niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kulizungumza hili na kuniunga mkono katika juhudi zangu za kutaka maslahi ya wapiganaji wetu katika vikosi vya SMZ yazingatiwe. Wengine wamesema kwamba nimepita sehemu zote, ni kweli, hakuna eneo lolote lile la wapiganaji wa SMZ ambalo mimi sikufika, na nimesikia mengi kama walivyosema na hayo yote walioyasema mimi nimeambiwa na hatimae nimeandika taarifa kupeleka serikalini juu ya hatua ambazo nyengine zitafuata kiutekelezaji.

Lakini nataka niseme kwamba hata mazingatio ya maslahi ya watumishi yalipozingatiwa mwaka huu basi na maslahi ya wapiganaji pia yamezingatiwa kwa uwezo uliopo wa serikali. Hata hivyo, serikali itafanya juhudi ya kuhakikisha kwamba maslahi ya askari wetu yanaongezeka siku hadi siku pale uwezo wa kifedha unapokuwa unaruhusu.

Mhe. Spika, mazingira wanayoishi askari ni kweli nataka nikubaliane nao, lakini ziko juhudi mbali mbali ambazo Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ inazifanya hivi sasa kwa ajili ya kukabiliana na changamoto hizo. Naomba wanipe muda kidogo nitakapokuja kwenye bajeti nitaelezea tumefikia wapi katika changamoto hizo.

Jengine tunazipokea pongezi ambazo kila mjumbe ametupa ambazo zimetoka kwa askari wetu wa Idara Maalum ambao wako kwenye vikosi mbali mbali kwa kufanikisha Sherehe za Mapinduzi ya Zanzibar kutimia miaka 50. Tunazipokea pongezi na nitazifikisha salamu hizi na baadhi ya makamanda wapo juu pale wananisikia, pengine mimi kabla sijakutana nao wapiganaji hao salamu hizi watazifikisha.

Mhe. Spika, limezungumzwa suala la Askari wa SMZ kupiga watu. Nataka niseme hili nimelisikia sasa na nitajaribu kulifanyia utafiti na serikali haijawaweka askari kwa madhumuni haya ya kuwapiga watu kama imetokezea ni bahati mbaya. Lakini hata hivyo, ninalichukua ili niende nikalifanyie kazi tukio lenyewe lilivyokuwa, mana ndio kwanza nimelipata hapa.

Jengine Mhe. Spika, askari kufanya vitendo viovu limezungumziwa, lile suala alilolizungumza Mhe. Salmin Awadh la Jimbo lake la Magomeni. Kama nilivyosema hili tunaendelea kulifanyia kazi, nadhani tutapata hatma ya jibu lilivyo.

Jambo jengine ambalo limejitokeza katika mjadala huu ni suala la uchafu wa miji na wengine wamejaribu kutoa mifano, kwamba wanapotoka eneo fulani wakifika mjini wanaanza kusikia harufu na uvundo. Lakini nataka niseme miji haijichafui yenyewe, miji inachafuliwa na sisi tunaoitumia. Sasa la kwanza katika hili lazima tukubali Wazanzibari turudi katika desturi yetu ya kuimarisha usafi. Tubadili tabia tuliyonayo sasa, tusipobadili tabia hata ashushwe malaika kutoka mbinguni miji hii haiwezi kuwa safi.

Tuwe na tabia kila mwenye nyumba yake akerwe na uchafu ulioko mbele ya nyumba yake, kila mwenye nyumba yake ambayo ina mashimo ya maji machafu basi yanapotoka maji yale machafu akubali kuyasafisha badala ya kusubiri watu wa Baraza la Manispaa waje wamsafishie. Bila shaka anaweza akenda katika taasisi yenye zana za kusafishia. Sasa utamaduni huo tumeuacha na kama tumeuacha miji yetu haiwezi kuwa misafi.

Kwa hiyo, uvundo madhali tumo wanaadamu utaendelea kuwepo kama hatutajirekebisha. Natoa wito kwa wakaazi wa mji na vijiji turudishe utamaduni wa kusafisha maeneo yetu. Nakubali kwamba Baraza la Manispaa linao wajibu wa jumla, lakini lina maeneo ya kuchukulia taka na hili amelizungumza Mhe. Mgeni Hassan Juma, nitalitolea ufafanuzi kwa nini mji unaendelea kuwa mchafu na magari yamepatikana. Nitaendelea kulitolea ufafanuzi baadae lakini kwanza niliona nilizungumzie hili la uchafu wa mji na namna ya kubadilisha tabia.

Limezungumzwa pia suala la vituo vya daladala. Sasa ndio utaratibu wenyewe huo. Kwamba mtu wa daladala leo akichukuliwa hatua anamtafuta Mwakilishi amuulizie suala kwa nini wanasumbuliwa. Mfanyabiashara anaefanya biashara kinyume na taratibu anamtafuta Mwakilishi amuulizie swali. Sasa ninaposema tubadilikeni lazima sote tuwajibike katika hili. Anapokosea mtu, ninapojiwa mimi Mwakilishi wa Tumbatu mfanyabiashara, mwananchi wangu, wa Jimbo la Tumbatu anafanya biashara Darajani kinyume na taratibu nimwambie hapo unafanya biashara kinyume na taratibu. Tusipofanya hivyo maana yake bado hatujakubali mji wetu uendelee kuwa na nidhamu ya usafi.

Kwa nini mjini kunakuwa kuchafu na magari yamekuja. Lazima tukubali kwamba tunazo changamoto nyingi kama nilivyowahi kusema hapa, kwamba hivi sasa tumepokea magari yale kutoka *World Bank*. Lakini yale magari ni ya

kuchukulia taka, lakini kuna magari ambayo yanatakiwa yanyanyue zile kontena kuweka kwenye magari. Hayo magari bado hayajafika tunatarajia saa yoyote kuanzia sasa yatafika, basi ufanisi wa uchukuwaji wa taka kutoka mjini kupeleka kwenye jaa kubwa utapatikana.

Lakini jambo jengine kuna wafanyakazi wengi sana wameshakuwa wazee na afya zao haziridhishi. Hivi sasa wote hao tumewapeleka Wizara ya Afya kujua historia ya afya zao zikoje na tutakuja kuchukua hatua na kuona kwamba huyu hana uwezo wa kuweza kufanya kazi hizi, nitakuombeni sana Waheshimiwa Wawakilishi msije kupiga hodi ofisini kwangu. Tunataka tuwaondoe hao na tuweke vijana ambao wana uwezo wa kuweza kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Spika, limezungumziwa suala la Boti za Uokozi. Tulichoripoti ni boti za kufanyia doria na hatujaripoti boti za uokozi pale yanapotokea maafa. Isipokuwa kwa sababu ya ukosefu, hizo boti za doria huwa tunazitumia saa nyengine kwa kufanyia uokozi. Serikali inaendelea na mipango yake ya kuweza kupata hivi vifaa vya uokozi na vitakapopatikana basi tutaweza kuvifanyia kazi kama ilivyokusuidiwa.

Suala la mafuta tumeripoti kwamba hivi sasa kikosi chetu cha KMKM kimepata bajeti ya kupata mafuta ya kufanyia kazi zake za doria, na wala hatutegemei mafuta kutoka *ZSTC*. Mafuta haya yanatokana na bajeti ambayo tumeongezewa na tunaishukuru Wizara ya Fedha. Mafuta yanayotolewa *ZSTC* yanakwenda kwenye *task force* ya karafuu katika Ofisi za Mikoa. Na hili lilikuwa likizungumzwa lakini hata waziri muhusika mkimuuliza wa Biashara atakwambieni. Kwa sababu jukumu letu sisi ni la kawaida. Kwa hivyo, tuna bajeti yetu.

Maeneo ya kulala wanafunzi watoto. Nimesema kwamba tayari tumechukua hatua kwa eneo la Unguja na hivi sasa tunajitayarisha kuchukua hatua kwa eneo la Pemba. Kilichotucheleweshe kule Pemba ni sababu tu ya ule muundo wa lile Gereza lenyewe. Lakini sisi kwenye wizara kwa kushirikiana na chuo tunafanya maandalizi ya kuweza kuona hilo jambo tunalitatua ndani ya mwaka huu, ili watuhumiwa watoto au wanafunzi watoto waweze kuwa na eneo lao.

Mhe. Spika, kuhusu suala la Zimamoto Mkoa wa Kaskazini Pemba. Hili nimeona ni vizuri nikalitolea ufanunuzi. Mhe. Spika, wala watendaji wangu hawajakwambia uongo na waliposema nilikuwepo na mimi nikalitilia nyama. Na mimi nimefanya ziara Pemba, Mkuu wa Mkoa nilikuwa nae wakati ananionesha kituo cha muda alichowapa Kaskazini Pemba pale Wete. Hakuniambia kama kawapatia hayo ambayo wameyasema kikosi ni ya uongo.

Kwa hiyo, waliyoyasema Maofisa ni ya ukweli, na mimi mwenyewe nimeshiriki katika kwenda kuona hayo maeneo ambayo mwanzo zimamoto toka mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya katiba Sheria na Utawala. Walipewa eneo la Mchangamdogo na baadae eneo hilo wakaambiwa hawawezi kulipata tena na mimi shahidi. Maana na mimi nimekuwa Mwenyekiti wa kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa miaka 8.

Kwa hivyo, kwa kiasi fulani shughuli zinazofanyika katika Ofisi hizi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa na hizi nyengine ambazo sasa zinasimamiwa na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala nazifahamu. Hilo eneo kweli walitakiwa wapewe Zimamoto na baadae wakaambiwa hawapewi tena. Na eneo la Wete waliambiwa kweli watapewa lakini baadae wakabadilishiwa kibao. Sasa hatuji hapa kwa kusema mambo ya vichochoroni tu.

Sasa huyo Mkuu wa Mkoa aliekwambia hivyo ananisikia huko aliko. Aje akwambie hayo ambayo mimi alinambia yatafautiane na yale. Ilivyokuwa Kamati ya Katiba na Sheria ndio inayofuatilia utendaji wa kazi zetu tutaripoti tena kwenu. Lakini kadiri ninavyojua mimi taarifa ndizo hizo.
Sasa nani anaehusika akabadilisha hicho kibao sijui. Kwa hiyo, watendaji wangu hawajadanganya bwana, wamesema yale yaliopo. Nakubaliana na changamoto za mazingira ya askari na hili tutalifanyia kazi.

Jambo jengine ambalo limejitokeza Mhe. Spika, ambalo litakuwa la mwisho kwa leo ni suala la Sera na Sheria za Serikali za Mitaa. Kama nilivyosema sera iko tayari na juzi hapa nililia Mhe. Spika, nikakwambia kwamba tayari rasimu ya Sheria ya Serikali za Mitaa na Utawala wa Mikoa.

Tunatarajia hivi karibuni tutakwenda kwa wahusika wengine kwa maana ya ile lugha nyengine inaitwa nini? "Wadau". Miongoni mwa wahusika wengine ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Nataka nirejee tena niseme kwamba kwa umuhimu wa sheria hizi nitakuomba sana tutapokuja kuleta ombi, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi mtukubalie ili sheria hizi zipitishwe na ziweze kufanya kazi zake.

Baada ya kwisha kusema hayo Mhe. Spika, nikushukuru tena, niishukuru Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya Mwenyekiti wake mahiri kabisa chipukizi kwa ripoti yake. Nikushukuruni sana Waheshimiwa Wajumbe kwa maoni yenu ambayo mmetupa. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe tuna dakika kama tisa tu kumaliza muda. Nitafurahi kama mtasema tuendelee mpaka tumalize.

Waheshimiwa Wajumbe nilikuwa nafanya uchunguzi wa haraka haraka nijue kama tuko tayari au laa. Inaonekana hatuko tayari.

Basi kwa kuwa muda uliobakia ni mfupi na nafikiri itampa tabu kidogo Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria. Nachukuwa nafasi hii sasa nikushukuruni na naakhirisha kikao hiki hadi kesho tarehe 29/01/2014 saa 3:00 barabara asubuhi.

(Saa 1:37 usiku Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 29/01/2014 saa 3:00 asubuhi)